# Nipashe

Jumatano Desemba 25 , 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580110

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710




## Vyuo vyatakiwa kuunda madawati kupambana na ukatili wa kijinsia

UKURASA 3




UKURASA 13

# Magoti ashtakiwa kutakatisha fedha

**ADAIWA** kutumia mtandao kujipatia mil. 17.3/-, aunganishwa na mtaalamu wa Tehama LHRC...*Endelea ukurasa wa 2*



Mshtakiwa Tito Magoti (kushoto) na mwenzake, Theodory Faustin Giyan, wakiwa chini ya ulinzi wa askari polisi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

**VIGOGO 83% WAKACHA KUTOA MATAMKO YA MALI**
KAMISHNA wa Maadili, Jaji mstaafu Harold Nsekela, amesema hali ya utoaji wa matamko ya mali kwa viongozi wa umma sio nzuri kwani hadi Desemba 20...

**UKURASA WA 8**

**MINADA YOTE TRA SASA KUENDESHWA KIMTANDAO**
MAMLAKA ya Mapato nchini (TRA) imebadili utaratibu wa kuendesha minada yote iliyokuwa ikifanyika kwa njia ya hadhara na sasa kufanyika kwa mfumo wa mtandao...

**UKURASA WA 26**

**CUF YAIBUKA NA OPERESHENI 2020**
CHAMA cha Wananchi (CUF), kimesema kitazindua operesheni mpya kiliyoipa jina la '2020 Mwaka wa Demokrasia na Maridhiano ya Kisiasa...


## MOSHI YAJAA WAGENI KRISMASI

UKURASA 12

# Nida hakuna kulala utoaji vitambulisho

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play · App Store



**MICHEZO** SIMBA YAPANIA KUENDELEZA DOZI UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Magoti ashtakiwa utakatishaji fedha

**Na Hellen Mwango**

OFISA Elimu kwa Umma wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Tito Magoti (26) na Mtaalamu wa Tehama, Theodory Gyan (36), wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jana, jijini Dar es Salaam wakikabiliwa na mashtaka matatu likiwamo la utakatishaji fedha Sh. milioni 17.3.

Magoti ambaye alikamatwa Desemba 20, mwaka huu, alifikishwa mahakamani akiwa na mwenzake.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Janeth Mtega.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na jopo la mawakili wanne, Mawakili wa Serikali Wakuu, Paul Kadushi, Faraja Mchimbi, Renatus Mkude na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon.

Wankyo alidai kuwa washtakiwa wote, katika tarehe tofauti kati ya Februari Mosi na Desemba 17, 2019 ndani ya Jiji la Dar es Salaam na mahali tofauti nchini Tanzania, kwa pamoja na watu ambao hawapo mahakamani kwa makusudi walishiriki kutenda makosa ya kiuhalifu ya kumiliki programu ya kompyuta iliyotengenezwa mahusus kufanya kosa la jinai na kuwawezesha kujipatia Sh. 17,354,535.

Nchimbi alidai katika tarehe tofauti kati ya Februari Mosi na Desemba 17, 2019, ndani ya jiji na Mkoa wa Dar es Salaam kwa pamoja washtakiwa hao na wengine ambao hawapo mahakamani, walimiliki programu ya kompyuta iliyotengenezwa mahususi kwa ajili ya kutenda makosa ya jinai.

Mkude alidai katika shtaka la tatu, inadaiwa kuwa kati ya Februari Mosi na Desemba 17, 2019, jijini Dar es Salaam washtakiwa hao kwa pamoja walitakatisha na kujipatia Sh. 17,353,535 wakati wakijua mapato hayo yametokana na zao la kosa la kushiriki genge la uhalifu.

Hata hivyo, washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo ya uhujumu uchumi mpaka ipate kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Mshtaka nchini (DPP) au upelelezi utakapokamilika, itahamishiwa Mahakama Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika hivyo wanaomba tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa.

Hakimu Mtega alisema kesi hiyo itatajwa Januari 7, 2020.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika.



Magari yakikwama kuendelea na safari jana, baada ya madereva wake kushindwa kupishana kwenye barabara ya Sewa, Mikocheni Dar es Salaam ambayo ipo katika ukarabati mkubwa. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Nida hakuna kulala utoaji vitambulisho

**Na Maulid Mmbaga**

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) imetangaza kuongeza kasi ya utoaji wa huduma ya usajili na utambuzi wa watu na ugawaji wa namba za utambulisho wa taifa ili kuwawezesha wananchi kupata fursa ya kusajili laini za simu kwa alama za vidole.

Taarifa iliyotolewa na Nida jana ilisema huduma hiyo itatolewa kila siku katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam.

Mkuu wa Mawasiliano na Hifadhi Hati wa mamlaka hiyo, Thomas Nyakabengwe, alisema namba na vitambulisho vitatolewa katika eneo tajwa kuanzia saa 2:00 asubuhi na kufunga 11:00 jioni hadi Desemba 31, mwaka huu.

Alisema huduma ya utoaji wa Namba za Utambulisho wa Taifa (NIN) inatolewa pia kwa Watanzania wote katika mikoa husika.

"Usajili huu kwa kupigwa picha, kuweka saini ya kielektroniki na kuchukuliwa alama za vidole, inatolewa kwa wakazi wa mkoa wa Dar es Salaam tu," alisisitiza Nyakabengwe.

Aliongeza kwamba wakazi kutoka mikoa mingine wanaohitaji huduma ya usajili watatakiwa kufika katika ofisi za Nida katika wilaya wanazoishi.

"Sherehekea Krisimasi na Mwaka Mpya ukiwa na namba ya utambulisho wa Taifa (NIN) ili usajili laini yako ya simu na kupata huduma nyingine," alisema Nyakabengwe katika taarifa hiyo.

Juzi, serikali ilisisitiza kuwa haitaongeza muda wa kusajili laini za simu kwa alama za vidole ifikapo Desemba 31 kama ilivyotangaza awali.

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, alisema suala hilo si la masihara na kwamba muda utakapofika watazifungia laini zote ambazo zitakuwa hazijasajiliwa kwa alama za vidole.

"Desemba 31 tunakamilisha usajili na tutafungia laini zote ambazo zitakuwa hazijasajiliwa. Niwaambie umuhimu wa jambo hilo. Tumefanya hivi kwa sababu Watanzania wengi wanaibiwa fedha zao kutokana na utitiri wa laini." Wakati Nida ilitoa taarifa hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa TCRA, James Kilaba, alisema tayari watu milioni tatu wana namba za usajili za Nida lakini hawajajitokeza kujisajili.

Pia alisema jumla ya laini zilizokuwa zimesajiliwa hadi Desemba 10, mwaka huu, laini zilizosajiliwa kwa alama za vidole zilikuwa 19,681,060 sawa na asilimia 42 zinazomilikiwa na watu milioni 7.6. Mei Mosi, mwaka huu, TCRA ilianza rasmi kazi ya usajili wa alama za vidole kwa kushirikiana na kampuni za simu za mikononi na kazi hiyo itafungwa rasmi Desemba 31 saa 6:00 usiku na mtumiaji wa simu ambaye hatajisajili laini yake itakuwa imefungwa rasmi.

## Vigogo 83% wakacha kutoa matamko ya mali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAMISHNA wa Maadili, Jaji mstaafu Harold Nsekela, amesema hali ya utoaji wa matamko ya mali kwa viongozi wa umma sio nzuri kwani hadi Desemba 20 ni asilimia 17 tu ambayo ni sawa na viongozi 2,369 ndio wametekeleza sheria hiyo, huku asilimia 83 wakishindwa kufanya hivyo. Akizungumza na waandishi wa habari jana, Jaji Nskela alisema kati ya viongozi wa umma 13,699 wanaotakiwa kuwasilisha tamko kwa kamishna wa maadili ni viongozi 2,369 ambao wametekeleza agizo hilo.

Alifafanua zaidi kuwa bado viongozi wa umma 11,330 (sawa na asilimia 83) hawajawasilisha matamko.

"Naomba viongozi watekeleze agizo hilo kwa sababu ni sheria ambayo imewekwa na Bunge, ni lazima itekelezwe," alisema Jaji Nsekela. Alisema sekretarieti haina mamlaka ya kusogeza mbele muda wa kuwasilisha tamko la mali, hivyo kila kiongozi ambaye anaguswa na Sheria ya Maadili Namba 13 ya Mwaka 1995 kupitia fungu la 9 (1) (a )-(c) ambalo linamtaka kila kiongozi wa umma aliyetajwa

katika kifungu cha nne kuhakikisha anampelekea kamishna tamko la maandishi katika hati rasmi. Alisema kuanzia jana imebaki wiki moja, hivyo kuwataka viongozi hadi kufikia muda uliowekwa kila mmoja awe ametekeleza. Alifafanua kuwa sheria ya maadili ya viongozi haiwataki tu viongozi wa umma kuwasilisha matamko yao ya rasilimali na madeni, bali inawataka kutoa taarifa za kweli ndani ya matamko yao.

Aidha, alisema kutoa tamko la uongo ni kosa chini ya fungu la 27 (2) ambalo linasema kiongozi yeyote wa umma anayetoa tamko la uongo kuhusu rasilimali zake atakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani atatozwa faini ya Sh. milioni moja na si zaidi ya Sh. milioni tano au kifungo cha mwaka mmoja.

Alisema viongozi wote wanapaswa kuzingatia makatazo

hayo ya kisheria kabla ya kuwasilisha matamko yao kwa kamishna wa maadili. Alisema viongozi watakaoshindwa kutekeleza matamko hayo watafikishwa katika Baraza la Maadili kujieleza ili kuchukuliwa hatua stahiki.

Alisema wamekuwa wakifanya utaratibu huo kila mwaka, hivyo haoni sababu ya watu hao kushindwa kufanya urejeshwaji wa matamko ya mali na madeni ya viongozi wa umma.

Katika hatua nyingine, alisema kuanzia mwakani wataanza kutumia njia ya mtandao kupokea matamko ya urejeshwaji mali na madeni ya viongozi wa umma ili kuwarahisishia wanaohusika kukamilisha kwa wakati.



Naibu Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), George Kuchio (kushoto), akimweleza jambo Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Faraji Mnyepe, wakati wa mazungumzo katika ofisi ndogo za wizara hiyo, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madawati jinsia kuanzishwa kudhibiti rushwa ya ngono



**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Francis Michael (pichani), ameagiza menejimenti za vyuo vya elimu ya juu kuanzisha madawati ya jinsia.

Ametaka kufanya hivyo ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alilolitoa wakati akifungua Kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia.

Dk. Michael ameyasema hayo jana jijini hapa wakati akifunga kikao kilichowakutanisha wakuu wa vyuo vya elimu ya juu kilichojadili namna ya kupambana na ukatili wa kijinsia ikiwamo rushwa ya ngono katika taasisi hizo.

Alisema ukatili wa kijinsia umekuwa ukishamiri katika vyuo vya elimu ya juu, hivyo kuzitaka menejimenti za vyuo hivyo kuweka mikakati ya kupambana na ukatili wa kijinsia kwa upana wake.

Menejimenti za vyuo, alisema zina wajibu wa kuhakikisha vyuo husika vinatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa kanuni, sheria na taratibu kwa kuhakikisha wanazalisha wataalamu bora na wenye weledi wa kutosha ili kulisaidia taifa katika kuleta maendeleo.

"Mkatekeleze maagizo haya na nitafuatilia kuona mmefikia wapi. Hatuwezi kuvumilia masuala haya hata kidogo kwani yanaharibu picha ya vyuo vyetu na taifa," alisema.

Pia aliwataka wakuu wa vyuo kuhakikisha watumishi wao wanafanya kazi kwa kuzingatia kanuni na sheria zilizopo kwa kuwa waadilifu na kuhakikisha wanaepukana na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na wanaume ikiwa ni ukatili wa kihisia, kimwili au ukatili wa kimtandao.

Dk. Michael aliwataka wakuu wa vyuo hao kuhakikisha wanafunzi wa watumishi wanatii sheria na kanuni zilizopo ili kuwezesha taasisi za elimu ya juu kutimiza malengo waliyojiwekea kwa ufanisi mkubwa na kuondokana na vitendo vya kikatili kwa kujenga mazingira yaliyo salama katika vyuo hivyo.

Naye Ofisa Mwandamizi Mkuu kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania TCRA, Semu Mwakyanjala, alisema taasisi hiyo imejipanga kupambana na ukatili wa kijinsia hasa wa mitandaoni.

Katika kupambana na vitendo hivyo, alisema tayari baadhi ya watuhumiwa wameshafikishwa mahakamani kutokana na kufanya vitendo vya kikatili mitandaoni kwa kuweke picha na maudhui yasiyofaa na yanayoumiza watu kihisia.

# Asomewa mashtaka amelazwa hospitalini

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA Maiko Mrina (67), amesomewa mashtaka katika wodi ya Taasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI), anakopata matibabu anayokabiliwa na wenzake wawili dhidi ya kuisababishia serikali hasara ya zaidi ya Sh. milioni 30.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Dereva Ally Athumani (36) na mlinzi Shabani Rashidi (57), ambao walisomewa mashtaka yao katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Vicky Mwaikambo.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Mkude Mshanga akisaidiana na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon na Wakili wa Serikali, Grory Mwenda.

Mshanga alidai kuwa Agosti 29, 2018 eneo la Ubungo jijini Dar es Salaam, mshtakiwa Athumani akiwa mwajiriwa wa Kampuni ya China Civil Engineering Contraction Corporation, anadaiwa kuiba tani nane za nondo zenye thamani ya Sh. 35,405,390, mali ya kampuni hiyo, zilizofika kwake kutokana na wadhifa wake.

Katika shtaka la pili ilidaiwa, kati ya Agosti 29 hadi 30, 2018, jijini Dar es Salaam, washtakiwa wote kwa nia ovu waliisababishia serikali hasara ya Sh. 30,405, 390.

Katika shtaka la tatu, ilidaiwa kwamba, Agosti 29, 2018, washtakiwa wote walitakatisha fedha hizo wakati wakijua ni zao la kosa la wizi.

Upande wa mashtaka ulidai, upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika na kesi iliahirishwa hadi Januari 7, 2020 kwa ajili ya kutajwa.

Washtakiwa walirudishwa rumande kwa sababu mashtaka ya kutakatisha fedha hayana dhamana.



HABARI KITAIFA

# Kabudi asifu uhusiano Tanzania, Uturuki

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, amekutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Uturuki nchini Tanzania, Ali Davutaglu, katika ofisi ofisi ndogo za wizara, jijini Dar es Salaam.

Waziri Kabudi amemweleza Balozi Davutaglu kuwa uhusiano kati ya Tanzania na Uturuki ni wa muda mrefu na uko imara.

"Ushirikiano wa Tanzania na Uturuki ni wa muda mrefu na ni imara kwa kweli, pamoja na mambo mengine uhusiano huu umekuwa ukijikita kuendeleza uwekezaji wa viwanda, elimu na utalii hasa katika kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania kwenyea Shirika la Ndege la Uturuki," alisema Prof. Kabudi.

Pia, alisema uhusiano wa Tanzania na Uturuki ni imara na kutaka kuuendeleza na kuuimarisha kwa kuwekeza katika sekta mbalimbali mfano sekta ya biashara na uwekezaji. "...naamini tukiwekeza katika viwanda hasa vya nguo hapa nchini ni fursa ambayo itaiwezesha taifa la Tanzania kupata bidhaa nzuri na imara," alisema Prof. Kabudi.

Balozi wa Uturiki nchini Tanzania, Davutaglu kwa upande wake alisema kuwa Uturuki ni nchi inayoheshimu taratibu za nchi na ni marafiki wazuri na wa siku nyingi hivyo ataendelea kuhakikisha kuwa malengo ya serikali yanasonga mbele ili kuiwezesha Tanzania kuwa na maendeleo endelevu.

"Uwekezaji ni muhimu sana kwa nchi zetu hizi mbili na tayari nimeshawasiliana na umoja wa wasafirishaji na mawakala wa utalii Uturuki ili waweze kutembelea Tanzania pamoja na kuangalia fursa za uwekezaji kwa lengo la kuwekeza na hatimaye kukuza sekta hizi na uchumi wa mataifa haya mawili," Alisema Balozi Davutaglu.




Taka zinazozalishwa na wafanyabiashara wa soko la Kawe, jijini Dar es Salaam, zimesababisha barabara kuwa finyu baada ya kutozolewa kwa muda mrefu, kama zinavyoonekana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Serikali yaitaka UNHCR kuheshimu mapatano

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imelitaka Shirika la Msalaba Mwekundu Tanzania (TRCS), kuendelea kutoa huduma za matibabu katika kambi za wakimbizi mkoani Kigoma.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Faraji Mnyepe, alitoa msimamo huo alipokutana na kufanya mazungumzo na Naibu Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), George Kuchio, katika ofisi ndogo za wizara, jijini Dar es Salaam.

Aidha, Dk. Mnyepe aliitaka UNHCR kuzingatia na kuheshimu makubaliano baina yake na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1991 hususani Ibara ya pili na ya tatu, zinazoelekeza UNHCR kushirikiana na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutekeleza majukumu yake nchini.

Hivi karibuni UNHCR ililitaka Shirika la Msalaba Mwekendu kukabidhi majukumu yake bila kuihusisha serikali, hatua ambayo inavunja makubaliano ya 1991.

Aliieleza UNHCR kwamba Shirika la Msalaba Mwekundu Tanzania litaendelea na majukumu yake kwa kuzingatia makubaliano yaliyopo mpaka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na UNHCR watakapokubaliana vinginevyo.


**KUPOTELEWA NA KADI YA TRAILLER**

VANILLA ENTERPRISES CO LTD anatangaza kupotelewa na kadi ya Trailler aina ya simba model yenye namba za usajili T 249 BHC. Chassis No. ST 037 9233.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi ARU/ARU/RB/581659/2019.


# Kilo milioni 19.2 korosho zakusanywa Tunduru

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

JUMLA ya kilo 19,249,302 za korosho zimekusanywa kutoka kwa wakulima wilayani Tunduru mkoani Ruvuma na kupelekwa katika maghala makuu kwa ajili ya kuuzwa kupitia utaratibu wa mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kilo 17,739,088 zenye thamani ya Sh. 47,943,367,584.00 zimeshauzwa kupitia minada saba iliyofanyika wilayani humo na fedha za malipo ya wakulima kwa minada mitano yameshafanywa kwa wakulima.

Hayo yalisemwa na Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika Wilaya ya Tunduru (TAMCU), Imani Kalembo, alipokuwa akitoa taaifa ya mauzo ya zao hilo kwa Mkuu wa Wilaya ya Tunduru.

Kalembo alifafanua kuwa takwimu zinaonyesha kuwa korosho ambazo zimebaki katika maghala makuu hadi Desemba 22, mwaka huu ni kilo 1,510,214 ambazo zipo tayari kuuzwa katika mnada wa 8 unatarajiwa kufanyika mwishoni mwa wiki hii.

Naye Mwenyekiti wa TAMCU, Hashim Mbalambala, alisema takwimu hizo zinazonyesha kuwapo kwa ongezeko la uzalishaji wa zao hilo katika msimu wa mwaka 2019/2020.

Alisema awali chama kikuu kilikisia uzalishaji wa kilo milioni 23, lakini kutokana na makusanyo yao kufikia kilo 19,249,302, huku kukiwa na korosho nyingi kwa wakulima, kunaonyesha chama hicho kuvuka malengo hayo.

Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, aliwataka viongozi wa vyama vya msingi kuzungumzia juhudi za kutoa elimu kwa wakulima ili uzalishaji huo ulete maendeleo kwa wakulima.

**Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kilo 17,739,088 zenye thamani ya Sh. 47,943,367,584.00 zimeshauzwa kupitia minada saba iliyofanyika wilayani humo na fedha za malipo yameshafanywa....**

HABARI KITAIFA



Mkurugenzi wa Jiji la Arusha akionyesha waandishi wa habari baadhi ya madawati yaliyokamilika. **PICHA WOINDE SHIZZA**

# DC aagiza daktari kusimamishwa kazi

**Na Gurian Adolf,** KATAVI

MKUU wa Wilaya ya Mlele mkoani Katavi, Rachael Kasanda, ameagiza kusimamishwa kazi mara moja Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Inyonga, Calvin Mnaso, kwa tuhuma za kuiba dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 2.4.

Pia ameagiza mganga huyo aondolewe kwenye nyumba anayoishi ambayo ni mali ya kituo hicho na ufanyike msako kwenye nyumba za watumishi wote wanaoishi kwenye maeneo ya karibu na kituo, ili kujiridhisha kama hawana tabia ya kuiba dawa kwenye bohari na kuficha kwenye nyumba zao.

Kasanda alitoa agizo hilo jana wakati alipokuwa akizungumza na wafanyakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele ofisini kwake. Kikao hicho kilihudhuriwa na wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama wa wilaya hiyo.

Alisema serikali imeongeza bajeti ya dawa na vifaa tiba, lakini anasikitika kuona baadhi ya watumishi wa afya wamekuwa si waaminifu kwa kuwa na tabia ya kuiba dawa na vifaa tiba kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali.

Mkuu huyo wa wilaya alisema katika wilaya yake kwenye kituo cha afya Inyonga hivi karibuni, mganga wa kituo hicho alikamatwa akiwa na dawa mbalimbali na vifaa tiba vya kutibia binadamu vikiwa ndani ya nyumba anayoishi.

Mmaso alikamatwa baada ya uongozi wa wilaya kupata taarifa kutoka kwa wananchi, ndipo alipoliagiza Jeshi la Polisi kufuatilia tuhuma hizo na polisi walifika nyumbani kwake kufanya upekuzi na kumkuta akiwa na maboksi matano yaliyakuwa na dawa mbalimbali za binadamu.

Mkuu huyo wa wilaya alivitaja vifaa vilivyokamatwa kwenye nyumba ya mganga huyo kuwa ni vifaa vya upasuaji, vya kufanyia tohara, godoro moja, sindano na dawa mbalimbali zinazotumika kutibu binadamu pamoja na vyandarua ambavyo huwa wanagawiwa wajawazito wanapohudhuria kliniki.

Vifaa hivi vyote ni mali ya serikali ambavyo viligawiwa kwa ajili ya kituo cha afya Inyonga na vina thamani ya Sh. 2,460,000, dawa na vifaa hivyo kwa mujibu wa sheria hakupaswa kuwa navyo ndani ya nyumba yake.

Kutokana na mtuhumiwa huyo kukamatwa na vitu hivyo, Kasnada alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele, Alexius Kagunze, kumwandikia barua ya kumsimamisha kazi mganga huyo kwa kuwa ndiye mwenye mamlaka ya kuandika barua.

Kagunze alisema maagizo hayo ya Mkuu wa Wilaya ameyapokea na atayatekeleza kwa wakati.

# Raia wa China kizimbani madai ya uhujumu uchumi

**Na Hellen Mwango**

RAIA wa China Zhang Chuanqi, amefikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, akikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kukutwa na vipande 12 vya madini ghafi aina ya amethisto vyenye thamani ya zaidi ya Sh. 800,000 aliyokuwa akiyasafirisha bila kibali.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka yake jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Salum Ally.

Wakili wa Serikali, Janeth Magoho, alidai kuwa Desemba 14, mwaka huu, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), mshtakiwa alikutwa na madini hayo yenye uzito wa gramu 239 kinyume na Sheria ya Madini.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa mshtakiwa huyo alikosa mkalimani wa kutafsiri lugha ya Kichina kwenda Kiingereza na Kiswahili ili aweze kufahamu mashtaka yanayomkabili.

Wakili wa utetezi, Kelvin Makebula, alikubaliana na hoja ya upande wa mashtaka na kudai kuwa tayari wameanza mazungumzo na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) kuhusiana na kesi hiyo.

Hakimu Ally alisema mahakama yake imesikiliza hoja ya upande wa Jamhuri kuiahirisha kesi hiyo mpaka mtuhumiwa atakapopata mkalimani.

Kesi hiyo imeahirishwa mpaka Desemba 27, mwaka huu na mshtakiwa amerudishwa rumande.


The Guardian Nipashe

Two Unbeatable Deals In One Place

Free Delivery at Your Door Step + more Than 20% Off On 1 Year Upfront Subscription.

Merry Christmas

| Number Of Dailies | Cover Price (Tsh) | Offer Price (Tsh) | Your Saving (Tsh) |
|---|---|---|---|
| 1 Month | 26,000 /= | 24,000 /= | 2,000 /= |
| 3 Months | 79,000 /= | 70,000 /= | 9,000 /= |
| 6 Months | 157,000 /= | 130,000 /= | 27,000 /= |
| 1 Year | 314,000 /= | 250,000 /= | 64,000 /= |

Please mention the start date from when you want to receive your subscription

**For enquiry,** Please contact Subscription Supervisor - **Mr Pastory Massawe**

+255 719 063 770

Email: subscription@guardian.co.tz

Offer valid from 16th Dec 2019 to 15th Jan 2020

Terms & Condition Apply.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Siku zilizobaki zitumike ipasavyo usajili wa simu

**HATIMAYE** muda uliotolewa na serikali kwa wamiliki wa laini za simu kuzisajili kwa mfumo wa alama za vidole umefikia ukingoni.

Ni ukingoni kwa sababu zimebaki siku saba kuanzia leo hadi siku ya mwisho ambayo ni Desemba 31.

Sharti la kusajili laini ya simu ni kwamba mmiliki anatakiwa kuwa na kitambulisho cha taifa. Kwa lugha nyingine ni kwamba hakuna mmiliki wa laini ya simu anayeweza kuisajili bila kuwa na kitambulisho cha taifa.

Kutokana na hali hiyo, ndiyo maana serikali imekuwa ikiwahimiza wananchi kujiandikisha kwa ajili ya kupata vitambulisho vya taifa kutokana na umuhimu wake, ikiwamo kuvitumia kusajili laini za simu.

Hata hivyo, licha ya kuripotiwa taarifa mbalimbali kwamba kwenye maeneo kadhaa nchini wananchi wengi hawajapata vitambulisho vya taifa, hivyo kukwama kusajili simu zao, lakini kwa wale ambao wamepata vitambulisho hivyo au namba hawanabudi kuzitumia siku chache zilizobakia kusajili laini zao za simu.

Haiingii akilini kusikia kuwa maelfu ya wananchi hawajasajili laini zao wakati umebakia muda mfupi.

Inawezekana wapo wanaokwazwa na kutokuwa na vitambulisho au namba za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), lakini pia wapo wale ambao wana tabia ya kujitokeza siku za mwisho na kusababisha usumbufu mkubwa hususan misongamano katika maeneo ya kusajili laini za simu.

Usajili wa laini za siku kwa mfumo wa alama za vidole ni muhimu kwa sababu bila kusajili laini simu itazimwa na mmiliki atakosa huduma muhimu kama mawasiliano na kufanya miamala.

Ili kuepukana na athari hizo, ni vyema kila mmiliki wa simu kwenda kusajili laini katika ofisi za kampuni za simu na za mawakala ambazo zinaendelea kutoa huduma hiyo.

Wapo wanaodhani kuwa serikali itaongeza muda. Hata hivyo, serikali imeeendelea kusisitiza kuwa muda hautaongezwa, na ikifika Desemba 31 laini zote ambazo hazijasajiliwa kwa kwa mfumo wa alama za vidole zitazimwa.

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, juzi alisema kuwa amebakiza siku nane kutekeleza uamuzi huo wa serikali.

Kamwelwe alisema hakuna tatizo linalowazuia watu washindwe kusajili, na kwamba watakaoshindwa kufanya hivyo, watakuwa wamekaidi, hivyo watakosa mawasiliano.

Alisisitiza kuwa suala hilo si la masihara, na badala yake watazifungia laini zote ambazo zitakuwa hazijasajiliwa kwa alama za vidole.

Wiki iliyopita, Mkurugenzi Mtendaji wa Mmlaka ya Mawasiliano TCRA, James Kilaba, alisema watu milioni tatu wana namba za usajili za Nida lakini hawajajitokeza kujisajili.

Alisema kati ya watu hao wenye namba za vitambulisho, wanatarajiwa kusajili laini milioni 5.6 kwa sababu mtu mmoja anamiliki zaidi ya laini moja.

Aidha, laini zilikuwa zimesajiliwa hadi Desemba 10, mwaka huu, zilikuwa 47,063,603, ambazo zinamilikiwa na watu milioni 21.1. Idadi ya laini zilizosajiliwa kwa alama za vidole zilikuwa 19,681,060 sawa na asilimia 42 zinazomiliwa na watu Sh. milioni 7.6.

Ni matarajio yetu kuwa ifikapo Desemba 31 kila mmiliki wa laini ya simu ambaye ni makini kwa kuelewa athari za kuzimiwa simu atahakikisha anajitokeza kusajili kabla ya muda uliopangwa.

Kwa wananchi ambao wameshindwa kupata vitambulisho na mamba za Nida kwa sababu za msingi, tunaamini kuwa serikali itaangalia njia nzuri za kuwasaidia wapate namba au vitambulisho ili wasajili laini na waendelee kupata huduma za mawasiliano.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Raphael Kibiriti

# Wakulima kufanywa daraja la mapato halmashauri liangaliwe

**LIKIZO** aliyoifanya Muungwana hivi karibuni katika mkoa wa Simiyu, Wilaya ya Maswa, imezidi kumfumbua macho zaidi juu ya changamoto ambazo bado wakulima na hasa wadogo wanakumbana nazo.

Na hiyo ni pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na serikali ya awamu ya tano zikilenga kuhakikisha kwamba, maslahi ya kundi hilo miongoni mwa Watanzania takribani milioni 55, sasa yanalindwa kwa udi na uvumba.

Ni katika ile dhima ya kuhakikisha jasho lao wanalolitoa kwenye uzalishaji wa shughuli hiyo muhimu kwa uchumi wa nchi, linawafaidisha kupitia pamoja na mengine, bei nzuri sokoni ya mazao wanayozalisha. Kwamba haiishii katika suala la bei nzuri sokoni, lakini pia hata kwenye mahitaji yao mengine yanayoboresha kilimo chao, kama huduma za ughani, pembejeo kwa maana ya bei nzuri ya mbegu, mbolea, dawa, huku upatikanaji ukiwa hauna mazonge.

Muungwana anasema kwa changamoto alizozishuhudia, bado Rais John Magufuli na wasaidizi wake wakuu, Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa wana kazi kubwa ya kufanya katika dhamira yao ya kuona ustawi wa wakulima nchini.

Likizo hiyo imemfumbua macho Muungwana kuona ukweli kwamba kumbe bado wakulima ni mtaji na chanzo kikubwa kwa baadhi ya halmashauri nchini ambazo huvuna fedha isivyo kihalali kutoka kwa mauzo ya mazao yaliyofanywa na wakulima.

Changamoto kubwa ambayo Muungwana ameipigia kelele kwa muda mrefu ilikuwa ni ya wakulima wa pamba na hasa Kanda ya Ziwa kutolipwa fedha zao toka walipouza pamba yao msimu uliomalizika karibuni.

Kwamba kuna wakulima ambao walikuwa hawajalipwa fedha kwa zaidi ya miezi minne toka walipouza pamba, kisha ikachukuliwa na kampuni za ununuzi wa zao hilo maeneo mbalimbali nchini. Ni vyema kwamba ahadi ya serikali kuwa wakulima wote wanaodai fedha zao watalipwa ifikapo Desemba hii imetekelezwa kwa sehemu kubwa na Muungwana ni shuhuda wa hili katika kijiji alikokuwa likizo.

Lakini si katika kijiji hicho, lakini hata kwenye vijiji vya jirani, wilaya na mkoa karibu wote wa Simiyu bila kusahau mikoa jirani ya Shinyanga, Mwanza na Geita, ambako nako ana taarifa za uhakika kwamba wakulima wamelipwa fedha zao.

Pamoja na serikali kusimamia hilo na kampuni za ununuzi kulipa wakulima, bado utaratibu uliowekwa na baadhi ya halmashauri kwa madai ya kukusanya fedha za pembejeo walizochukua wakulima si muafaka kwa maoni ya Muungwana.

Kwa mfano Halmashauri ya Maswa ilielekeza kampuni za ununuzi kupeleka fedha walizokuwa wanadai wakulima wa pamba katika halmashauri hiyo, badala ya kuzipeleka moja kwa moja kwa Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS).

Sasa halmashauri ndiyo iliyokuwa inatoa maofisa wa kwenda kulipa wakulima ili waweze kukusanya fedha za pembejeo walizowakopesha wakulima msimu uliopita wa kilimo.

Muungwana hana shida na utaratibu huo, ingawaje ulikuwa unachelewesha fedha za wakulima bila sababu, shida yake ni kwamba makato ya pembejeo yaliyokuwa yakifanywa yalikuwa ni ya kukadiria, kwani hakukuwa na nyaraka zinazoonyesha mkulima husika alichukua nini na kwa kiwango gani. Hivyo kilichokuwa kikifanyika ni kwa maofisa hao kuangalia mkulima amepata shilingi ngapi na kisha kuamua akatwe kiasi fulani kutoka kwenye fedha zake na ilipotokea mkulima kupinga makato hayo, aliambiwa aache fedha zake, walipwe wengine.

Kwa 'usawa' huu ambapo mkulima alishakaa miezi akisubiri fedha hizo, hakuna mkulima kimsingi aliyekuwa tayari kuendelea kukataa makato hayo, zaidi ya kuyakubali kama yalivyokuwa yanabainishwa na maofisa wa halmashauri.

Matokeo yake wakulima wamekatwa fedha nyingi zaidi ya kile ilivyostahili kulipia mikopo ya pembejeo, hivyo halmashauri kufaidika kupitia mgongo wao.

Ni maoni ya Muungwana kwa serikali kwamba itupie jicho changamoto hii, ili wakulima wasiendelee kuwa daraja la halmashauri na watendaji wengine serikalini la kuvuna fedha isivyo kihalali kutoka kwao.

# Hii kero Mikese hadi lini?

**Ndugu Mhariri**

*SISI wananchi tunaoishi Kitongoji cha Ukomanga, Kijiji cha Fulwe, Kata ya Mikese, mkoani Morogoro tunaleta masikitiko yetu makubwa kwako ili wahusika wapate kulielewa hili tukitegemea kupatiwa ufumbuzi kabla ya hali ya sintofahamu haijatokea.*

*Masikitiko yetu makubwa/kero yetu kubwa ni juu ya uwepo wa baadhi ya makanisa katika kitongoji chetu na utaratibu wake wa uendeshwaji kwa kutofuata sheria, ambapo imefikia kuwa kero, mateso, adhabu na hata kukosa amani.*

*Baadhi ya kero hizo ni pamoja na upigaji kelele kwa kutumia spika kubwa ambazo hutoa muziki mkubwa usiku kucha na kila siku, mbaya zaidi, makanisa haya yapo katikati ya makazi ya watu.*

*Hali hiyo husababisha wagonjwa, watoto, wazee na wanafunzi kuteswa na kelele na hata kupelekea kutofanya vizuri kimasomo.*

*Aidha, miradi yao ya ufugaji wao wa nguruwe pasipo kufuata utaratibu, kwani hufuga katikati ya jamii na kuwaacha wakizurura ovyo, usafi mdogo na mabanda yanayopelekea kutoa harufu kali na isiyovumilika, hali ambayo inahatarisha afya zetu.*

*Sisi kama wanakitongoji tulishawahi kuwaita hawa wamiliki wa makanisa na kuwaeleza tena kiungwana tu juu ya haya tukitegemea kupata suluhu, na badala yake wakawa na majibu yasiyotarajiwa.*

*Wakatoa majibu kuwa wao wana kibali cha serikali na wataendelea bila mtu yeyote kuwasumbua. Ninauliza hivi kweli huu ndio utaratibu wa uendeshaji wa makanisa? Je, kwa majibu haya kuna amani hapa?*

*Haya malalamiko ya kero hizi tumezifikisha katika uongozi wa serikali ya kijiji, Ofisi ya Diwani, Kata ya Mikese lakini utekelezaji haupo.*


*Hivyo basi, kwa matumaini makubwa tuliyonayo kupitia gazeti lako pendwa, barua yetu wahusika wataiona na kulitatua hili kabla ya hali kuwa mbaya zaidi.*

**Ahsante ni sisi wanakitongoji, Ukomanga-Fulwe, Mikese.**


**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz


# Mfano huu ni wa kuigwa, kuboresha shule za umma




**Na Sabato Kasika**

KWA kawaida mafanikio katika elimu yanategemea ni namna gani wadau mbalimbali wanatekeleza wajibu wao kwa ajili ya kufikia malengo ya kuwaelimisha wanafunzi.

Wazazi na walezi ni miongoni mwa wadau wakubwa kwenye maendeleo ya elimu nchini, kwa kuchangia kwa hali na mali, katika kuboresha miundombinu ya shule za serikali kwenye maeneo yao.

Hata hivyo, kumekuwa na tatizo kwenye shule hizo, ambazo kimsingi ni za umma, kufuatia baadhi ya wazazi na walezi kutokuwa na mwamko wa kushiriki katika maendeleo ya shule hizo.

Unaweza kukuta shule ina matatizo, ambayo yangeweza kutatuliwa na wao, lakini wakawa wagumu kushiriki, katika kuyatafutia ufumbuzi, kwa kudai kwamba hiyo ni kazi ya serikali.

Kwa shule za umma, wazazi na walezi wasiishie kufuatilia maendeleo ya watoto wao tu, bali wajue kuwa shule hizo ni zao, wanatakiwa kushiriki kikamilifu katika kutatua matatizo yanayozikabili.

Unaweza kukuta shule zinakabiliwa na ubovu wa miundombinu ya madarasa, vyoo na mingine, ambao unaweza kutafutiwa ufumbuzi na wazazi na walezi, lakini wengine hawako tayari katika hilo.

Watu wenye mawazo ya aina hiyo hawana budi kubadilika na kutambua kwamba mchango wao ni muhimu kwenye maendeleo ya shule za umma, ambazo kimsingi ni zao.

Wazazi, walezi na wadau wengine wa elimu, wana wajibu wa msingi wa kuhakikisha watoto wao wanasomea katika mazingira stahiki, hivyo ni muhimu washiriki kuboresha miundombinu ya shule za umma.

Kwa wale wanaotambua hilo, wamekuwa wakibuni mbinu mbalimbali za kuwawezesha kuboresha miundombinu ya shule katika maeneo yao, lengo likiwa ni kuhakikisha watoto wanasomea katika mazingira mazuri.

Wakazi wa kijiji cha Mwiringo, Kata ya Busambara, Musoma Vijijini, ni miongoni mwa wale, ambao wanatambua umuhimu wa kushiriki katika kuboresha miundombinu ya shule kwa manufaa ya watoto wao. Desemba 20 mwaka huu walijiwekea malengo ya kuongeza kasi ya maendeleo ya shule yao na ya kijiji kwa ujumla kwa kushirikiana na serikali kutekeleza miradi yao ya maendeleo.

Ilikuwa ni katika Jubilee ya miaka 50 ya shule hiyo, iliyoshirikisha walimu waanzilishi wa shule hiyo, wale wote waliowahi kusoma hapo na wanakijiji ambao kwa pamoja waliweka mikakati ya kuiboresha.

Wadau hao wa elimu, walikubaliana kuendelea kuboresha miundombinu ya shule hiyo na sasa wanachanga fedha za kukamilisha ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi ya walimu.

Mbali na kuchangia shule hiyo ya msingi, michango mingine ni kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vyoo vya wavulana, katika Shule ya Sekondari Busambara, ambayo ni mpya.

Iwapo mfano huu utaigwa na watu wote nchini, unaweza kusaidia kupunguza kama si kumaliza kabisa matatizo yanayozikabili shule za umma za msingi na sekondari, ambayo yako ndani ya uwezo wa jamii.

Ikumbukwe kuwa dunia ya leo inahitaji ushirikiano, hivyo suala la elimu bora inayopatikana katika mazingira bora, linahitaji jamii kuhusika kwa njia moja au nyingine na siyo kuiachia serikali kila kitu.

Kinachotakiwa ni viongozi wa ngazi zote kuendelea kuwahamasisha wazazi na walezi, ambao bado hawajatambua kuwa wanatakiwa kushiriki kwa hali na mali kwa ajili ya maendeleo ya shule wajue hilo.

Wananchi wanaweza kuwa na Jubilee kama hiyo iliyofanywa na wakazi wa kijiji cha Mwiringo kwa lengo la kuweka mkakati wa kushiriki, katika kuboresha miundombonu ya shule hiyo kongwe.

Kusubiri serikali ifanye kila kitu ni sawa na kukwamisha maendeleo ya shule, kwani ina mambo mengi ya kushughulikia, hivyo yale ambayo yako ndani ya uwezo wa wananchi, basi wayashughulikie.

Hilo linatokana na ukweli kwamba ni wajibu wa kila mwananchi kushiriki shughuli za maendeleo ya shule na ufuatiliaji wa karibu wa shughuli zote zinazofanyika shuleni, ili kumwezesha kila mtoto kupata elimu bora.

Kila Mtanzania ni vyema ajiulize, amechangia nini kuboresha miundombinu ya shule kwenye eneo lake au amechangia nini, katika maendeleo ya elimu nchini? Binafsi ninaamini hilo linawezekana cha muhimu ni kutimiza wajibu.

**KABWELA** — Na Fadhili Mohammed



# Mtatiro atimua viongozi ushirika

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MKUU wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, amewafukuza kazi viongozi 20 wa vyama vya msingi vya wakulima na Chama Kikuu cha Ushirika cha Wakulima wa Wilaya ya Tunduru (TAMCU) kwa tuhuma za ubadhirifu wa fedha za wakulima wa korosho.

Viongozi waliofukuzwa ni waandishi wakuu na wasaidizi wao kutoka katika vyama vya msingi Nguvumali Amcos, Nakatete Amcos, Namsosa Amcos, Naluale Amcos, Mshikamano Amcos, Chiliwena Amcos, Mlimi Amcos na Mlingoti Mashariki.

Sambamba na hao, wako viongozi kutoka ofisi za TAMCU Said Chuma, Omari Matola, Mohamed Selemani, Ashura Ndomondo na Filemoni Komba.

Sambamba na kufukuzwa huko, pia Mtatiro amemtaka Mkuu wa Polisi Wilaya ya Tunduru, kuwaweka chini ya ulinzi na kuwaweka ndani wakati akiandaa taarifa za wizi huo na kuzikabidhi kwa Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (Takukuru).

Mtatilo alitoa maelekezo hayo katika kikao chake na viongozi wa vyama vya ushirika kilichofanyika katika ukumbi wa Klasta ya Walimu wa Tarafa ya Mlingoti Magharibi mjini hapa.

Alisema uamuzi huo amechukua kutokana na ofisi yake kujiridhisha na taarifa za uendeshaji mbovu wa vyama hivyo.

Kutokana na hali hiyo, Mtatiro amemwagiza Ofisa Ushirika wa Wilaya ya Tunduru, George Bisani, kuandaa taratibu za kisheria ili kujaza nafasi zao.

Pia katika taarifa hiyo, Mtatiro ametuma salamu kwa Meneja wa Chama Kikuu na mwenyekiti wao kwa kuwataka kujipanga upya katika utendaji wao vinginevyo hatasita kuwaondoa na kuweka viongozi wapya.

"Acheni kufanya kazi kwa mazoea. Serikali iko macho, hivyo haiwezi kuvumilia vitendo vya viogozi wa vyama vya msingi na chama kikuu kutia mikono katika kapu la fedha za wakulima na kuzivuruga," alisema.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti nje ya ukumbi, baadhi ya wajumbe wa mkutano huo walisema kuwa kitendo cha kukamatwa mara kwa mara na kufukuzwa kwa viongozi hao, kunawatia shaka waandishi wa vyama mbalimbali kuendelea na kazi hiyo.

Wajumbe hao ambao waliomba wasitajwe majina yao, walisema hawakatai kuwapo kwa makosa madogo madogo yanayojitokeza katika utendaji wa shughuli zao, hivyo serikali kama msimamizi ilitakiwa kuwaonya na kuwafanya waendelee na shughuli zao tofauti na kuwafukuza kazi.

# Minada yote sasa kuendeshwa kimtandao

**Na Beatrice Shayo**

MAMLAKA ya Mapato nchini (TRA) imebadili utaratibu wa kuendesha minada yote iliyokuwa ikifanyika kwa njia ya hadhara na sasa kufanyika kwa mfumo wa mtandao.

Kadhalika, minada iliyokuwa ikifanyika TRA, imedaiwa kuhusishwa na vitendo vya rushwa vinavyowahusisha maofisa wa mamlaka hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam jana, Kamishna Mkuu wa TRA, Dk. Edwin Mhede, alisema wameamua kuanzisha mfumo huo ili kuokoa gharama katika uendeshaji wa mnada.

Alisema gharama za uendeshaji wa mnada wa hadhara ni kubwa na kuhusishwa na vitendo vya rushwa hali iliyowalazimu kuanzisha mfumo huo.

"Washiriki wa mnada ni walewale wanajirudia rudia. Hata hivyo wengi wao sio wanunuzi na mara kadhaa wamekuwa wakiingilia minada na kuharibu na kufanya wanunuzi wenye nia kushindwa kununua bidhaa hizo," alisisitiza Mhede.

Pia alisema kumekuwa na vitendo vya kuzuia wengine na kupanga bei ambayo ni kinyume na busara ya misingi ya uchumi kunakofanywa na baadhi ya watu wenye hila kwa mtandao waliouweka.

Kadhalika bidhaa haziuzwi kwa wingi zinapotangazwa.

"Kumekuwa na tuhuma na vitendo vya rushwa vikiwahusisha hata baadhi ya maofisa wetu," alisema.

Dk. Mhede alisema ulipaji wa malipo ya awali ya asilimia 25 kwa washindi unahitaji washiriki kwenda eneo la mnada na fedha taslimu na kwa wale wanaolipa kwenye akaunti zao iliwalazimu wawe na akaunti ya benki iliyopo kwenye eneo la mnada.

"Kumekuwa na mrundikano wa bidhaa zilizopitisha muda kwenye maeneo mbalimbali yaliyopo chini ya forodha bila kuuzwa jambo ambalo linaloathiri operesheni na kushindwa kutoa bidhaa zingine zinazoingia au kutoka nchini kwa wakati," alisema.

Alisema gharama zinazotumiwa na mamlaka kuendesha minada hiyo ni kubwa na hivyo kazi hiyo kufanywa kwa tija ndogo. Dk. Mhede alisema kutokana na changamoto hizo mamlaka iliamua kuchukua hatua za kusitisha minada ya hadhara kwa kipindi cha mwezi mmoja.

Alisema kwa sasa minada imerudi na itakuwa inafanyika kwa njia ya mtandao lengo likiwa ni kutatua changamoto zilizokuwa zimejitokeza awali. Kadhalika, alisema kuanza kwa mfumo huo wanatarajia kuuza bidhaa nyingi kwa wakati pamoja na kuwapo kwa ushindani ulio wa haki na hatimaye makusanyo ya kodi kuongezeka.

Alisema Watanzania wengi wenye nia watapata fursa ya kununua bila kuongeza gharama kwa kutumia madalali.

"Gharama zinazotumika na mamlaka kuendesha minada hii kwa njia ya mtandao inatarajiwa kuwa ndogo ikilinganishwa na utaratibu wa awali na kuwezesha kazi hii kufanywa kwa tija kubwa," alisema.

Alisema mnada utaanza rasmi Januari 2, 2020, mshiriki atatakiwa kuingia kwenye tovuti ya TRA ambayo ni www.tra.go.tz .



Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Dk. Edwin Mhede, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu uendeshaji wa minada ya forodha kwa njia ya mitandao. Kushoto ni Mkurugenzi wa Mafunzo, Charles Palapala na Naibu Kamishna Godfrey Kitundu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wakulima kitanzini mikopo pembejeo

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

SERIKALI imewataka wakulima waliokopa pembejeo kwa ajili ya kupulizia mikorosho kulipa madeni yao kabla ya Januari 5, mwakani na kwamba ambaye hatalipa atajulikana kuwa mwizi.

Ili kuhakikisha kila mkulima aliyekopa analipa kwa wakati, Mkuu wa Wilaya Tunduru, Julius Mtatilo, amewataka waandishi wa vyama vya msingi vya ushirika wa wakulima (Amcos) kuorodhesha majina ya wahusika na kuyapeleka ofisini kwake. Akizungumza kuhusu suala hilo jana, Mtatiro alisema wakulima ambao hawatalipa fedha hizo watakumbwa na operesheni maalumu ambayo itaongonzwa na ofisi yake kwa kuwakamata na kuwachukulia hatua za kisheria.

Awali Kaimu Meneja wa Mipango ya Kilimo Bodi ya Korosho Tanzania, Juma Yusuph, alisema wakulima hao wanadaiwa Sh. 468,081,500.

Yussuph alisema katika mikopo hiyo, wako wateja ambao walipokea mkopo wa asilimia 50 ya bei soko ya pembejeo husika na wengine walichukua mikopo hiyo kwa kulipiwa asilimia 100 ya bei ya soko ya pembejeo za dawa walizohitaji.

Akifafanua kuwa pamoja na nia nzuri ya serikali kutoa mikopo hiyo kwa wakulima, kasi ya urejeshaji ni ndogo ikilinganishwa na kasi malipo ya korosho zao kwa sasa.

Hadi Desemba 21, mwaka huu, alisema kiasi kilichorejeshwa kutoka kwa wateja hao zilikuwa Sh. 94,898,852.27 sawa na asilimia 20 ya mkopo huo. Alisema takwimu zinaonyesha kuwa fedha hizo zilikopeshwa kwa wakulima kutoka katika vyama vya msingi 34 kati ya 37 vilivyoko wilayani hapa.

HABARI KITAIFA

# Walalamikia bei za nguo Kariakoo

**Na Maulid Mmbaga**

BAADHI ya wananchi wamelalamikia ongezeko la bei za bidhaa masokoni wakati huo wa sikukuu za mwisho wa mwaka.

Mkazi wa Dar es Salaam, Fred John, alitoa malalamiko hayo wakati akifanya manunuzi ya nguo kwa ajili ya watoto wake katika soko la Kariakoo, jana.

Alisema kumekuwapo na ongezeko la bei hususan nguo, ambapo wafanyabiashara wengi wamepandisha thamani ya bidhaa hizo tofauti na walivyo kuwa wakinunua siku za kawaida.

Aliongeza kuwa katika kipindi hiki kuna uhitaji mkubwa wa bidhaa, hivyo wafanyabiashara wanatumia kigezo hicho kupandisha bei za bidhaa.

"Nguo yenye thamani ya Sh. 15,000 unakuta unauziwa Sh. 20,000, hali inayosababisha wanunuzi wengi kushindwa kukidhi mahitaji yao ipasavyo," alisema John.

"Wafanyabiashara wauze nguo bei inayoendana na thamani ya bidhaa husika," alisisitiza John. Mfanyabiashara wa nguo katika soko hilo, Naomi Iddy, aliwakosoa wanaolalamika kuhusu kupanda kwa bei za bidhaa hizo.

Alisema kipindi cha sikukuu bidhaa hutoka kwa wingi, hivyo zinapoisha hupatikana kwa shida, na huwalazimu kuagiza kutoka nje ya nchi ili kukidhi mahitaji ya wateja.

"Tunaagiza bidhaa kutoka China, hivyo hilo hupelekea thamani ya nguo kuongezeka ili kukidhi gharama za uendeshaji wa biashara," alisema Iddy.

Aliongeza kwamba wanajitahidi kuhakikisha wanawaletea wateja wao bidhaa zenye ubora na zinazokidhi mahitaji ya wanunuzi kipindi hiki cha sikukuu.

"Napenda kuwashauri wateja wanapokuja kununua nguo katika soko hili hasa kwa kipindi hiki, wafike katika maduka husika, wasifanye manunuzi nje ili kuepuka matapeli," alishauri Iddy. Katika soko la Buguruni lililopo, hali ya bei za vyakula na matunda ni ya kawaida, na wananchi huendelea kufanya manunuzi ya bidhaa za majumbani zinazohusishwa na maandalizi ya sikukuu.



Baadhi ya wakazi wa Jiji la Dodoma wakinunua kuku ikiwa ni maandalizi ya sikukuu ya Krismasi kama walivyokutwa nje ya soko kuu la Majengo jijini humo, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mwakilishi awakosoa wanawake kazi za ufundi

**Na Mwandishi**
WETU, PEMBA

MWAKILISHI wa Ziwani Wilaya ya Chakechake Pemba, Suleiman Said Ali, amewataka wanawake kuacha dhana potofu ya kuwa wanaume peke yao ndio wanaohusika na shughuli za ufundi, badala yake wajue na wao wanaweza kufanya kazi hiyo na kuwaletea tija katika maisha yao.

Alisema nchi inaelekea kwenye uchumi wa kati wa viwanda, hivyo ipo haja kwa wanawake nao kusomea ufundi ili zitakapotoka ajira katika viwanda, wapate fursa ya kuajiriwa.

Akizungumza kwa niaba ya mwakilishi wa Kwahani, Ali Salim Haji, wakati akifunga mkutano wa kuwahamasisha wanawake kujiunga kwenye vituo vya Elimu Amali mjini Wete, alisema wanawake wanaweza na wapo ambao ni mafundi, madereva na wanaotengeneza taa za sola.

"Wanawake msijijenge kuwa ufundi unawahusu wanaume tu, hapana, na nyinyi pia mna uwezo huo, hivyo jiungeni kwenye vituo vya elimu amali musomee fani, kwanza nchi inaelekea kwenye uchumi wa viwanda, hivyo mtapata fursa za ajira," alieleza.

Alisema serikali haiwezi kuajiri watu wote na ndio maana inajenga vituo vya elimu amali Unguja na Pemba, ili kuhakikisha vijana wanapata elimu, itakayowasaidia wananchi wake kupata maendeleo.

"Tujiungeni kwenye vituo vya elimu amali, kuna mambo mengi ya kujifunza, hivyo mtafaidika kwani kazi ya ufundi unafanya popote pale utakapokwenda," alieleza.

Aliipongeza Jumuiya ya Maendeleo ya Vijana ya Mkunguni Zanzibar (MYDO) kwa kuimarisha na kuhakikisha wanawapatia vijana wa kike taaluma ya kujiunga na vituo hivyo, kwani imeonekana wengi wao hawajiungi, ambapo hujiunga wanaume zaidi.

Mratibu Mipango na Sera kutoka Wizara ya Elimu Pemba, Ramla Abass Farhan, alisema malengo ya serikali ni jamii inainuka kiuchumi na ndio maana ikafanya kila jitihada kuhakikisha vijana wote wanapata elimu ili wajikomboe na kupata maendeleo.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka kila mmoja apate alimu ambayo itamsaidia katika maisha yake na kwa wale ambao hawakuendelea na elimu ya juu, serikali imewawekea vituo vya elimu amali ili waweze kujiajiri na wasiwe wanazurura," alieleza. Mwalimu mkuu wa kituo cha Elimu Amali Vitongoji, Juma Mussa Ali, alisema wananchi wanapaswa kuipongeza serikali kwa kuweka mpango wa kuanzisha vituo hivyo, jambo ambalo litasaidia kuongeza ustadi wa kiufundi kwa vijana na kujiajiri wenyewe.

"Unapopata elimu ya ufundi unaweza kujiajiri mweyewe na kujiendeleza kiuchumi, nje kuna vijana wengi wamemaliza na wamekuwa mafundi mahiri," alisema.

Naye Katibu wa Jumuiya ya MYDO, Ali Kombo Hassan, alisema serikali inaendelea kujenga vituo vya mafunzo ya elimu amali ili vijana wasome, kwani mafunzo hayo ni muhimu kwa watu wote kutokana na kuwa atafanya kazi zake na kujipatia fedha bila ya kuajiriwa na serikali.

Akichangia katika mkutano huo, Hidaya Hemed Khamis alishukuru MYDO kwa kuwapatia vijana wa kike mafunzo hayo, kwani yatawasaidia kujiendeleza pale inapotokezea hawakufaulu vizuri masomo yao.

Ofisa Vijana Wilaya ya Wete, Hadia Mohamed Omar, aliwataka vijana wa kike kujiendeleza na masomo ya kiufundi, ili kujiajiri wenyewe, jambo ambalo litasawasaidia katika shughuli zao.

Mradi huo unatekelezwa na MYDO chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB).

# Wafagilia ujenzi daraja

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

WAKAZI wa Kijiji cha Miungo Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, wameipongeza serikali kwa kuwajengea daraja la kisasa lenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 65.6.

Daraja hilo ambalo linaunganisha vijiji mbalimbali vya Kata ya Mkululu na Mbuyuni limekuwa kichocheo cha uchumi mkubwa kwa wakazi wa vijiji hivyo.

Pongezi hizo walizitoa wakati Mbunge wa Lulindi, Jeremo Bwanausi na Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Selemani Mzee pamoja viongozi wengine walipotembelea kukagua maendeleo ya ujenzi huo.

Kasimu Hamisi, mkazi wa Miungo alisema wanaipongeza serikali kwa hatua ya kuamua kujenga daraja hilo ambapo ni wazi lilikuwa ni kero kubwa katika kuvuka hasa kipindi cha masika kama hiki.

Alisema moja ya kero kubwa ambayo ilikuwa kikwazo kwa wananchi pale wanapotaka kwenda kupata huduma za afya katika zahanati ya Mbuyuni ilikuwa shida kwa wakazi wa Miungo kuvuka.

Alisema adha nyingine ilikuwa kwa wajawazito kipindi cha masika ilikuwa ngumu kuvuka mto huo kwani ulikuwa ukijaa maji, hivyo wajawazito waliamua kujifungulia majumbani.

Naye Fatuma Mohamedi alisema maamuzi ya serikali kuamua kujenga daraja la kisasa katika mto huo kutaleta faraja kubwa kwa wakazi hao kwa sababu daraja hilo litafungua fursa za kiuchumi.

"Tunampongeza Rais John Magufuli na serikali yake kwa kutujengea daraja hili ni wazi likikamilika litasaidia uwepo wa fursa za kiuchumi kwetu," alisema.

Naye Athumani Ngaweje alisema ujenzi wa daraja hilo mkombozi kwa wananchi wanaotumia eneo hilo kufika kutoka Mbuyuni na kwenda vijiji vya jirani kama Miungo.

Mwenyekiti wa kijiji cha Miungo, Omari Mussa, alisema adha ya mto huo ni pale watoto na wanawake walipokuwa wakivuka kwenda vijiji vya jirani kufuata huduma za kijamii.

Aliishukuru serikali kwa ujenzi wa daraja hilo muhimu kwa wananchi wa Jimbo la Lulindi.

Naye Meneja wa Wakala Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) Wilaya ya Masasi, William Tizalwa, alisema kupitia serikali imetoa fedha zaidi ya Sh. bilioni 65.6 kwa ajili ya kujenga daraja hilo.

Mbunge wa Lulindi, Jerome Bwanausi, aliishukuru serikali kwa jitahada zake za uboreshaji wa huduma za kijamii katika jimbo hilo.

# Korosho zatumbua viongozi wa ushirika

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MKUU wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, Julius Mtatiro, amewafukuza kazi viongozi 20 wa vyama vya msingi vya wakulima na Chama Kikuu cha Ushirika cha Wakulima wa Wilaya ya Tunduru (TAMCU) kwa tuhuma za ubadhirifu wa fedha za wakulima wa korosho.

Sambamba na kuwafukuza, pia Mtatilo amemwagiza Kamanda wa Polisi Wilaya ya Tunduru kuwakamata watuhumiwa na kuwaweke ndani wakati akiandaa taarifa za wizi huo kisha kuzikabidhi kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kwa uchunguzi zaidi.

Mtatiro alitoa maagizo hayo katika kikao chake na viongozi wa vyama vya ushirika mjini hapa, na kwamba maamuzi hayo yametokana na ofisi yake kujiridhisha na uwapo wa taarifa za uendeshaji mbovu wa vyama vyao.

Mtatiro kadhalika, amemwagiza Ofisa Ushirika wa Wilaya ya Tunduru, Georgi Bisani kufanya taratibu za kisheria ili kujaza nafasi zao kwa lengo la kuendelea kuwahudumia wakulima. Aidha, katika taarifa hiyo, Mtatiro pia ametuma salamu kwa meneja wa chama kikuu na mwenyekiti wao kwa kuwataka kujipanga upya katika utendaji, vinginevyo hatasita kukivuruga chama hicho na kuwaondoa na kuweka viongozi wapya.

"Acheni kufanya kazi kwa mazoea, serikali ipo macho, hivyo haiwezi kuvumilia vitendo vya viogozi wa vyama vya msingi na chama kikuu kutia mikono katika kapu la fedha za wakulima na kuzivuruga," alisisitiza Mtatiro.

Viongozi waliofukuzwa ni waandishi wakuu na wasaidizi wao katika vyama vya msingi Nguvumali Amcos, Nakatete Amcos, Namsosa Amcos, Naluale Amcos, Mshikamano Amcos, Chiliwena Amcos, Mlimi Amcos na Mlingoti Mashariki ambacho mwenyekiti wake, Alifa Abdala Alifa pia alikumbwa na kadhia hiyo.

Viongozi kutoka ofisi za chama kikuu cha wakulima wa Wilaya ya Tunduru Tamcu waliokumbwa na timua timua hiyo ni Said Chuma, Omari Matola, Mohamed Selemani, Ashura Ndomondo na Philemon Komba.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti nje ya ukumbi, baadhi ya wajumbe wa mkutano huo walisema kitendo cha kukamatwa mara kwa mara na kufukuzwa kwa viongozi hao kinawatia shaka waandishi wa vyama mbalimbali kuendelea na kazi hiyo.

Ofisa Ushirika Wilaya ya Tunduru, Gorgi Bisani, alisema ofisi yake imepokea maelekezo hayo na kwamba atayafanyia kazi haraka ili kuruhusu shughuli za kupima korosho na kuwalipa wakulima ziendelee.



Mfanyabiashara wa vifaa vya urembo akipanga vizuri bidhaa zake kwa ajili ya kusubiri wateja katika eneo la stendi kuu ya mabasi wilayani Masasi Mkoa wa Mtwara jana. **PICHA: HAMISI NASIRI.**

# Kamati maadili zahimizwa taasisi umma

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

KUKOSEKANA kwa kamati za maadili katika taasisi za umma na mashirika yasiyo ya kiserikali, mkoani Shinyanga kumetajwa kuwa chanzo cha migogoro baina ya viongozi wa taasisi hizo na watumishi wakati wa utoaji wa huduma kwa wananchi.

Hayo yalisemwa na Kaimu Mkuu wa Kanda Ofisi ya Rais, Sekteratieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Kanda ya Magharibi Tabora, Gerald Mwaitebele, wakati akitoa mafunzo kwa wajumbe wa kamati za maadili kutoka taasisi mbalimbali kuhusiana na sheria ya maadili ya viongozi.

Alisema kuwa, kamati hizo zipo kwa mujibu wa sheria na zinatakiwa kuwapo kwa kila taasisi ya umma na ile isiyo ya umma na kutokuwapo kwa taasisi hizo ndio kunasababisha kuibuka kwa migogoro baina ya viongozi na watumishi wakati wa majukumu.

"Ofisi nyingi kumekuwa kukiibuka kwa migogoro baina ya viongozi wa taasisi na watumishi hasa katika utoaji wa haki kwa mtumishi anapokosea au kwenda kinyume cha sheria za utumishi wa umma, viongozi wamekuwa wakipendelea na kuibuka kwa taharuki," alisema Mwaitebele.

Aliongeza kuwa: "Kamati hizi zipo sheria na zinatakiwa kuwepo kila ofisi ya umma, na niwatake wakuu wote wa taasisi na mashirika ya umma kuanzisha kamati hizi na kutozihusisha kamati ambazo zimemaliza muda wake ili kuboresha utendaji kazi kwa watumishi ambao mnawasimamia.

Aidha, Mwaitebele alisema kamati hizo zitasaidia kuondoa migongano ya kimaslahi baina yao na watumishi katika maeneo yao ya kazi na mnaweza kujadili na kuzipatia changamoto mbalimbali zinazowakabili watumishi hususani wanapokiuka maadili ya utumishi wa umma.

Akifungua mafunzo hayo Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Albert Msovela, aliwataka wakuu wa mashirika na taasisi za umma kufanya kazi kwa weledi pasipo kupendelea na kuepuka vitendo vya rushwa ambavyo vinaweza kukwamisha utendaji kazi.

Pia Msovela aliwataka viongozi wote wa mashirika ya umma mkoani hapa kuhakikisha wanaziunda kamati za maadili ili kuepuka migogoro ya kimaslahi ambayo ndio chanzo za ukwamishaji wa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umma.

# Mabasi mabovu yapewa kibano

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, limewataka madereva wa mabasi yaendayo mikoani kutoendesha vyombo hivyo, huku wakijua ni vibovu.

Badala yake wametakiwa wayarekebishe ili kuendelea kutoa huduma kwa wananchi bila kuleta madhara yoyote.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Sofia Jongo, aliyabainisha hayo jana katika operetioni maalumu ya kukagua mabasi ya abiria yaendayo mikoani katika kituo kikuu cha mabasi cha mjini Kahama.

Alisema kuwa mabasi yanayokwenda mikoani mengi ni mabovu na yamekuwa yakifungwa hadi kamba za katani kwenye spring na kuonya kuwa jeshi hilo halitaruhusu magari mabovu kuendelea kutoa huduma za usafirishaji na kuhatarisha usalama wa abiria.

"Magari mengi hayana breki, spring na mengine yamefungwa kamba za katani kwenye spring, na madereva wa magari haya mnayaona, lakini mnashindwa kutoa taarifa katika Jeshi la Polisi mnasubiria mpaka itakapotokea ajali," alisema Jongo.

Mkuu wa Usalama Barabarani, Ahamada Abdallah Hamisi, alisema katika ukaguzi wa magari uliofanywa kituo kikuu cha mabasi Kahama wamebaini magari mengi yanayotoa huduma ya usafirishaji ni mabovu.

Alisema jumla ya mabasi 15 ya abiria yamefungiwa kutoa huduma ya usafirishaji wa abiria, huku 65 yakitozwa faini na 22 yakionywa baada ya kubainika kuwa na hitilafu mbalimbali.

Ahamada alilazimika kulizuia kuendelea na safari basi la kampuni ya Fresta Investment lililokuwa likisafisha abiria 60 kutoka Dar es Salaam kwenda Bukoba, baada ya kubainika spring kufungwa mipira na kamba za katani.

Mohamed Hassani na Adela Mbecha, wasafiri walikuwa wakitokea Dar es Salaam kwenda Bukoba, walilishukuru Jeshi la Polisi kwa kuyazuia magari mabovu yasiendelee na safari na kushauri wamiliki wa vyombo hivyo wawajibishwe.

# China kutumika kuongeza watalii

**Na Allan Isack, ARUSHA**

WADAU wa utalii nchini wametakiwa kulitumia soko la kimataifa la China kuitangaza kimataifa Tanzania na vivutio vyake ili kuongeza idadi ya watalii nchini, kutoka 17,000 kwa kipindi cha mwaka 2016 hadi kufikia milioni 10 mwaka 2030.

Akizungumza jijini hapa, katika kongamano la wadau wa utalii lililoandaliwa na Chama cha Waongoza Utalii nchini Tatoo, Balozi wa Tanzania nchini China, Mberwa Kairuki, alisema soko la utalii nchini China linakuwa kwa kasi na kipindi cha mwaka 2018, watalii milioni 130, kutoka China walitembelea nchi mbalimbali duniani zikiwamo nchi za Bara la Afrika.

Balozi Kairuki, aliwataka wadau wa utalii nchini, kutumia fursa ya soko hilo kutangaza vivutio vilivyopo hapa nchini, ikiwamo Mlima Kilimanjaro ili kuongeza idadi ya watalii wanaoingia nchini na kufikia lengo la kuwa na watalii milioni 10 ifikapo mwaka 2030.

Alisema ongezeko la watalii nchini litakuza uchumi na kuongeza pato la taifa.

"Tanzania tunaongoza kuwa na vivutio vingi vya utalii ikiwamo Mlima Kilimanjaro kinachotakiwa ni kutumia fursa hii kutangaza vivutio hivyo kimataifa ili mataifa yatambue kuwa Mlima Kilimanjaro upo Tanzania," alisema.

Alisema ongezeko la watalii kutoka nchini China ni kutoka 17,000 mwaka 2016 hadi kufikia watalii 32,000 kwa mwaka 2018.

Pia alisema kuna haja ya kuongeza mpango mkakati ili idadi ya watalii kuongeza na kufikia mpango wa serikali wa kuwa na watalii milioni mbili ifikapo mwaka 2020.

Kadhalika ameziomba sekta mbalimbali ikiwamo ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Mambo ya Nje, Wizara ya Mambo ya Ndani, Bodi ya Utalii nchini (TTB), na wamiliki wa mahoteli kujipanga kuitangaza Tanzania na vivutio vyake katika soko la China.

Makamu Mwenyekiti wa Tatoo, Hendri Kimambo, amepongeza jitihada zinazofanywa na serikali kwa kuwatumia balozi wake kutangaza utalii na vivutio vilivyopo nchini.

Alisema hatua hiyo ya serikali kutumia mabalozi wake kutangaza vivutio vya utalii ni jambo jema kwa lengo la kuongeza idadi yao nchini.

"Sisi kama Tatoo tumejipanga kulipokea soko la China na tunaunga mkono jitihada zinazofanywa na serikali kuimarisha utalii hapa nchini," alisema Kimambo.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, akionyesha silaha za kivita aina ya Chinese 56 Sub Machine Gun (SMG) na risasi 147 zilizokuwa zimehifadhiwa ndani ya kopo katika msitu wa Enguserosambu, Tarafa ya Loliondo. Vitu hivyo vilikutwa baada ya majibizano baina ya polisi na majangili ambao walikimbia. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Mnyeti ajifagilia uchapaji kazi

**Na Allan Isack,** MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, amejitapa kuwa ndiye Mkuu wa Mkoa anayeongoza nchini kwa kuwatumikia wananchi kwa zaidi ya asilimia 90 baada ya kutembelea na kutatua kero kwenye vijiji vyote vilivyopo mkoani humo.

Aliyasema hayo juzi, Mjini Babati wakati wa kikao cha ushauri cha mkoa huo (RCC) kilichowakutanisha wakuu wa wilaya, wabunge na wakurugenzi watendaji wa halmashauri.

Alisema kwa kipindi cha miaka miwili cha uongozi wake, mkoani Manyara amefanikiwa kutembelea vijiji na kutatua matatizo mbalimbali kwa asilimia 90, jambo ambalo halijawahi kufanywa na mkuu wa mkoa yeyote.

"Ninyi wenyewe ni mashahidi hata juzi hapa mlisikia kule Morogoro, Mkuu wa Mkoa amekaa miaka minne, lakini hata kufanya mikutano kwenye vijiji vyake ilikuwa ni shida," alisema Mnyeti.

Alisema kauli hiyo, ameitoa siyo kwa kujisifia bali amefanikiwa malengo ya kusikiliza na kutatua kero zinanazowakabili wananchi wa eneo hilo.

"Kwa mambo mazuri niliyofanya kwenye mkoa huu, Rais John Magufuli amenionea huruma na akanipa gari jipya kwa kuwa gari lililokuwapo lilitumiwa miaka sita na wakuu wa mikoa watatu kwa waliopita na walitembea nalo umbali wa kilomita 160,000, pamoja na mimi kwa kipindi cha miaka miwili nimelitembelea kwa umbali wa kilomita 300,000," alisema Mnyeti.

Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, Tumaini Magessa, alisema, Mnyeti amejitahidi kutimiza wajibu wake ipasavyo tangu alipoteuliwa kushika nafasi hiyo.

"Amefanikisha kuwaunganisha wananchi na viongozi na kuondokana na migogoro isiyo kuwa na tija ambayo ingeturudisha nyuma," alisema Magessa.

Mnyeti aliteuliwa na Rais John Magufuli Oktoba 26, 2017 kuwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara na mkoa huo ulianzishwa rasmi mwaka 2002 baada ya Mkoa wa Arusha kugawanywa.

# Wapongeza kikosi cha usalama barabarani

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

WAKAZI wa Mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, wamewapongeza askari polisi wa Kikosi cha Usalama Barabarani kwa kupunguza ajali hatua iliyotokana na kutowabughudhi watumiaji wa vyombo vya moto hususani waendesha bodaboda.

Wakizungumza na Nipashe jana, wakazi hao walidai kuwa askari hao, wamekuwa wakitoa elimu ya usalama barabarani badala ya kuwakamata madereva ovyo.

Mmoja kati ya madereva wa bodaboda, Ally Juma, alisema askari polisi wa usalama barabarani hawawanyanyasi wala kuomba rushwa kama awali.

"Miaka iliyopita kipindi kama hiki cha mwishoni mwa mwaka huwa tunasumbuliwa kwa kuombwa rushwa za sikukuu tofauti na sasa wanafanya kazi ya kutoa elimu ya usalama barabarani ili kupunguza ajali," alisema.

Alisema askari wa usalama barabarani wa eneo hilo, sasa hivi hawaonei watu na mtu akikamatwa anakuwa na kosa linalostahili.

Mkazi wa mji mdogo wa Mirerani, Nyinda Baruti, alisema askari wa usalama barabarani wa Mirerani wanapaswa kupongezwa kwa namna wanavyofanya kazi zao tofauti na miaka iliyopita.

"Mkuu wa askari polisi wa usalama barabarani wa Wilaya ya Simanjiro (DTO), Nicolaus Mushi, anastahili pongezi kwa namna vijana wake wanavyofanya kazi ya usalama barabarani," alisema Baruti.

Alisema askari polisi wa usalama barabarani wa maeneo mengine wanapaswa kuiga askari wa Mirerani ambao wanatoa elimu kuliko kukamata ovyo pikipiki za watu kwa makosa ambayo hayana maana.

Hata hivyo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Manyara, Agostino Senga, alisema askari polisi wa usalama barabarani wanatekeleza wajibu wao ili kuhakikisha ajali zinapungua au kumalizika.

Senga alisema elimu imeendelea kutolewa kwa askari polisi hao wa usalama barabarani ili wawatumikie watumiaji wa barabara.

"Hivi sasa mambo yamebadilika kwa hiyo hata askari wetu nao wamebadilika kwa kutimiza wajibu wao kwa wadau wa barabara ndiyo maana unasikia pongezi hizo," alisema.

# Moshi yafurika wageni Sikukuu Krismasi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MJI wa Moshi umejaa idadi kubwa ya wageni kutoka mikoa mbalimbali nchini, huku msongamano wa magari madogo yanayoingia na kuelekea vijijini ukiongezeka.

Msongamano huo unatokana na utamaduni wa wenyeji wa Mkoa wa Kilimanjaro, kurejea makwao kila inapofika sherehe za mwisho wa mwaka za Krismasi na Mwaka Mpya.

Kuanzia majira ya 4:00 asubuhi jana, katikati ya mji huo na kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani, hali ilikuwa tete pia kutokana na idadi kubwa ya abiria kugombea mabasi madogo yanayofanya safari zake kati ya Moshi mjini na maeneo ya Rombo, Marangu, Machame, Siha, Old Moshi na Uru.


Nipashe lilishuhudia Polisi wa Kikosi cha Usalama Barabarani, wakiwa wamepangwa kila kona kudhibiti upakiaji wa hatari wa abiria hao.

Meneja wa kituo kikuu cha mabasi cha Moshi Mjini, Samwel Mlay, akizungumzia msongamano wa abiria hao kituoni hapo, alisema abiria wengi waliletwa na treni ya abiria ambayo imesaidia kupunguza matumizi ya mabasi madogo ya kukodi kutoka Dar es Salaam kuja Moshi.

"Tumshukuru sana Rais wetu Dk. John Magufuli kwa kuleta treni ya abiria Moshi, kwa sababu kipindi hiki hali huwa mbaya kwa usafiri, tunamwomba ikimpendeza zaidi aongeze mabehewa mengine ili kuchukua abiria wengi zaidi ya hawa," alisema Mlay.

Kutokana na kuongezeka kwa abiria katika msimu wa sikukuu za mwisho wa mwaka, Shirika la Reli Tanzania (TRC), lilitangaza kuongeza safari za Dar es Salaam/Moshi kutoka nne kwa wiki (mbili kwenda na mbili kurudi) hadi sita.

Hatua hiyo inatokana na mahitaji makubwa yaliopo tangu treni ya abiria irejee kufanya safari zake kutoka Dar es Salaam kwenda Moshi, Desemba 6, mwaka huu baada ya miaka 25 ya kusitishwa, kwa safari moja zaidi ya abiria 600 husafiri.



Sehemu ya wataalamu kutoka Chama Kikuu cha Ushirika cha Akiba na Mikopo Tanzania (SCCULT Ltd-1992), Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kumaliza kuandaa masharti, sera za mfano na miongozo kwa ajili ya kuviongoza Vyama vya Akiba vya Kuweka na Kukopa nchini (Saccos) jana, jijini Arusha. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Karibu Kili Fair kufanyika Januari

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MAONYESHO ya kimataifa yanayobeba maudhui na utajiri wa Tanzania unaotokana na sekta ya utalii maarufu kama 'Karibu Kili Fair' yamepangwa kufanyika tena kwa mara ya pili jijini Arusha kati ya Juni 5 hadi 7, 2020.

Jana, akitoa taarifa ya mwaka kuhusu shughuli za utalii zilivyoitangaza mikoa ya Kanda ya Kaskazini, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Kili Fair Promotion Ltd, Tom Kunkler, alisema maonyesho hayo yamepangwa kufanyika eneo la Friedkin Recreation Center jijini Arusha, zamani ukijulikana kama viwanja vya TGT.

Kwa mujibu wa Kunkler, maonyesho hayo yatahusisha kampuni za utalii zipatazo 500 kutoka nchi 15 duniani.

Inaelezwa kuwa maonyesho hayo mwaka ujao yanatarajiwa kuvutia wanunuzi zaidi ya 8,000 kutoka ndani na nje, zikiwamo nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Alisema tayari wafanyabiashara wa kimataifa, wenye kampuni ya uongozaji wa utalii, wamiliki wa hoteli za kitalii, mashirika ya ndege ya kimataifa na wasambazaji wa vifaa vya utalii duniani, wamethibitisha kuja nchini mwaka ujao kushiriki maonyesho hayo.

Alisema wafanyabiashara hao, wameeleza nia yao ya kuja Tanzania kutoa uzoefu wao wa biashara ya utalii pamoja na kuainisha changamoto ambazo Tanzania inapaswa kuzikabili.

Kivutio kipya mwaka ujao ni Hifadhi mpya ya Taifa ya Burigi/Chato yenye ukubwa wa kilometa za mraba 4,702.

Hifadhi hiyo sasa, inakuwa ni hifadhi ya tatu kwa ukubwa hapa nchini, ikitanguliwa na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ambayo ni ya kwanza kwa ukubwa ikiwa na eneo la kilomita za mraba 20,300 na maili 7,800, huku Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ikiwa na kilomita za mraba 14,763 ikishikilia nafasi ya pili kwa ukubwa.

Kingine ni uwekezaji wa kampuni ya kimataifa ya utafutaji na uokozi ya Kilimanjaro SAR iliyowekeza Dola za Marekani milioni tatu, kuanzisha kliniki maalumu ya kwanza ya tiba barani Afrika ambayo kwa siku moja inafanya safari zisizopungua nane.

Kliniki hiyo ina madaktari wasio na mipaka na inatoa msaada wa uokozi na matibabu kwa watalii wanaopata ajali na kuathiriwa na mabadiliko ya hali ya hewa katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro na Mlima Meru uliopo ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Arusha.

Kliniki hiyo ina madaktari wasio na mipaka na inatoa msaada wa uokozi na matibabu kwa watalii wanaopata ajali na kuathiriwa na mabadiliko ya hali ya hewa katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro na Mlima Meru uliopo ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Arusha.

## Watahadharisha usafirishaji madini shaba

**Na Mwandishi Wetu,** MWANGA

BAADHI ya wakazi wa Wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro, wameiomba serikali kuangalia uchimbaji na usafirishaji wa madini ya shaba yanayochimbwa katika eneo la Vuchama/Ndambwe katika Kata ya Shigatini.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana kuhusu usafirishaji wa madini hayo, Danstan John na Joachim Mmbaga na Anuary Mfinanga, walisema Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, inapaswa kusimamia malalamiko yanayotokana na usafirishaji wa malighafi hiyo kama unafuata taratibu.

Mmbaga alisema malalamiko kuhusu kutofuatwa kwa baadhi ya taratibu za serikali kunatishia mapato ya serikali na fedha nyingi za umma zinapotea.

Mmbaga alisema, "Kuna ujanja mwingi unafanyika huko na watu wanaosimamia mapato yatokanayo na madini hayo wanapigwa chenga na wenye magari pamoja na baadhi ya wafanyabiashara ambao wanatumia njia nyingi kukwepa kulipa mapato."

"Sisi tunaomba serikali itupie macho eneo hilo ili wananchi wanufaike, halmashauri inufaike na taifa kwa ujumla lipate haki yake."

Wilaya ya Mwanga ina utajiri mkubwa wa madini ya shaba na jasi (Gypsum) yanayopatikana, lakini hata hivyo bado uwekezaji wake haujaweza kuwa na tija, zaidi ya kuchimbwa kwa kiwango cha chini na wachimbaji wadogo.

Hata hivyo, taarifa zinazohusu fursa ya uwekezaji kwenye madini, iliyowekwa katika tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, inaeleza kuwa madini mengi hadi sasa hayajachimbwa ama yanachimwa kwa kiwango kidogo. Zaidi taarifa hiyo imeeleza, madini ambayo yanachimbwa kwa wingi na yanaipatia halmashauri hiyo mapato kwa kiasi kikubwa ni madini ya ujenzi yanayotokana na uchimbaji wa mchanga.

Uzalishaji wa madini ya jasi nchini ni tani 354,000 na mahitaji ya soko ni tani 30,000 kwa mwezi katika viwanda vya saruji nchini.

Ukurasa 17



**Askari wa UN kuendelea na ulinzi wa amani DRC**

Waandishi watakiwa kutumia mbinu hizi kuibua wanawake katika uongozi



Ukurasa 15

**Kimataifa**



**Johnson amaliza hatua ya kuitoa Uingereza EU Januari 2020**

Ukurasa 20

siasa

JUMATANO DESEMBA 25, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe



**Sudan yaanza uchunguzi imara wa makosa ya jinai**

Ukurasa 14

# Uchaguzi Chadema wa dhihirisha roho ya vyama vingi bado ina dunda

**Na Ani Jozeni**

CHAMA tangulizi cha upinzani nchini, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimemaliza uchaguzi wake wa ndani ambao Mwenyekiti wa Taifa, Freeman Mbowe, alisema ulikuwa na mazingira magumu kuliko kawaida.

Siyo jambo la kushangaza kutokana na mabadiliko makubwa katika mfumo na utendaji kisiasa tangu awamu ya tano ianze, hivyo kuendesha siasa kwa jumla ni ngumu zaidi, na watumishi serikalini watakiri kuwa hali zao kiutawala au kimatarajio zimebadilika, kwani mabadiliko yanaweza kutokea wakati wowote.

Wako wanaodhania hali hii ni hitilafu ya kiuongozi lakini fikra hiyo kwa jumla si sahihi, kwani maendeleo ya nchi yalikuwa yanahitaji kwenda kwa 'mchakamchaka,' kwa lugha ya Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa; amewahi kukiri mara kadhaa mabadiliko kama haya yalikuwa ni lazima.

Unapofanyika uchaguzi katika nchi au katika chama cha siasa, yako maeneo mawili ya kuangalia, na kila moja lina umuhimu kwa uhai wa mfumo husika, uwe wa nchi au chama cha siasa.

Eneo la kwanza ni viongozi ambao watu au wapigakura husika wanawachagua, kama yapo mageuzi na ni kwa kiasi gani, halafu eneo lingine ni kujitokeza kwa wapigakura, kama kulifikia viwango tarajiwa au waliona wabakie nyumbani.

Katika mazingira ya siasa hapa nchini, suala la kujitokeza kwa wagombea na idadi ya wapigakura, na undani wa ushindani ni mambo ya kuangalia.

Mtihani wa kwanza uliokuwa mbele ya wajumbe wa mkutano mkuu wa uchaguzi Chadema, ulikuwa ni kuamua jinsi wanavyotaka wao kuongozwa, na siyo kusikiliza 'wapiga filimbi wa Hamelin' waliokuwa wa-

Endelea 16



**Kwa hili Chadema ni sawa, swali mlikuwa wapi lakini?** Ukurasa 19

Na Mashaka Mgeta

## MZOZO WA DARFUR;

# Sudan yaanza uchunguzi imara wa makosa ya jinai



Jenerali Omar al –Bashir.**PICHA: MTANDAO**

SUDAN imeanza kuwachunguza watuhumiwa wa makosa ya jinai yaliyofanyika mkoa wa Darfur, wakati wa utawala wa Rais aliyeondolewa madarakani, Omar al-Bashir.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Uingereza (BBC), Mwendesha Mashtaka wa Serikali nchini humo, Tagelsir al-Heber amesema shauri hilo linaweza kuendeshwa nje ya nchi hiyo.

Miaka 10 iliyopita, Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Jinai (ICC) iliyopo The Hague, Uholanzi ilitoa 'waranti' ya kukamatwa kwa Bashir, akikabiliwa na tuhuma za mauaji ya halaiki na jinai dhidi ya ubinadamu.

Mgogoro kati ya vikundi vya waasi na wanamgambo waliokuwa watiifu kwa serikali katika eneo hilo, ulianza mwaka 2003. Umoja wa Mataifa (UN) unasema kiasi cha watu 300,000 walikufa.

Baada ya kuwapo madarakani kwa zaidi ya miaka 30, Bashir aliondolewa madarakani mapema mwaka huu, baada ya maandamano yaliyodhihirisha nguvu ya umma.

Hivi sasa nchi hiyo inaongozwa na serikali ya mpito inayoundwa na watawala wa kijeshi na viongozi wa vikundi vilivyoratibu na kufanikisha maandamano yaliyomtoa madarakani kiongozi huyo.

**ALICHOKISEMA MWENDESHA MASHTAKA**

Heber amesema upelelezi kuhusu kadhia ya Darfur unajielekeza katika "shauri dhidi ya viongozi wa utawala uliopita." Hakuwataja majina, lakini akasema hakuna hata mmoja wao atakayeachwa katika uchunguzi huo.

Akasema, kila aina ya jinai iliyofanyika kwenye mzozo wa Darfur itashughulikiwa, vikiwamo vitendo kadhaa vya mauaji na ubakaji.

Akasema itakapobidi, shauri kuhusiana na madai hayo linaweza kufanyika nje ya Sudan.

**KILICHOTOKEA DARFUR**

Mapigano yalitokea Darfur wakati 'mtu mweusi' alipochukua silaha akiishutumu serikali ya Bashir iliyojaa watu wenye asili ya Uarabu, kwamba walikuwa wanalikandamiza eneo hilo.

Mapigano ya silaha yalilipuka zaidi yakiwapinga wanamgambo wa vilivyokuwa vikundi maarufu vya Janjaweed vilivyokuwa vikimuunga mkono Bashir.

Walikuwa wanashutumiwa kwa kuendesha ngamia na farasi wao vijijini, wakiwaua wanaume, kuwabaka wanawake na kuiba vitu walivyovikuta.

Vikundi vya kutetea haki za binadamu viliishutumu serikali ya Bashir kwa kutumia mbinu ya uharibifu wa rasilimali za wapinzani wake. Kiasi cha watu waliokadiriwa kuwa milioni mbili waliyakimbia makazi yao.

**WASAIDIZI WA BASHIR WAKO WAPI?**

Baada ya kuondolewa madarakani Aprili mwaka huu, Mwendesha Mashtaka wa ICC alielezea azma yake ya kuendesha mashtaka kuhusiana na mauaji ya Darfur.

Kwa mujibu wa Heber, aliyekuwa Mkuu wa Intelijensia na Usalama wa Taifa (NISS) katika utawala wa Bashir, Salah Gosh, naye anachunguzwa.

Mkuu huyo wa NISS, alijiuzulu Aprili, siku mbili baada ya Bashir kuondolewa madarakani na akaondoka nchini humo.

"Kuna mashauri manne kumhusu Salah Gosh na tumeshaanza mchakato kumrudisha hapa (Sudan) kwa kushirikiana na polisi wa kimataifa (Interpol)," anasema.

Bado haijajulikana kama aliyekuwa kiongozi wa vikosi vya Janjaweed Mohamed Hamdan "Hemeti" Dagolo anachunguzwa.

Kinara huyo wa zamani wa Janjaweed huko Darfur, alimgeuka Bashir kadri maandamano ya kumwondoa madarakani yaliposhika kasi na alitangazwa kuwa Makamu wa Rais wa Baraza la Mpito la Kijeshi (TMC) baada ya Bashir kung'olewa madarakani.

Agosti mwaka huu, alikuwa miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Taifa linalosimamia kipindi cha mpito kuelekea kwenye utawala wa kiraia.

Taasisi ya Human Rights Watch, inamshutumu Hemeti kwa kusimamia unyanyasaji wa raia ikiwamo mateso, mauaji na ubakaji huko Darfur na katika majimbo mengine ya Southern Blue Nile na Southern Kordofan.

**MBABE WA KIVITA**

Hemeti amewahi kusema matumizi ya nguvu huko Darfur yalihitajika ili kuwalinda raia wake.

Mapema mwezi huu, Bashir alihukumiwa kifungo cha miaka miwili baada ya kukutwa na hatia katika shauri lililomhusisha na rushwa.

> Hivi sasa nchi hiyo inaongozwa na serikali ya mpito inayoundwa na watawala wa kijeshi na viongozi wa vikundi vilivyoratibu na kufanikisha maandamano yaliyomtoa madarakani kiongozi huyo.

Waendesha mashtaka wamemshtaki pia kwa mauaji ya waandamanaji wakati wa maandamano yaliyosababisha kuondolewa kwake madarakani.

Pia anachunguzwa kwa mapinduzi ya kijeshi ya mwaka 1989, yaliyomwingiza madarakani.

**ALIVYOONDOLEWA MADARAKANI**

Aliingia madarakani baada ya mapinduzi ya kijeshi ya mwaka 1989 na kutawala hadi 2011.

Alipochukua madaraka, Bashir aliikuta Sudan ikiwa katika miaka 21 ya vita vya wenyewe kwa wenyewe kati ya Sudan Kaskazini na Sudan Kusini.

Ingawa serikali yake ilisaini makubaliano ya kusitisha mapigano 2005, mapigano mengine yaliibuka wakati huo huo kwenye mkoa wa Magharibi wa Darfur, ambapo Bashir anashutumiwa kwa makosa ya jinai dhidi ya ubinadamu, akisakwa na ICC.

Pamoja na kusakwa na ICC, Bashir alitangazwa mshindi wa mfululizo katika Uchaguzi Mkuu wa nchi hiyo uliofanyika 2010 na 2015.

Licha ya kutakiwa na ICC, Bashir alifanya ziara katika nchi kadhaa zikiwamo Misri, Saudi Arabia na Afrika Kusini pasipo kukamatwa na polisi wa kimataifa.

Lakini Juni 2015, alilazimika kuondolewa nchini Afrika Kusini baada ya Mahakama nchini humo kujadili uwezekano wa kukamatwa kwake.

**SHUTUMA DHIDI YA BASHIR**

Pamoja na mengine, anadaiwa kuwaua watu wa vikundi vya makabila madogo ya Fur, Masalit na Zaghawa na kuwasababishia wengine wao maumivu ya mwilini na akili.

Pia anatuhumiwa kwa mauaji yakiwamo yaliyofanyika kwa kuchinja watu, kulazimisha watu kuhama makazi yao, ubakaji, mateso, kuwashambulia raia huko Darfur na kuangamiza miji na vijiji.

Lengo lake linaelezwa kwamba lilikuwa ni kuendeleza muungano wa Sudan Kusini na Sudan Kaskazini, lakini makubaliano ya kusitisha mgogoro uliokuwapo yalitambua kuwapo kwa taifa la Sudan Kusini.

Kura ya maoni ya Januari 2011, ilitoa matokeo ya asilimia 99 ya Wasudan Kusini waliotaka kujitenga na taifa hilo likatangazwa miezi sita baadaye.

**KUZALIWA KWAKE**

Bashir alizaliwa mwaka 1944, katika familia ya wakulima, Kaskazini mwa Sudan.

Anatoka katika kabila la al-Bedairyya al-Dahmashyya la Bedouin kwa jamii ya walio wengi ya Ja'alin.

Alijiunga katika Jeshi la Misri alipokuwa kijana na akapanda vyeo hadi kufikia kupigana vita mwaka 1973 dhidi ya Israel.

Habari za ndani zinaeleza kwamba hana mtoto na kwamba alimuoa mke wake wa pili akiwa katika umri wa miaka 50.

Na Sabato Kasika

# Liundi: Waandishi tumieni mbinu hizi kuibua wanawake katika uongozi



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan (aliyesimama), katika moja ya shughuli zake za uongozi. **PICHA: MTANDAO**

HIVI karibuni waandishi wa habari kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Rukwa, Shinyanga, Ruvuma na Morogoro, walishiriki warsha maalum ya kuwajengea uwezo wa jinsi kuripoti masuala ya kijinsia katika mambo ya uongozi yakiwamo ya kisiasa.

Katika warsha hiyo, iliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), waandishi wanaelekezwa kutumia kalamu zao kwa kuwaibua wanawake wanaliothubutu kupata nafasi mbalimbali za uongozi, ili waelezee mafanikio na changamoto walizopitia.

Wanakumbushwa kwamba ili kufikia usawa wa kijinsia, waandishi wa habari hawana budi kuandika habari za simulizi za wanawake mashujaa walioshika nafasi za uongozi, ili kuhamasisha wanawake wengine wawe na ujasiri wa kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika jamii.

Ushauri huu unatolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, na kufafanua kuwa wanawake wanatakiwa kushiriki katika uongozi kuanzia ngazi ya vitongoji hadi taifa.

"Mnatakiwa kutumia kalamu zenu kuhamasisha jamii kutambua kuwa wanawake wana uwezo wa kuongoza kama wanaume, ili nao wachaguliwe na kuteuliwa kwa wingi, katika nafasi mbalimbali za uongozi," anasema Lilian.

**UMUHIMU WA KUIBUA**

Liundi anasema, viongozi wanawake waliopo wakipewa nafasi ya kusikiliza simulizi zao na kuandikwa, dunia itajua na hatua hiyo itasaidia wale waliokata tamaa kupata ujasiri wa kugombea nafasi za uongozi.

"Ninaamini wapo baadhi ya wanawake waliopitia matatizo mengi ikiwamo mila na desturi kandamizi hadi kufikia hapo walipo, hivyo simulizi zao zitasaidia kuwajenga wengine," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema, kuna wanawake mashujaa, ambao taarifa zao zinatakiwa kujulikana, hivyo waandishi waongee nao, hasa walioshinda uchaguzi wa serikali za mitaa, madiwani, wabunge na viongozi wengine, ambao wote wanatakiwa kutiwa moyo badala ya kukatishwa tamaa.

Anasema, kalamu za waandishi wa habari zina nguvu kubwa za kusaidia kuhamasisha mabadiliko katika masuala ya uongozi na hatimaye kuwe na uwiano kati ya wanaume na wanawake.

Katika mkakati wa kuhakikisha uchaguzi mkuu ujao wanawake wanajitokeza kwa wingi kuwania uongozi, anasema, TGNP, imeandaa ilani ya uchaguzi ya wanawake, kwa ajili ya kubeba ajenda ya mwanamke.

Anasema, lengo la ilani hiyo ni kuhakikisha wanawake wanapata nafasi za uongozi katika nyanja zote na kushiriki katika ngazi za maamuzi kama ilivyo kwa wanaume, kwa vile wana uwezo wa kuongoza.

"Kwa ujumla ilani hii pia inataka wadau wote wa uchaguzi wazingatie misingi ya ushindani wa haki na huru na usawa wa jinsia kama ilivyoainishwa kwenye katiba, sheria, sera na mipango ya nchi na kubainishwa kwenye mikataba ya kimataifa na kikanda, ambayo serikali yetu imeridhia," anasema.

**HALI ILIVYO SASA**

Mkurugenzi huyo anasema siyo kwamba hakuna lililofanyika kwa wanawake katika uongozi, bali kuna haja ya kuendelea kuibua wanawake zaidi ili idadi yao iwe kubwa kama ilivyo ya wanaume.

"Ikumbukwe kuwa historia iliyowekwa katika nchi yetu ni kwa mara ya kwanza kupata Makamu wa Rais mwanamke, Mama Samia Suluhu Hassan, aliyepatikana katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015," anasema.

Anamtaja pia mgombea mwanamke wa nafasi ya urais, Dk. Anna Mghwira, ambao wote ni dalili kwamba nchi inakoelekea ni kuzuri katika kupata usawa kwenye nafasi za uongozi na hasa za kisiasa.

Liundi anawataka waandishi wa habari kuhamasisha vyama vya siasa kuteua wanawake wengi kwa ajili ya kuwania nafasi mbalimbali zikiwamo za udiwani, ubunge na kuhakikisha wanashinda kwa wingi katika uchaguzi.

"Ninasema hivyo kwa sababu ukiangalia hata wanawake wanaoteuliwa na vyama vya siasa kuwania nafasi ya majimbo ni ndogo, na hatimaye wanaoshinda ni kidogo zaidi. Yaani wanawake wachache sana huteuliwa na vyama vyao kuwania nafasi za uchaguzi," anasema.

Anaamini kwamba kila hatua zikienda vizuri, uchaguzi unafanyika bila manung'uniko na kwamba umefika wakati sasa wanawake kuchagua wanawake wenzao wanaowania uongozi bila kuangalia vyama wanavyotoka, ili mradi wawe na uwezo wa kuongoza.

**DHANA POTOFU**

Anasema, kumekuwapo na dhana ya kwamba wanawake hawapendani, ambayo imekuwa ikichangia kuwagawa, hivyo isipewe nafasi, kwa vile wao ni kitu kimoja, na wamekuwa wakikutana katika warsha bila ubaguzi wa vyama.

"Waandishi saidieni kuhamasisha wanawake wasikubaliane na dhana hiyo, kwani ikiruhusiwa itatugawa na kuendelea kukwamisha harakati za kutafuta usawa kwenye uongozi," anasema.

Anaongeza kuwa kila zinapofika kampeni za uchaguzi, baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakiwatungia wanawake tuhuma za kuwadhalilisha zikiwamo za mambo ya ngono yanayowavunjia heshima mbele ya jamii.

"Ni vyema waandishi mkaandika mazuri ya mgombea mwanamke kama njia ya kuhamasisha wanawake wengine kuwania uongozi kuliko kujikita kwenye ubaya tu, kwani hakuna binadamu aliyekamilika," anasema.

Liundi anasema, wanawake kwa wanaume, wote wanafanya makosa, lakini ya mwanamke ndiyo huwa yanapewa nafasi kubwa kana kwamba wanaume hawakosei, na kwamba hali hiyo inawavunja moyo wanawake.

"Njia nzuri ya kusaidia katika hilo, ni waandishi kuibua wanawake kwa mazuri yao na kuachana na hayo mengine ambayo wakati mwingine yanaweza kuwa ni ya kutungwa kwa lengo la kumkwamisha," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema, suala la uongozi linahusu watu wa jinsia zote na siyo kwa kundi moja tu, hivyo juhudi za makusudi zifanyike ili kuhakikisha mwanamke haachwi nyuma katika nafasi mbalimbali za uongozi.

Anasema, ni muhimu kutambua kuwa wanawake wana uwezo wa kuongoza kama wanaume, hivyo wasiachwe nyuma kwa visingizio au mbinu zozote zenye lengo la kuwakwamisha.

UCHAMBUZI

# Uchaguzi Chadema wadhihirisha roho ya vyama vingi bado inadunda

Inatoka Uk. 13

nataka chama hicho kibadilishe uongozi.

Haikuwa kazi rahisi na taarifa zinasema kuwa uchaguzi ulifanyika na mijadala migumu katika nafasi tofauti za uchaguzi hadi alfajiri ndiyo unakamilika.

Itakumbukwa kuwa Chama tawala (CCM) kilimaliza kikao cha Kamati Kuu cha kutoa orodha ya majina matano ya watangaza nia wa kuchujwa na kupatikana mgombea mbele ya Halmashauri Kuu na mkutano mkuu kesho yake, majira ya saa sita au saba usiku.

Haikuwa rahisi hata kidogo kwa wajumbe kukubaliana kuwa ni majina gani yapo na ni majina gani yameondolewa au kuchujwa kwa utaratibu huo.

Mwenyekiti wa taifa alitoa taarifa baadaye kuwa kulikuwa na tatizo la kupata ‘coverage’ ya uchaguzi huo, hasa kwa suala la kutangaza kinachoendelea moja kwa moja, lakini vyombo tofauti vya habari vikasita kwa suala hilo.

Uongozi ulijaribu hata kununua muda huo wa matangazo kwa gharama zake lakini bado ikawa tabu, isionekane kuwa mwenye chombo hicho anataka kuweka ishara na hisia zake za kisiasa ziko upande gani.

Ni mazingira magumu ya kuendesha mkutano wa uchaguzi, lakini kwa upande mwingine iliwapa wajumbe faragha waliyoihitaji, kwani jambo linapokuwa linatangazwa moja kwa moja kuna anayefaidika, na anayeogopa kuonekana anasema nini hapo.

Kwa maana hiyo tatizo la kutangazwa moja kwa moja inawezakana lipo lakini lina pande mbili, siyo tatizo la wazi ambalo kila mshirika alipata hisia hiyo kwa maana ile ile kama mwingine.

Wapo ambao walijisikia huru zaidi na wapo ambao walipata simanzi kiasi fulani, waliokuwa wanatazamia kutumia ‘nguvu ya umma’ huku nje kuathiri kinachotokea katika ukumbi wa mkutano, suala ambalo siyo rahisi kulitatua bila kuangalia mtiririko wa ukinzani (ndiyo na hapana) kuhusu watangaza nia na masuala yanayowaunganisha au kuwatenganisha. Ina maana kuna aina tofauti za demokrasia, pana na finyu zinazofanya kazi wakati wote, na athari za nguvu za nje (za umma au za dola) zinahusika katika kuweka mazingira safi zaidi ya mkondo mmojawapo kuhusu masuala hayo, ya nani anapata faida.

Kwa upande wa umuhimu wake kitaifa, mkutano mkuu wa uchaguzi wa chama hicho umeondoa chokochoko za kisiasa ambazo hazikuwa ndani ya chama hicho pekee bali ni sehemu ya maisha ya kisiasa, ushindani na hata kwa upande mwingine jitihada za ziada za kudhoofisha mshikamano



Katibu Mkuu mstaafu wa Chadema, Dk. Vincent Mashinji ( wa tatu kushoto), akimkabidhi fomu ya kugombea uenyekiti wa chama hicho, Mwenyekiti wa sasa Freeman Mbowe (kulia). **PICHA ZOTE: MTANDAO**

“Uongozi ulijaribu hata kununua muda huo wa matangazo kwa gharama zake lakini bado ikawa tabu, isionekane kuwa mwenye chombo hicho anataka kuweka ishara na hisia zake za kisiasa ziko upande gani.

ndani ya chama.

Siyo muhimu kuwa juhudi hizo zinatoka wapi, kwani zipo za aina mbili, zinazoanzia nje kwa wasiokitakia chama mema kwa pamoja, na zipo pia juhudi zinazoanzia ndani, miongoni mwa wale ambao dhamira zao hazikufikia tamati njema.

Mara nyingine si ajabu wahisi kuwa wamechezewa rafu; kuna eneo moja (uchaguzi wa ukanda wa Pwani) ilisemekana labda ungerudiwa.

Ni kielelezo cha ukinzani (dhidi ya viongozi waliokuwepo) na siyo lazima kuwa walishindwa kwa ‘demokrasia tupu.’

Ndiyo hapo labda kunakuwa na funzo moja la kisiasa, kuwa tatizo la ufuatiliaji na uthibitishwaji wa demokrasia siyo kati ya dola na wananchi kama wanaharakati kwa jumla wanavyopenda kuamini bali pia ni la kijamii, kuwa kuna aina ya kutokubali kushindwa.

Kwa mfano katika nchi zilizoendelea katika demokrasia



Wafuasi wa Chadema katika moja ya mikutano ya chama hicho.

mgombea anayeshindwa anatoa pongezi kwa aliyeshinda, kuwa mpango wake umekubaliwa na wapigakura, na anaahidi kuangalia upya mustakabali wa chama husika (iwe ni sera zake, au yeye mwenyewe kuachia ngazi kama kiongozi wake baada ya kushindwa katika uchaguzi).

Katika nchi kama Tanzania jambo hilo halipo kwani wafuasi wa aliyeshindwa katika kinyang’anyiro hicho hawatazamii kabisa aonyeshe udugu au urafiki wa aina hiyo, mshikamano au chochote kingine.

Labda kuna haja ya kutupia jicho na kujaribu kutafsiri maana ya kisiasa ya ushindani kati ya mwenyekiti Mbowe na Cecil Mwambe, mbunge wa chama hicho Jimbo la Ndanda mkoani Mtwara.

Nje ya kutwaa fomu kugombea nafasi ya uenyekiti wa taifa, siyo mmoja wa viongozi wa chama hicho wanaotambulika kwa urahisi miongoni mwa wapigakura au wananchi kwa jumla kama kiongozi wa kitaifa wa chama hicho, ambao wana sura za kitaifa na miaka mingi ya uongozi kando ya mwenyekiti huyo walijipima na kuona hawana sababu ya kuanzisha mvutano kama huo, hivyo wakakaa pembeni.

Ndizo dalili zinazojionyesha kuwa hapakuwa na mpinzani halisi kwa Mbowe, hata Tundu Lissu.

Somo la siasa katika suala hili ni kuwa kile kinachoitwa ukomo wa uongozi katika kundi fulani kimsingi ni jambo la kuachiwa wanachama wenyewe, kwani kuna ‘nguvu ya uvutano’ kati ya kiongozi wa chama na wale anaowaongoza na siyo rahisi atokee mtu mwingine apewe nafasi hiyo, labda awe na ngazi kubwa kitaifa.

Ndicho kilichotokea wakati (Edward) Lowassa alipopewa kadi ya Chadema na kuteuliwa papo hapo kuwa mgombea, kuwa ngazi yake ya uongozi kitaifa ilikuwa inamruhusu kuruka viunzi vyote vya kichama, kwa mfano kuaminiwa na watu, mchujo, n.k.

Waliosema kuwa uteuzi wake haukuwa wa kidemokrasia hawaijui siasa, kwani umaarufu wa mtu siyo ndani ya chama kwanza ila ndani ya nchi, na ndiyo maana mwenyekiti Mbowe akaondoa ushindani/mchujo, akamsimamisha.

“Katika nchi kama Tanzania jambo hilo halipo kwani wafuasi wa aliyeshindwa katika kinyang’anyiro hicho hawatazamii kabisa aonyeshe udugu au urafiki wa aina hiyo, mshikamano au chochote kingine.




Majeshi ya Umoja wa Mataifa ya kulinda amani nchini DRC (MONUSCO). **PICHA: MTANDAO**

## Askari wa UN kuendelea na ulinzi wa amani DRC

BARAZA la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) limeidhinisha nyongeza ya mwaka mmoja wa kulinda amani katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), huku Umoja wa Mataifa (UN) ukipunguza idadi ya jeshi na kuongeza maofisa wa polisi.

Baraza hilo limeidhinisha nyongeza ya mwaka mmoja wa kulinda amani nchini DRC.

Azimio lililowekwa katika rasimu ya Ufaransa, ambalo pia linaweka mkakati wa kuondoka nchini humo, lilikubaliwa kwa hiari na baraza la wanachama 15.

Balozi wa Afrika Kusini, Xolisa Mabhongo, akizungumza kwa niaba ya washirika watatu wa Baraza la Afrika, alipongeza mpango huu na kusema ni muhimu kujiondoa kwa Monusco kwa msingi wa mabadiliko, baada ya kufikiwa mafanikio katika mkutano wao.

Kwa upande wake, mwakilishi wa DRC, Paul Empole Losoko Elambe, amesema, “wazo la kulenga vikosi vya Monusco katika majimbo sita ambapo uwepo wa vikosi unadhaniwa kuwa ni muhimu sawia na ombi la serikali la kujikita zaidi katika majimbo ambayo yana kiwango cha juu cha vitisho na kupunguza uwepo wa jeshi katika maeneo ambayo si tishio tena.”

Kikosi cha Jeshi la Umoja wa Mataifa (MUNUSCO), kitapunguzwa kutoka askari 16,875 hadi 14,660.

Kulingana na mwanadiplomasia mmoja hatua hiyo ni “ishara nzuri” kwa ajili ya mabadiliko katika serikali mpya na kuimarishwa kwa usalama katika maeneo mengi. Vikosi vya UN vimefanikiwa kuzuia jaribio la baadhi ya mashambulizi DRC.

Katika rasimu hiyo, Baraza la Usalama linataka Sekretarieti ya UN, izingatie kupunguzwa zaidi kwa kiwango cha kupelekwa wanajeshi kwa kuzingatia mabadiliko mazuri ya hali nchini DRC, hasa katika mikoa ambayo inakabiliwa na tishio la vikosi vya wahalifu wenye silaha.

Rasimu hiyo pia inazingatia utafiti wa kimkakati wa kujitegemea nchini humo, uliofanywa hivi karibuni na inasema kwamba kuna haja ya kipindi cha chini cha mpito kwa takriban miaka mitatu na inasisitiza hitaji la kuhamisha kazi za Monusco hatua kwa hatua kwa serikali ya DRC.

Azimio hilo linaitaka serikali kumteua mratibu kuongoza juhudi za kudhibiti silaha na mipango ya kujumuisha kwa wapiganaji wa zamani, na kuanzisha kesi za kisheria dhidi ya wale wanaohusika na ukiukwaji wa haki za binadamu.

Bajeti ya Monusco ni karibu dola bilioni moja kwa mwaka na Umoja wa Mataifa umekuwapo kutekeleza kazi za kijeshi DRC kwa miaka 20 sasa.

**AFP**

TUJIKUMBUSHE

# Wafahamu wanaodaiwa kumuua mwanahabari Jamal Khashoggi

VYOMBO vya habari nchini Uturuki, vimewaorodhesha raia 15 wa Saudi Arabia, ambao mamlaka nchini humo zinawashuku kuhusika katika mauaji ya mwandishi wa habari Jamal Khashoggi.

Khashoggi raia wa Saudia, aliyekuwa mkosoaji kinara wa sera za Mwanamfalme Mohammed Bin Salman, mara ya mwisho alionekana akiingia ndani ya ofisi za ubalozi mdogo wa Saudia jijini Istanbul, Uturuki Oktoba 2 na kuuawa akiwa ndani.

Awali Saudia walidai kuwa mwanahabari huyo ambaye alikuwa akiishi Marekani, alitoka ndani ya ubalozi wake.

Baada ya shinikizo wakasema kuwa aliuawa alipojaribu kupambana na baadaye wakakiri kuwa aliuawa katika operesheni isiyo rasmi na ambayo haikubarikiwa na Bin Salman.

Wengi wa washukiwa hao 15 waliingia Uturuki saa chache kabla ya Khashoggi kuingia kwenye ofisi za ubalozi kufuatilia nyaraka kuhusu ndoa yake na kuondoka Uturuki siku hiyo hiyo wakitumia ndege binafsi za kukodi.

Mamlaka za Uturuki zinaamini kuwa washukiwa hao ni maofisa wa usalama na majasusi wa serikali ya Saudia, tuhuma ambazo zinathibitika kwa vyanzo vya kiupelelezi vilivyo wazi.

Washukiwa hao ni wafuatao;



**SALAH MUHAMMED A TUBAIGY (47)**

Dk. Tubaigy ni daktari bingwa wa uchunguzi wa magonjwa ya binadamu ikiwamo uchunguzi wa sababu za vifo.

Daktari huyo alipata shahada yake ya uzamivu kutoka Chuo Kikuu cha Glasgow, Uskochi na mwaka 2015 alifanya kazi kwa miezi mitatu katika kituo cha uchunguzi wa kitabibu cha Victorian nchini Australia.

Katika ukurasa wake wa Twitter, Tubaigy anajitambulisha kama mkuu wa Baraza la Wachunguzi wa Matibabu wa Saudia. Ukurasa huo una uhusiano na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Saudia.

Maofisa wa Uturuki, wanadai kuwa Dk. Tubaigy alitua katika uwanja wa ndege wa Istanbul akiwa na msumeno.

Daktari huyo aliingia Uturuki alfajiri ya Oktoba 2, na kufikia hoteli ya Movenpick iliyopo mita 500 kutoka katika ofisi za ubalozi wa Saudia. Aliondoka Uturuki siku hiyo hiyo saa 5 kasoro dakika nne usiku.

Inadaiwa sauti ya daktari huyo inasikika katika mkanda wa sauti ulionasa tukio la kuteswa kisha kuuawa kinyama kwa Khashoggi.

Yadaiwa sauti ya mtu anayetambulika kama daktari ilikuwa ikiwaita wengine wasikilize muziki, wakati akimkata Khasoggi vipande vipande.

Hata hivyo, Dk. Tubaigy hajazungumza kitu mpaka sasa, lakini mtu mmoja aliyejitambulisha kama mjomba wake ameandika mitandaoni kuwa daktari huyo hawezi kushiriki unyama kama huo.

**MAHER ABDULAZIZ MUTREB (47)**

Inaaminika alifanya kazi kwa miaka miwili katika Ubalozi wa Saudia jijini London, nchini Uingereza.

Chanzo kimoja cha mambo ya ujasusi kimeiambia BBC kuwa ni ofisa usalama Saudia na alikutana naye mwaka 2011, alipomfundisha matumizi ya teknolojia ya ujasusi iitwayo spyware.

Aidha, CNN pia wamemnukuu mtoa taarifa wao mmoja ambaye amemtaja Mutreb kuwa kanali wa kikosi cha ujasusi cha Saudia.

Picha mbalimbali zinaonyesha aliambatana na Bin Salman katika matukio matatu tofauti mwezi Machi mwaka huu, kitu kinachoashiria kuwa alikuwa sehemu ya ulinzi wa mwanamfalme huyo.

Gazeti lililo upande wa serikali ya Uturuki la Sabah limetoa picha za CCTV zinazoonyesha kuwa Mutreb aliingia ofisi ndogo za ubalozi Istanbul saa 4:55 asubuhi ikiwa ni takriban saa tatu kabla ya Khashoggi kuingia katika ofisi hizo.

Mutreb anaaminika kuingia Uturuki akitumia ndege moja na Dk. Tubaigy yenye namba ya usajili HZSK2 na alifikia Movenpick pia. Aliondoka na ndege nyingine ya kukodi ya HZSK1 SAA 12:40 jioni ya siku hiyo hiyo.

**ABDULAZIZ MOHAMMED M ALHAWSAWI (31)**

Gazeti la New York Times limemtaja jasusi mmoja wa Ufaransa ambaye amewahi kufanya kazi na familia ya Kifalme ya Saudia ambaye amemtambua Alhawsawsi kuwa mmoja wa walinzi wanaombatana na Bin Salman.

Alhawsawi aliingia Istanbul kwa kutumia ndege ya abiria usiku wa saa 7:43 na akafikia katika hoteli ya Wyndham Grand Istanbul Levant iliyopo kilometa moja kutoka ubalozi wa Saudia.

Aliondoka Istanbul kwa ndege ya HZSK2 pamoja na Dk. Tubaigy.

**THAAR GHALEB T ALHARBI (39)**

Mwezi Oktoba mwaka jana, mtu mwenye jina kama hilo ambaye alikuwa akifanya kazi katika kikosi cha ulinzi wa familia ya kifalme alipandishwa cheo kwa ushujaa wake katika kumlinda mwanamfalme Bin Salman.

Katika tukio hilo, mtu mwenye silaha aliwaua walinzi wawili kabla ya kuuawa.

Alharbi aliingia Uturuki na ndege ya HZSK2 na kufikia Mövenpick, kisha akaondoka na ndege ya HZSK1.

MOHAMMED SAAD H ALZAHRANI (30)

Mlinzi aliyevalia magwanda yenye jina kama hilo alipigwa picha na kurekodiwa akiwa na Bin Salman mwaka 2007, kwa mujibu wa mwanaharakati Iyad el-Baghdadi.

Alzahrani aliingia Istanbul kwa kutumia ndege ya kukodi na kufikia hoteli ya Wyndham Grand na kuondoka kwa kutumia ndege ya HZSK2.

KHALID AEDH G ALOTAIBI (30)

Gazeti la Washington Post liliripoti kuwa raia wa Saudia mwenye jina kama hilo aliingia nchini Uturuki mara tatu pamoja na wanafamilia ya kifalme ya nchi hiyo.

Aliingia na kutoka Istanbul kwa kutumia ndege za abiria siku hiyo hiyo. Naye pia alifikia katika hoteli ya Wyndham Grand.

NAIF HASSAN S ALARIFI (32)

Ukurasa wa Facebook wa mtu mwenye jina kama hilo unamwonyesha akiwa amevaa magwanda ya kikosi maalum cha kijeshi cha Saudia.

Aliingia Istanbul kwa kutumia ndege ya abiria na kufikia hoteli ya Wyndham Grand na kuondoka na ndege ya HZSK2.

**MUSTAFA MOHAMMED M ALMADANI (57)**

Almadani anasadikiwa kuwa jasusi wa Saudia na aliingia Istanbul kutumia ndege ya HZSK2 na kufikia hoteli ya Mövenpick. Aliondoka Istanbul kwa kutumia ndege ya abiria siku hiyohiyo.

**MESHAL SAAD M ALBOSTANI (31)**

Albostani anasadikiwa kuwa luteni katika jeshi la anga la Saudia.

Aliingia Istanbul kutumia ndege ya abiria na kufikia hoteli ya Wyndham Grand. Aliondoka na ndege ya HZSK2.

Oktoba 18, gazeti la Uturuki la Yeni Safak liliripoti kuwa Albostani alifariki katika ajali ya gari yenye utata jijini Riyadh, lakini hawakutoa maelezo zaidi.

**WALEED ABDULLAH M ALSEHRI (38)**

Mtu mwenye jina kama hilo alipandishwa cheo katika jeshi la anga na Bin Salman mwaka jana, vyombo vya habari vya Saudia viliandika.

Alsehri aliingia Istanbul kwa ndege ya HZSK2 na kufikia Mövenpick, aliondoka na HZSK1.

**MANSOUR OTHMAN M ABAHUSSAIN (46)**

Mtu mwenye jina kama hilo alinukuliwa kama kanali katika kurugenzi ya ulinzi wa raia nchini Saudia na moja ya magazeti ya nchi hiyo mwaka 2014.

Abahussein aliingia Istanbul kwa kutumia ndege ya abiria na kufikia hoteli ya Wyndham Grand na kuondoka na ndege ya HZSK2.

FAHAD SHABIB A ALBALAWI (33)

Albalawi ni jasusi wa Saudia na aliingia na moja ya ndege za kukodi na kufikia Mövenpick. Aliondoka na ndege ya HZSK1.

**BADR LAFI M ALOTAIBI (45)**

Alotaibi aliingia Istanbul kwa HZSK2 na kufikia Mövenpick, aliondoka kwa HZSK1.

SAIF SAAD Q ALQAHTANI (45)

Kwa mujibu wa Washington Post, Alqahtani anafanya kazi na Bin Salman. Aliingia Uturuki na HZSK2 na kufikia Movenpick na kuondoka na ndege ya abiria.

**TURKI MUSERREF M ALSEHRI (36)**

Alsehri aliingia Istanbul kwa HZSK2 na kufikia Mövenpick, aliondoka kwa HZSK1. BBC

UCHAMBUZI

Na Mwandishi Wetu

# Kwa hili Chadema ni sawa, swali mlikuwa wapi lakini?



Katibu Mkuu wa Chadema, John Mnyika. **PICHA: MTANDAO**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kilihitimisha uchaguzi wa viongozi wake ngazi ya taifa wiki iliyopita, huku kukiwa na hotuba mbalimbali kutoka kwa wanachama na wageni waalikwa.

Moja ya hotuba hizo ni ya Mwenyekiti wa Chadema Taifa, Freeman Mbowe, ambayo alitoa mbele wajumbe wa mkutano mkuu wa uchaguzi, baada ya kutetea nafasi hiyo, atakayoishikilia kwa miaka mingine mitano ijayo.

Kwenye sehemu ya hotuba yake alioitoa katika mkutano huo, Mbowe anasema, wao kama Chadema wameamua chama kisiendelee kuwa cha viongozi bali sasa kiwe ni cha wanachama.

"Chadema chama ambacho tuliamua kwa makusudi kabisa, kwamba chama kisiendelee kuwa chama cha viongozi, chama kiwe cha wanachama," anasema kwenye sehemu ya hotuba yake.

Uamuzi huo ni mzuri, hasa kwa kuzingatia kwamba uhai wa chama ni wanachama tena imara, lakini kikiwa cha viongozi hakiwezi kuwa imara, kitabaki kuwa cha mashabiki tu.

Kama Chadema ndio wameshtuka sasa na kuamua kushusha chama kwa wanachama, basi hii ni sawa na kukumbuka shuka kukiwa kumekucha, kwani kilitakuwa kuwa cha wanachama tangu kilipoanzishwa.

Mtindo wa kufanya chama kuwa cha viongozi ni kosa la kiufundi, ambalo inawezekana kusababisha chama kujulikana juu tu wakati ngazi ya chini hakipo, hivyo kuliona hilo ni hatua nzuri ingawa imechukua muda mrefu.

**MANUFAA**

Njia kuu ya chama kuwa cha wanachama, ni kujiimarisha kimtandao kuanzia ngazi ya shina hadi taifa, hatua ambayo inaweza kukifanya kiendelee kuwa imara na kuongeza idadi ya wanachama wapya na kuwa kimbilio la wananchi.

Katika mfumo huu, chama kinaweza kuaminiwa na Watanzania wengi na kukipa kura za kukiwezesha kuunda serikali, kutokana na imani ya wananchi juu ya chama hicho.

Iwapo Mbowe alikuwa na maana ya kwamba kwa muda mrefu Chadema kilikuwa chama cha viongozi, basi uamuzi mpya unaweza kusaidia kukiletea mabadiliko makubwa hapo baadaye.

Miongoni mwa mabadiliko hayo ni kuongeza wanachama wengi zaidi, kwa vile chama kitakuwa kwa wanachama, ambao kimsingi hawako juu bali wanapatikana ngazi za chini kuanzia kwenye mashina.

Pamoja na kwamba CCM ndiye mpinzani mkubwa wa Chadema, nadhani siyo vibaya kujifunza uzoefu kutoka kwa CCM ambayo imejiimarisha kuanzia ngazi ya chini kabisa ikiwa na wajumbe wa nyumba kumi.

Kujiimarisha kwa CCM kumeisaidia ijulikane hadi kwa watoto wadogo, hivyo si vibaya kuiga uzoefu huo na kuufanyia kazi kwa kutambua kuwa kwa kawaida wanachama wako ngazi ya chini.

Mfumo huo umekifanya Chama tawala kuendelea kushika dola licha ya upinzani mkali kutoka vyama vingine vya siasa, kwani kimejiimarisha kuanzia ngazi ya chini.

Inawezekana ndiyo maana ni cha pili kwa ukubwa barani Afrika kikitanguliwa na African National Congress (ANC) cha Afrika Kusini, hivyo si vibaya vyama vingine kuiga mfano na ikiwezekana kuboreshwa pale inapoonekana kuna kasoro.

Kwa kuwa chama hicho kimemaliza uchaguzi na kusema kimeamua kwa makusudi kiwe ni cha wanachama, basi hilo liandane na ubunifu wa kukiwezesha kuwa imara zaidi.

**CHANGAMOTO**

Chama kutokuwa cha wanachama kuna matatizo yake ikiwamo viongozi kutowajibika kwa wanachama na kutotii kile ambacho wanachama wanataka, bali kuamua mambo wanavyotaka wenyewe.

Lakini chama kikifuata mfumo wa kuwa cha wanachama, utasaidia kujiimarisha, kutokana na ukweli kwamba kisiasa mfumo huo unafanana na maendeleo ya nchi ambayo yanategemea kodi za wananchi.

Hivyo maendeleo ya chama yanategemea ada za wanachama na michango mingine, ambayo ni muhimu, na kama viongozi wa Chadema wamegundua kosa na kuchukua hatua hizo, ni sahihi ingawa wamechelewa.

> "Chadema chama ambacho tuliamua kwa makusudi kabisa, kwamba chama kisiendelee kuwa chama cha viongozi, chama kiwe cha wanachama," anasema kwenye sehemu ya hotuba yake.

Bila kuchukua hatua hizo, matokeo yake ni chama kutotii sauti au matakwa ya wanachama, ambao kimsingi ndiyo wenye chama na kubaki kusikiliza tu kile ambacho viongozi wanaamua bila wao kushirikishwa.

Ni muhimu chama kujitegemea kwa fedha na katika mambo mengi, kwa kutumia wanachama wake kama, ambavyo ni wajibu kwa chama cha siasa kuwatumikia wanachama wake na wananchi kwa ujumla.

Hayo yote kama nilivyosema, hayana budi kuendeshwa kwa kutegemea zaidi michango ya wanachama, si kuwa na mashabiki tu, ambao wakati mwingine wanaweza kukimbia kwa vile hawana uchungu na chama.

Lakini ni lazima uendeshaji wa chama cha siasa ulingane na hali ya kiuchumi ya chama chenyewe na wanachama kwa ujumla na si kuwakamua kutoa hata kile wasichokuwa nacho.

**HISTORIA**

Historia inaonyesha kuwa Chadema ilianzishwa mwaka 1992, ikiwa chini ya uenyekiti wa aliyewahi kuwa Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Edwin Mtei, ikiwa na falsafa ya nguvu ya umma.

Kwa imani kwamba umma ni sehemu ya serikali inayotoa ridhaa ya maamuzi na ruhusa ya mfumo wowote huku itikadi ikiwa ni mlengo wa kati unaoamini katika soko huria lenye kusimamiwa.

Baadaye mwaka 1998 nafasi ya mwenyekiti wa chama hicho taifa ilichukuliwa na Bob Makani ambaye alishika wadhifa huo hadi mwaka 2003 alipomaliza muda na kuamua kuendelea na kazi zake kama mwanasheria wa kujitegemea.

Mkongwe huyo alibaki kuwa kiongozi na mshauri wa chama hadi alipokutwa na umauti huku nafasi ya mwenyekiti wa chama taifa ikiwa tayari imeshachukuliwa na Mbowe, ambaye hadi sasa ni mwenyekiti.

Chama kilianza kushiriki uchaguzi mkuu wa kwanza ndani ya mfumo wa vyama vingi uliofanyika mwaka 1995, na katika uchaguzi huo kilipata wabunge wanne na madiwani 42.

Uchaguzi wa mwaka 2000, chama hicho kilipata wabunge watano na madiwani 75, kisha uchaguzi wa mwaka 2005, chama hicho kiliendelea kuongeza idadi ya wabunge wakafikia 19, huku madiwani wakiwa ni 103 na uchaguzi wa mwaka 2010 kilipata wabunge 24, na mwaka 2015 kikavuna wabunge 34.

# Johnson amaliza hatua ya kuitoa Uingereza EU Januari 2020

**Na Nimi Mweta**



Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson. **PICHA: MTANDAO**

KUKAMILISHA 'Brexit' sasa kuko bayana baada ya Boris Johnson kukiongoza chama cha Conservatives kupata ushindi mkubwa ambao chama hicho hakikuwahi kufikia tangu ashinde Margaret Thatcher na chama hicho mwaka 1979.

Akiwa na ushindi wa zaidi ya viti 300 wakati chama kiongozi cha upinzani hakifiki viti 250, takriban kila hatua atakayoamua kuchukua katika mchakato wa kuondoka Umoja wa Ulaya na kufikia mkataba mwingine wa biashara, kwa mfano ule unaopigiwa chapuo wa 'soko huria' kati ya pande hizo mbili sasa ana uhakika wa kushinda.

Dhamira ya kutaka Brexit ikamilike ilivuta wapigakura kuachana na Labour, wakisitasita tu.

Wachunguzi wanasema waziri mkuu huyo anaelekea kupata 'Brexit laini' ambako Uingereza inabaki katika soko la pamoja (kama umoja huo ulivyokuwa zamani, kabla ya kuongeza uhuru wa kwenda kokote ndani ya nchi wanachama, n.k.).

Jitihada za kuwa na 'Brexit ngumu' kwa maana ya kuondoa mahusiano ya kina na umoja huo na kuanza kutafuta au kufanikisha azma tofauti katika biashara ilikuwa ni moja ya sababu za mifarakano katika Bunge lililopita, na hata ndani ya chama tawala cha Conservative.

Brexit laini itatuliza washikadau hasa wenye viwanda wanaohofia kuwekewa ushuru wa forodha na kukwama kuuza bidhaa kwa wingi soko la Ulaya.

Wingi wa wabunge wa Conservative katika kupigia kura muswada wa kujitoa EU uliokuwa katika hatua ya kwanza, katika Bunge hilo ambalo pia lilikuwa na spika mpya baada ya yule mtanashati Jim Bercow kujiuzulu, aliyemgomea Johnson elekezo la kusimamisha Bunge kwa muda, akaenda mahakamani.

Johnson alishindwa na Bunge likaendelea na kazi, wakamsakama kila hatua ya makubaliano na EU, akasisitiza ufanyike uchaguzi mwingine wa wabunge, akiwa anaona upepo unaenda upande wake.

Uchaguzi wa wabunge wa EU uliwapa waunga mkono Brexit viti vingi, na wanaositasita wakapoteza nafasi zao na Labour ilipokubali ikanyong'onyea.

Kupita kwa muswada huo katika hatua ya kwanza kunaleta hisia kuwa kazi iliyobaki ni utaratibu tu kufuatwa kwani kishindo cha ushindi wa Conservative kiliainisha kuwa suala hilo sasa ndiyo tamati yake.

Kinachotakiwa ni kukamilisha utaratibu huo ili Umoja wa Ulaya na Uingereza watie saini rasmi makubaliano ya kusitisha uanachama wake EU ifikapo Januari 31, na pia kuanza hatua za awali za kufikia makubaliano mapya ya soko la pamoja, lisilo na viambatanishi vya umoja wa kisiasa kwa sehemu kubwa, hasa katika masuala ya uhamiaji, uraia, n.k..

Katika upigaji kura bungeni, wabunge sita wa Labour walijiunga upande wa Conservatives kukubali muswada.

Ilikuwa siyo rahisi kwa wabunge hao kukubaliana na muswada huo, vile kulikuwa na maelekezo ya kina kutoka kwa viongozi wa chama hicho, wazee au wanachama waandamizi, hasa kwa vile muswada huo unaonekana kupunguza kulinda haki za wafanyakazi.

Wakati hapakuwa na yeyote kati ya wabunge walioacha msimamo wa Conservatives kupiga kura kupinga muswada, wabunge wa Labour hawakuwa na uwezo wa kusimamia msimamo wa chama chao, kwani wengi kati ya wapiga kura wao wanaunga mkono mwelekeo huo.

Waliounga mkono walizidi kwa kura 124 kuingiza muswada katika kusomwa mara ya pili, wakati waliounga mkono kwa jumla walikuwa 358 na waliopinga wakawa 234. Baadhi ya wabunge wa Labour hawakuwapo kwa kukata tamaa.

Juhudi za awali za kukamilisha Brexit zilikwama kwa sababu vyama vilikuwa vina nguvu karibu sawa bungeni, na baadhi ya wabunge wa Conservatives walikuwa wanahama chama chao katika kura hizo wanapiga kura na upinzani.

> Kupita kwa muswada huo katika hatua ya kwanza kunaleta hisia kuwa kazi iliyobaki ni utaratibu tu kufuatwa kwani kishindo cha ushindi wa Conservative kiliainisha kuwa suala hilo sasa ndiyo tamati yake.

Ikafika wakati ndugu wa kuzaliwa wa Boris Johnson ambaye alikuwa katika Baraza la Mawaziri kuanzia wakati wa Waziri Mkuu Theresa May aliyejiuzulu kwa kushindwa kukamilisha Brexit kwa Bunge kukubali mkataba aliofikia na Umoja wa Ulaya, akajiuzulu uwaziri.

Alisema hawezi kuendelea katika hali ya kumpinga kaka yake kisiasa na huku anamuunga mkono na kumtakia heri kama ndugu yake, akaona aondoke.

Akipokea ushindi huo na kusisitiza msimamo wa umoja bungeni, Johnson alisema kuwa hakuna haja ya kuendelea na harakati za 'leave' (ondoka) na 'remain' (bakia) yaani katika Umoja wa Ulaya na badala yake Waingereza waungane kuwa kitu kimoja kwa ajili ya taifa, baada ya kura kumaliza utata huo.

Alieleza kuwa kukamilisha mchakato wa Brexit itakuwa ni sura mpya katika historia ya nchi hiyo, kujenga uhusiano mpya na Ulaya, kusimama wima katika masuala ya dunia na kuanza kazi ya kuponya majeraha ya mvutano huo katika jamii kwa miaka kadhaa.

Inatazamiwa kuwa sehemu iliyobaki ya kupitishwa muswada huo itakamilika bungeni kabla ya Januari 9 ili kuufikisha baraza la juu la Bunge (House of Lords), na Malkia Elisabeth atie saini.

Bado kuna matatizo mbele ya safari kwani soko la pamoja na Ulaya siyo kazi rahisi kufikia, kutokana na nchi wanachama kutotaka kutoa 'zawadi' yoyote kwa Uingereza kwa uamuzi wa kujitoa EU.

Baadhi wanasema kuwa azma ya Johnson ya kufikia mustakabali mpya na umoja huo kabla ya mwisho wa mwaka unaoanza wiki ijayo haitafikiwa kwa urahisi na huenda ikwame kwani kilichofikiwa hadi sasa ni vipengele kuhusu 'mpaka laini' wa Ireland ya Kaskazini na Jamhuri ya Ireland.

Ina maana bado kuna hatari ya kuondoka EU bila mkataba halisi endapo majadiliano ya kuundwa kwa soko huria kati ya pande hizo mbili yakishindikana au yahitaji muda zaidi ya miezi 11 ya mwaka 2020.

Kuna mivutano mingi inayohitaji Uingereza ielekee, kwa mfano kuwa na uhusiano maalum wa kiuchumi na Marekani, wanaouhofia Waingereza.



# JPM aombwa kutatua mgogoro wa ardhi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Mtaa wa Pambogo katika Kata ya Kyela jijini Mbeya, wamemwomba Rais John Magufuli kuingilia kati kutatua mgogoro wa ardhi unaofukuta baina yao na Halmashauri ya Jiji la Mbeya kwa madai kuwa Jiji hilo linataka kuwapora eneo lao lenye ukubwa wa hekta 22.

Eneo wanalolalamikia wananchi hao ni lile lililokuwa la tahadhari (Buffer zone), wakati Uwanja wa Ndege wa zamani wa Mbeya ulipokuwa unatumika ambapo wananchi hao wanadai ni la kwao la asili na walikuwa wanalitumia hata wakati uwanja unatumika. Mmoja wa wazee wa eneo hilo, Anyitike Mwaikambo, alisema awali hata eneo ilipojengwa Shule ya Msingi Pambogo lilikuwa la kwao, lakini kutokana na uhitaji wa shule waliamua kulitoa bure na wakashirikiana na serikali kujenga shule hiyo.

Hata hivyo, alisema sehemu ya eneo hilo walilokuwa wameligawa kwa ajili ya kujenga nyumba za walimu, liliuzwa na baadhi ya watumishi wa Jiji na walionunua wamejenga makazi, lakini bado Jiji halithamini mchango wao na linataka kuwapora eneo lililobakia.

Alisema kwa muda mrefu wamekuwa wakifuatilia serikalini wapimiwe eneo hilo ili waendelee na ujenzi wa makazi baada ya uwanja kufungwa, lakini wamekuwa wakipigwa chenga, na kwamba wana nyaraka mbalimbali zinazoashiria kuwa eneo ni la kwao. "Wamekuwa wakitupiga chenga tunapotaka tupimiwe, sasa kilichotushtua zaidi ni wataalamu wa Jiji wamekuja wameweka mabango usiku yanayosema 'ni marufuku kuendelea kulima katika eneo hili' sasa tumekwama na hatuelewi chochote," alisema Mwaikambo.

Naye Mzee John Mwanguku alisema wao ni wazaliwa wa eneo hilo na walikuwa wanayalima mashamba hayo kwa muda wote bila kubugudhiwa na mtu lakini shida iliibuka mwaka 2017 baada ya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Amos Makalla kuzuia wasipimiwe na kumilikishwa.

Alisema walikuwa tayari wameshapimiwa viwanja 76 na kilichokuwa kimebakia ilikuwa ni kupewa hati na Ofisi ya Kamishna wa Ardhi wa Kanda, lakini Makalla akazuia kwa maelezo kuwa ni eneo la uwanja wa ndege.

"Kuna baadhi ya familia zina makaburi yao hapa, tumejaribu kumfuata Mkuu wa Mkoa lakini anatupiga chenga, hataki kuonana na sisi na hata kwenye chama tumefikisha malalamiko yetu lakini hatujapata msaada, sasa tunamwomba Rais Magufuli atusaidie," alisema Mwanguku.

Naye Nicholas John alisema yeye ni kizazi cha tatu na amezaliwa akijua kuwa eneo hilo ni mali yao na kwamba walipofuatilia walibaini kuwa Mpango Kabambe wa Jiji la Mbeya wa mwaka 1984 hauonyeshi kuwa eneo hilo ni sehemu ya uwanja wa ndege.

Alisema wamepata taarifa kuwa serikali inataka kujenga shule katika eneo hilo, huku wakiwa hawajafikia mwafaka wa mgogoro uliopo na dalili zimeanza kuonekana kwa watendaji wa Jiji kuweka mawe mapya pamoja na kurundika makontena katika eneo hilo. Alisema kwa mujibu wa sheria za nchi ni kwamba serikali ikitaka kulitumia eneo la wananchi ni lazima iwafidie, lakini wao hakuna mazungumzo yoyote ya aina hiyo na kwamba baadhi ya wazee waliohamishwa kupisha eneo la Shule ya Pambogo hawajalipwa pia. Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliwatahadharisha wananchi hao kutoisumbua serikali kwa maelezo kuwa eneo hilo ni la umma na serikali imeamua kujenga shule.

Alisema alichokibaini ni kwamba wananchi hao walishirikiana na watumishi wachache wa serikali ambao aliwaita wahuni kutengeneza nyaraka za uongo kwa madai kuwa zipo nyaraka ambazo zinaonyesha eneo hilo ni la umma, lakini baadaye zikatengenezwa ambazo zinaonyesha viwanja. "Wakiendelea kusumbua watacharazwa bakora za kutosha na wiki lijalo vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), wanaingia kuvuruga kwa ajili ya kuanza ujenzi wa shule ya msingi na baadaye tutajenga na sekondari," alisema Chalamila.




Maaskari wa Jeshi la Polisi mkoani Mbeya wakipita na magari katika mitaa mbalimbali ya Jiji la Mbeya jana, kwa ajili ya kuonyesha utayari wa kukabiliana na matukio ya uhalifu wakati wa sikukuu za mwisho wa mwaka. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

## Mbaroni tuhuma za meno ya tembo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za kukutwa na vipande 11 vya meno ya tembo.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema jana kuwa watuhumiwa hao walikamatwa Desemba 21, mwaka huu majira ya saa 12:30 jioni katika eneo la Soweto jijini Mbeya.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni, Abdulmark Upete (41) Mkazi wa Uyole jijini Mbeya, Mohamed Omary (50) mkazi wa Kilosa mkoani Morogoro, Ayoub Kindumba (49) mkazi wa Ilembula mkoani Njombe na Lawi Kalonga (50) mkazi wa Jiji la Dodoma.

Alisema watuhumiwa walikuwa wanasafirisha pembe hizo kutoka mkoani Njombe kuingia jijini Mbeya na kwamba upelelezi unaendelea ili kujua walikokuwa wanapeleka baada ya kuingia nazo Mbeya.

Alisema watu hao walikamatwa kufuatia mtego uliokuwa umewekwa na Jeshi la Polisi baada ya kuushtukia mtandao huo na ndipo walipofika eneo la Soweto wakanaswa.

"Walipofika Mbeya walizihifadhi nyara hizi kwenye mfuko wa sandarusi na kisha wakaficha kwenye duka la kuuza vipuri vya magari mali ya Upete na yawezekana walikuja nazo huku kwa ajili ya kutafuta wateja," alisema Matei.

Alisema upelelezi unaendelea, na baada ya kukamilisha watuhumiwa watafikishwa mahakamani.

# RC apiga jeki mabati 3,000 madarasa kidato cha kwanza

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

OFISI ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, imekabidhi mabati 3,000 kwa wakuu wa wilaya zote za mkoa huo kwa lengo la kuharakisha ujenzi wa vyumba kwa ajili ya wanafunzi waliofaulu mitihani ya darasa la saba na kutakiwa kujiunga na masomo ya sekondari mwezi Januari, lakini majina yao yamezuiliwa kutokana na uhaba wa vyumba.

Takwimu za mkoa huo zinaonyesha watoto 2,716 waliofaulu majina yao yamezuiliwa kutokana na uhaba wa vyumba na kwamba ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi hao vinahitajika vyumba vya madarasa 59 ambavyo ujenzi wake unaendelea katika hatua mbalimbali.

Akikabidhi bati hizo juzi, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema mabati hayo ni sawa na bando 250 zenye bati 12 kila moja na kwamba thamani ya mabati yote ni Sh. milioni 72.5 na kwamba lengo ni kupunguza tatizo na sio kulimaliza kabisa.

Alisema fedha zilizotumika kununua bati hizo zimetokana na vyanzo mbalimbali vya mapato na kwamba sio pesa kutoka katika mfuko wake binafsi.

Alisema kwenye mgawo wa mabati hayo, Halmashauri ya Mbarali ambayo inadaiwa vyumba 36 imepewa bando 70, Jiji la Mbeya na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya zimepewa kila moja bando 55, Kyela, Busokelo na Chunya kila moja bando 15 na Wilaya ya Rungwe bando tida.

Alisema bando zingine zimegawiwa kwa shule moja moja ikiwemo Shule ya Sekondari ya Uporoto iliyopo wilayani Rungwe ambayo inamilikiwa na Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambayo ilipewa bando nane.

"Tunataka watoto wetu waanze masomo mapema, tutaangalia maendeleo kufikia mwezi Januari ili kama bado kutakuwa na uhitaji tusaidie tena, kwa sasa wakuu wa wilaya na wasaidizi wao wakapambane kwanza," alisema Chalamila.

Alisema baada ya kukamilisha vyumba hivyo zipo fedha zingine ambazo zitatumika kutengeneza madawati, kujenga maabara za kisasa na kununua vitabu hasa vya masomo ya sayansi.

Akizungumza kwa niaba ya wakuu wa wilaya wote, Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Chalya, ambaye ndiye mwenyekiti, alisema mabati hayo yatasaidia kupunguza tatizo kwa kiwango kikubwa.

Alimshukuru Mkuu wa Mkoa kwa juhudi zake za kutafuta fedha kupitia katika vyanzo mbalimbali vya mapato kwa ajili ya kuhakikisha vyumba vya madarasa vinakamilika mapema na watoto wanaanza masomo mapema kama ilivyoagizwa na serikali.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Francis Mtega, alisema katika halmashauri hiyo mbali na mabati hayo waliyopewa pia hata wao wanaendelea na michakato mingine ya kukamilisha vyumba hivyo.



HABARI DODOMA

# Waziri aonya wasaka vyuma chakavu katika miundombinu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, George Simbachawene, amekemea watu wanaojihusisha na vitendo vya kuhujumu miundombinu ya umma na ya watu binafsi ili kupata chuma chakavu, akiwataka kuviacha mara moja.

Vilevile, amezitaka mamlaka za serikali za mitaa, zifuatilie watu binafsi, kampuni na viwanda kuhakikisha kuwa sheria na kanuni za udhibiti wa taka hatarishi zinazingatiwa ipasavyo ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira.

Alitoa agizo hilo jijini hapa jana ofisini kwake alipotoa taarifa kuhusu kanuni za udhibiti na usimamizi wa taka hatarishi za mwaka 2019, kanuni za udhibiti na usimamizi wa taka za kielektroniki za mwaka 2019 na kanuni za ada na tozo za usimamizi wa mazingira za mwaka 2019 ambazo zimerekebishwa.

Alisema hatua iliyochukuliwa na ofisi hiyo ya kufanya marekebisho katika kanuni hizo na kuweka mfumo bora wa kisheria wa kusimamia taka hatarishi ili si tu kuhakikisha mazingira yanalindwa na kusimamiwa, bali pia miundombinu ya nchi inalindwa ipasavyo.

"Kama inavyofahamika, mojawapo ya taka hatarishi ni chuma chakavu, kuna baadhi ya wafanyabiashara na watu ambao siyo waaminifu, wanafanya biashara hii bila kuwa na vibali husika, lakini wapo ambao wana vibali, lakini hawafuati masharti yaliyowekwa chini ya vibali hivyo," alisema.

Waziri huyo aliwataka baadhi ya wanaofanya biashara hiyo huku wakikwepa kulipa kodi stahiki, kuacha udanganyifu huo kwa kuwa sasa serikali imeweka mfumo wa kiutawala, kisheria na kikanuni ambao siyo rahisi kufanya udanganyifu huo tena bila kugundulika.

Aliongeza kuwa katika kuboresha usimamizi wa mazingira, ofisi yake imefanya marekebisho ya kanuni mbalimbali pamoja na kutunga kanuni mpya zikiwamo za udhibiti na usimamizi wa taka hatarishi.

Simbachawene alifafanua kuwa kanuni mpya za mwaka 2019, zimeainisha aina ya shughuli za usimamizi wa taka hatarishi ambazo zinapaswa kuwa na kibali cha waziri mwenye dhamana ya mazingira.

Alizitaja shughuli zinazopaswa kuombewa kibali ndani ya nchi kuwa ni kukusanya, kutunza, kusafirisha na kumiliki au kuendesha mtambo wa usimamizi wa taka hatarishi.

Alisema shughuli za usafirishaji nje ya nchi, kuingiza au kupitisha nchini taka hatarishi, pia zinapaswa kuombewa kibali ambacho pia hutolewa na waziri husika na zimeelekeza shehena yoyote ya taka hatarishi itakayoingizwa au kupitishwa nchini bila kufuata masharti ya kanuni hizi, itachukuliwa kuwa ni usafirishaji haramu wa taka hatarishi na zinapaswa kurejeshwa katika nchi zilikotoka kwa gharama za msafirishaji.

Waziri Simbachawene aliongeza kuwa kanuni hizo zimeweka adhabu kali zaidi kwa makosa ya kutokuwa na kibali cha kusimamia taka hatarishi nchini zikiwamo faini kuanzia Sh. milioni tano hadi bilioni 10 au kifungo kisichozidi miaka 12 au vyote kwa pamoja.

"Napenda kusisitiza kuwa hatua hii iliyochukuliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais ya kufanya marekebisho katika kanuni hizi na kuweka mfumo bora wa kisheria wa kusimamia taka hatarishi, inalenga siyo tu kuhakikisha kuwa mazingira yanalindwa na kusimamiwa, bali pia miundombinu ya nchi inalindwa ipasavyo," alisema.

"Kama tunavyofahamu, mojawapo ya taka hatarishi ni chuma chakavu, kuna baadhi ya wafanyabiashara na watu ambao siyo waaminifu wanafanya biashara hii bila kuwa na vibali husika, lakini pia wapo ambao wana vibali lakini hawafuati masharti yaliyowekwa chini ya vibali hivyo.

"Moja ya sharti muhimu ni kwamba kila mwenye kibali cha chuma chakavu, anapaswa kutoa taarifa ya chanzo cha chuma chakavu hicho na mahali anapokipeleka.

Na hiyo inafanyika kwa kujaza 'tracking form' Na. 3, kutokufanya hivyo ni kosa kubwa chini ya kanuni hizi," alitahadharisha.



Wakazi wa kijiji cha Chipogoro wilayani Mpwapwa wakiondoa baadhi ya miti na mbao zilizokuwa zimesombwa na maji ya mafuriko yaliyotokea juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Askofu aona 'bomu' watoto wa mitaani

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Pentecostal Holiness Association Kanda ya Kati, Julius Bundala, ameiomba serikali, taasisi za kidini na mashirika yasiyo ya kiserikali, kuchukua hatua dhidi ya ongezeko la watoto wa mitaani ili kuliepusha taifa kutengeneza bomu litakalolipuka baadaye.

Askofu Bundala alisema hayo wakati wa semina elekezi iliyoambatana na maandalizi ya msimu huu wa sikukuu za mwishoni mwa mwaka na mwaka mpya iliyofanyika katika kanisa hilo jijini Dodoma.

Alisema serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi za kidini zina wajibu kuangalia kundi hilo linaloishi mitaani, akieleza kuwa kwa sasa linazidi kuongezeka.

Alisema kundi hilo likiachwa bila kuangaliwa kwa umakini, kuna hatari taifa na jamii kukawa na vijana watakaoigharimu serikali, taasisi na mashirika baadaye.

Aliwataka wazazi na walezi kukaa pamoja na watoto ili kuwaepusha kujiingiza kwenye makundi maovu. "Tatizo kubwa lililopo kwa baadhi ya wazazi na walezi hawana ukaribu na watoto, hivyo watoto hujikuta wakiangukia mikononi mwa shetani," alisema.

Askofu huyo pia aliwakumbusha wazazi kuchukua tahadhari ya matumizi ya fedha kipindi hiki cha sikukuu, akiwataka kujiwekea akiba ya kutosha ya fedha kwa ajili ya maandalizi ya masomo ya wanafunzi. "Pamoja na uzuri wa sherehe hizo mbili, lakini ni muhimu tukawakumbuka watoto wetu, wakafanyiwa maandalizi ya kutosha yanayohusu masomo," alishauri.

Askofu huyo pia alitumia nafasi yake kuwaonya Wakristo kuhusu matendo maovu kwenye kipindi chote cha sikukuu hizo.

## TCRA yaonya wasambazaji picha za utupu mitandaoni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA), imewataka wananchi kuacha kuwanyanyasa wanawake kijinsia kwa kutuma picha za utupu mitandaoni pale wanapokuwa wamesitisha uhusiano wa kimapenzi, badala yake watumie mitandao hiyo kufanya maendeleo.

Ofisa Mwandamizi Mkuu wa TCRA, Semu Mwakyanjala, aliyasema hayo wakati wa mkutano wa wawakilishi wa vyuo vya elimu ya juu uliofanyika jijini juzi, kwa lengo la kutokomeza rushwa ya ngono vyuoni na sehemu za kazi.

Mwakyanjala alisema jamii inapaswa kupunguza kuweka mitandaoni mambo binafsi badala yake iitumie mitandao hiyo kuweka vitu vya msingi ambavyo vitawapa manufaa makubwa katika maisha yao ya kila siku.

"Tanzania tuna uhuru mkubwa sana wa kufanya vitu katika mitandao, tutumie nafasi hii kufanya maendeleo kupitia mitandao na siyo 'kuposti' vitu vya kuumizana, havina faida yoyote," alishauri.

Alisema mfumo wa matumizi ya kimtandao umekua kwa kiasi kikubwa na umeleta faida kubwa kwa jamii kutokana na kuokoa muda wao hasa pale wanapoitumia kulipa bili mbalimbali badala ya kupanga foleni kulipia huduma hizo.

Hata hivyo, alieleza kusikitishwa na baadhi ya watu ambao hawaoni umuhimu wa kufanya vitu hivyo badala yake wanaitumia mitandao kufanya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake wanaokuwa nao katika uhusiano ya kimapenzi.

"Jamii punguzeni kupiga picha za ovyo unapokuwa na mpenzi wako au mwenzi wako, fanyeni mambo ya msingi ili kuepuka udhalilishaji na ukatili wa kijinsia," alishauri.

"Naomba watu wanaofanya hivi waache tabia hiyo kwa sababu wanachangia kukatiza ndoto za watu," alieleza ofisa huyo na kufafanua kuwa wengi wanaokumbwa na adha hizo, wamekuwa wakijiua, wengine kukatisha masomo.

"Jamii tuhakikishe kwamba hatuposti picha za namna hiyo, tunapaswa kutafuta maendeleo na elimu ya kujiendeleza kwenye mitandao kama wanavyofanya wengine," alisema.



## Walimu waaswa kuwapenda wenye mahitaji maalumu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISA Mdhamini Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale Pemba, Khatib Juma Mjaja, amewataka walimu wanaowafundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum kuwapa taaluma na kuwalea ili kuonyesha upendo.

Alisema watoto wenye ulemavu wana haki sawa na wengine na endapo watazifuata mbinu za ufundishaji za wanafunzi hao wanaweza kufikia katika mustakabali wa kuyakabili maisha.

Aliyasema hayo wilayani Chakechake katika tamasha la wanafunzi wenye mahitaji maalum kisiwani Pemba.

Mdhamini huyo aliwataka wazazi na walezi wenye watoto wenye ulemavu kutowafungia ndani watoto hao kwa kuwa ni kuwakosesha haki zao za msingi ikiwamo elimu, huduma za afya na kuwaandikisha katika taasisi zao.

Mratibu Idara ya Michezo na Utamaduni, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba, Mzee Ali Abdalla, alisema jamii inapaswa kuwaunga mkono walimu wanaowafundisha wanafunzi hao kwa kuwa wana mchango mkubwa wa kufanya vyema kwa wanafunzi hao ikiwamo ufaulu wao na michezo.

Akisoma risala ya wanafunzi hao, mwalimu kutoka Shule ya Pandani, Wilaya ya Wete Pemba, Said Khamis, alisema wanaishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuanzisha kitengo maalum cha elimu mjumuisho ambayo inawapatia stadi mbalimbali za maisha na kuwatatulia changamoto zao zinazowakabili.

# Ahimiza mafunzo lugha ya alama

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mtendaji Kamisheni ya Maafa, Makame Khatib Makame, amesema watu wenye ulemavu wa kusikia wanahitaji kupewa mafunzo ya lugha za alama ili waweze kujinusuru wanapofikwa na matatizo.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Idara ya Ulemavu, Abeida Rashid, wakati wa kufunga mafunzo ya lugha ya alama kwa watu wenye ulemavu wa kusikia, alisema elimu hiyo ni ya lazima kupatiwa watu hao kwa lengo la kukuza lugha ya alama na kutumika kwenye jamii ili wanapofikwa na madhara waweze kufahamika. Alisema mafunzo hayo yanatoa mwanga wa kuelewa ili kutoa ushahidi mahakamani watu wenye ulemavu huo wanapofikwa na vitendo viovu hasa vya udhalilishaji ambavyo vimekithiri nchini.

"Mafunzo haya ya lugha ya alama, nakutakeni muyatumie vizuri ili muweze kutoa huduma kwa watu wenye ulemavu wa kusikia pale wanapofikwa na vitendo viovu ikiwamo vya udhalilishaji hasa panapotakiwa kutolewa ushahidi," alisema Mkurugenzi huyo.

Alisema serikali inaangalia fursa ya kutoa lugha za alama ili kutumika sehemu mbalimbali ikiwamo sehemu za mikutano, katika Baraza la Wawakilishi na sehemu nyingi zinazotumiwa na jamii.

Hata hivyo, aliwaomba watoaji wa mafunzo hayo kufahamu kukamilika kwa mafunzo hayo isiwe mwisho yawe endelevu na kutoa mafanikio zaidi.

Naye mwanafunzi wa mafunzo hayo, Fatma Said Khamis, akisoma risala aliitaka serikali ione umuhimu wa kuwapatia mafunzo ya ulemavu wa kusikia ili kuhudumia jamii na kuisaidia wanapofikwa na matatizo.

Alisema wanaomba mafunzo hayo yawe endelevu kwa serikali na binafsi ili waweze kutumia taaluma kwa watu wenye ulemavu wa kusikia kwa kuhakikisha wanapatiwa haki zao.

Kadhalika alisema wamefarijika kwa kupatiwa mafunzo hayo ya lugha za alama na kupata mwamko wa kutoa huduma kwa jamii. Waliishukuru Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Idara ya Watu wenye Ulemavu kwa kuwapatia mafunzo hayo ambayo watayafanyia kazi na kuwa walimu kwa wenzao.

Kwa upande wake mshiriki wa dawati la jinsia, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Salum Khamis Machano, alisema mafunzo hayo yatawasaidia hasa wanaokumbwa na vitendo vya udhalilishaji.

Mafunzo hayo ya siku 10 yamewashirikisha wadau mbalimbali wakiwamo Jeshi la Polisi, Mahakama, Wanasheria na Dawati la Jinsia.



Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja na Shughuli za Kanda, Salome Mallamia, akizungumza katika hafla ya utiaji saini mkataba wa makubaliano wa ununuzi wa dawa baina ya Wizara ya Afya na Bohari Kuu ya Dawa (MSD), hafla iliyofanyika katika ukumbi wa Wizara ya Afya Mnazi Mmoja Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Atahadharisha siasa za kibaguzi, uchochezi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Abdulla Juma Mabodi, amesema siasa za ulaghai na uchochezi wa vurugu zinazofanywa na upinzani visiwani Zanzibar, hazizuii ushindi wa CCM katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Amesema CCM kitapata ushindi wa kihistoria kwa

majimbo ya Unguja na Pemba ambao haujawahi kutokea toka kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi nchini mwaka 1992.

Kauli hiyo aliitoa wakati akifungua kongamano la Wiki ya Maskani ya CCM Kachorora, lililofanyika katika ukumbi wa kituo cha kulelea wazee Sebleni Wilaya ya Amani Zanzibar.

Alisema ushindi huo utapatikana kutokana na utekelezaji mzuri wa Ilani ya CCM ya mwaka 2015/2020 kwa wananchi wote mijini na vijijini, ambao kila mwananchi kwa sasa ananufaika na huduma muhimu za kijamii zilizoimarishwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alieleza kuwa hakuna chama cha siasa chochote duniani kilichopata kibali na ridhaa ya kuongoza dola kupitia njia ovu za vurugu, vitisho na uongo badala yake vyama vinavyoongoza dola ni vile vilivyokuwa karibu na wananchi kutokana na uhodari wa kutekeleza kwa vitendo matakwa ya wananchi.

Dk. Mabodi, alisema CCM itaendelea kuweka vipaumbele vya kuisimamia serikali itekeleze kwa vitendo sera za maendeleo kwa wananchi, huku wapinzani wakiendelea kujinadi na kupiga porojo zisizokuwa na tija kwa wananchi.

"Chama Cha Mapinduzi hakitishwi na hakiogopi taasisi yoyote ya kisiasa wala kundi la watu, kwa kuwa ni chama imara na chenye historia kubwa barani Afrika na duniani kote, hivyo hao walioanza kujitokeza kuleta uchochezi tunawaonya waache kuchafua nchi vinginevyo watajuta kwa uovu wao," alisema.

Kupitia kongamano hilo alivitaka vyombo vya ulinzi na usalama nchini kutekeleza wajibu wao kwa kudhibiti uvunjifu wa amani na utulivu, ulioanza kuvunjwa na baadhi ya wanasiasa wanaotamka kauli za uchochezi bila kuchukuliwa hatua za kisheria.

Alisema Chama Cha Mapinduzi kwa muda mrefu kimekuwa na uvumilivu wa kisiasa kwa kuheshimu sheria, miongozo na kanuni za uchaguzi na nchi, lakini hakitokuwa tayari kuona baadhi ya wanasiasa wanaibuka na kuhamasisha vurugu.

"Itafikia wakati uvumilivu wetu utakuwa na kikomo kama vyombo vya ulinzi na usalama mtashindwa kuwadhibiti hao wanaofanya vurugu wakiweka mguu wa kushoto na sisi tutaweka mguu wa kulia, nchi haitakalika na hatutaki kufikia huko bali tushindane kwa hoja na sera za kimaendeleo," alisema.

Aliwataka wanachama wa CCM walioshiriki katika kongamano hilo kuwa wanatakiwa kuwahamasisha wanachama wenzao na wananchi kwa ujumla kujitokeza kwa wingi kushiriki katika uandikishaji wa daftari la wapiga kura linalotarajiwa kuanza Januari 18, kisiwani Pemba. Alisema ushiriki wa wana-CCM katika daftari la wapigakura ni sehemu muhimu ya kuandaa mazingira ya ushindi wa CCM kwa kuwa ndio chimbuko la kupatikana wapiga kura watakaofanikisha ushindi wa CCM uchaguzi mkuu ujao.

Dk. Mabodi, aliwataka wabunge, wawakilishi na madiwani kufanya mikutano ya hadhara katika maeneo yao na kueleza kwa kina namna walivyotekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2015/2020. Akizungumzia umuhimu wa maskani, Dk. Mabodi, alisema maskani ni sehemu ya kueneza itikadi na kupanga mapinduzi ya kiuchumi yenye kuleta maendeleo endelevu.

Alisema viongozi namba moja ndani ya Chama Cha Mapinduzi ni mabalozi wa mashina na maskani na kuwataka viongozi washuke katika ngazi hizo kufahamu mahitaji yao na kupokea ushauri wa kujenga chama.

Naye Katibu wa Maskani ya Kachorora, Samia Leonard Shirima, alisema lengo la kufanya kongamano hilo ni kutoa elimu ya masuala mbalimbali yanayotekelezwa na CCM pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Maskani hiyo inasherehekea miaka 20 toka kuanzishwa kwake na inafanya shughuli mbalimbali za kijamii zikiwamo za usafi, kutembelea viongozi wastaafu na wazee wa Chama Cha Mapinduzi.

# Fedha za pamba zamtia karani matatani

**Na Tiganya Vincent,** NZEGA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, ameliagiza Jeshi la Polisi wilayani Nzega mkoani Tabora kumsaka na kumkamata karani wa Chama cha Msingi cha Ushirika cha Ikwabansabo kwa tuhuma za kutoroka na Sh. milioni 15.9 za wakulima wa pamba.

Alisema mtuhumiwa huyo, Raphael Malimbi, alikiuka taratibu za uchukuaji wa fedha kwa ajili ya malipo ya mauzo ya pamba ya wakulima, ambapo alichukua fedha taslimu badala ya kuwalipa kupitia akaunti za wakulima za benki au simu za mkononi.

Mwanri alitoa kauli hiyo juzi wakati wa mkutano wa majumuisho na watendaji wa vijiji, kata, maofisa ugani na watumishi wa Wilaya ya Nzega ikiwa ni siku ya mwisho ya ziara yake ya siku tatu kuhamasisha kilimo cha mazao mbalimbali ikiwamo pamba.

Alimtaka Kamanda wa Polisi Wilaya ya Nzega, SSP Constatine Mbogambi, kuhakikisha ndani ya saa 24 mtuhumiwa anakamatwa na kuanza taratibu za kumchukulia hatua za kisheria ikiwamo kumfikisha mahakamani.

Mwanri alisema hatua ya kwanza ya kufanikisha hilo ni vema Jeshi la Polisi likaanza kwanza kumkata Diwani wa Kata ya Milambo Itobo ambaye ndiye aliyedhamini mtuhumiwa na kudai kuwa atalipa fedha hizo za wakulima.

Alisema serikali haiwezi kukubali vitendo vya kuwadhulumu wakulima fedha zao vikajirudia kwani ndivyo vilivyosababisha wakachukia ushirika katika miaka ya nyuma.

Mwanri aliwaonya viongozi wengine ambayo wamechaguliwa kusimamia vyama vya ushirika vya msingi (AMCOS) kutodiriki kugeuza ushirika ni sehemu ya kujipatia fedha kinyume cha sheria.

Alisema kama kuna kiongozi amejiingiza katika uongozi wa AMCOS ili kupata utajiri amekosea njia ni kuondoka mapema kabla ya hatua mbalimbali dhidi yake hazijachukuliwa.

Katika hatua nyingine, Mwamri aliwaonya maofisa ushirika wa halmashauri zote mkoani humo kuhakikisha wanajiridhisha uhalali wa malipo kabla ya kuyapitisha.

Alisema ikibainika kuwa ofisa ushirika yeyote alishiriki katika malipo machafu atachukuliwa hatua ikiwamo kufukuzwa kazi.

Aidha, Mwanri alisema kama kuna wakulima wa pamba ambao wanadai ni vema maofisa ushirika hao wakaorodhesha majina yao na kuyapeleka kwa wakuu wa wilaya kwa ajili ya kufuatilia malipo.



Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Mateo (kushoto), akishiriki mazoezi ya utayari na askari mbalimbali wa jeshi hilo, jana, kwa ajili ya kukabiliana na matukio ya uhalifu wakati wa sikukuu za mwisho wa mwaka. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# TPA yakamilisha ujenzi wa meli ya MV Mbeya II

**Na Elizabeth Zaya,** KYELA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), imekamilisha ujenzi wa meli mpya ya kisasa ya Mv Mbeya II inayotarajia kuanza kufanya shughuli zake Januari 2020.

Meli hiyo ilianza majaribio juzi na itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 200 na mizigo tani 200 kwa wakati mmoja.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Bandari ya Kiwira, wilayani Kyela mkoani Mbeya, Meneja wa Bandari za Ziwa Nyasa, Abedi Gallus, alisema meli hiyo ni mwarobaini wa changamoto ya usafiri katika Kanda ya Ziwa hilo.

"Meli hii itakuwa ni mwarobaini wa changamoto ya usafiri katika Kanda ya Ziwa Nyasa kwa sababu itakuwa inapakia abiria na mizigo mikubwa na midogo, mtu akiwa na tani moja, mbili au tano tunampakilia tofauti na meli za mizigo pekee ambazo zinapakia mizigo mikubwa kidogo, "alisema Gallus.

Alisema meli hiyo imetengenezwa na kampuni ya kizalendo ya Songoro Marine ya Mwanza na imegharimu Sh. bilioni 9.1 ambayo ni mapato ya ndani ya TPA.

"Ujenzi wa meli hii ulianza Julai mwaka 2017 na tunatarajia Januari mwakani uanze kufanya safari zake ziwani, leo (juzi) imeanza majaribio," alisema Gallus.

"Ni meli yenye usalama na ina mwendo wenye kasi na haijawahi kutokea meli kama hii katika Ziwa Nyasa iwe kwa upande wa Msumbuji, Tanzania au Malawi."

"Meli hii haichagui miundombinu, inafunga nanga popote ilmradi pawe na kina, lakini TPA ili kurahisisha upakiaji na upakuaji lazima tuboreshe miundombinu yetu na tumedhamiria hilo katika bandari zetu zote."

"Serikali imeweka mradi huu si kwa bahati mbaya bali kwa malengo maalum na kubwa ni kuboresha shughuli za usafirishaji. Kabla ya hapo hakukuwapo na meli kubwa katika ziwa hili na hivyo kusababisha changamoto ya usafiri kwa wananchi wanaolizunguka ziwa hili."

Mbali na meli hiyo, Gallus alisema tayari wana meli nyingine mbili za mizigo za Mv Ruvuma na Mv Njombe ambazo zote zimejengwa katika kipindi cha serikali ya awamu ya tano.

"Meli hizi mbili za mizigo ujenzi wake ulianza Januari 2015 na kumalizika Julai mwaka 2017 na kila moja iligharimu Sh. bilioni 5.5 ambazo zimetokana na mapato ya ndani ya TPA."

# Cuhas yajiwekea malengo miaka 50

**Na Anthony Gervas**, MWANZA

CHUO Kikuu Katoliki cha Sayansi ya Tiba za Afya ya Binadamu Bugando (Cuhas), kimeweka malengo ya miaka 50 ijayo kuanza upanuzi wa ujenzi wa taasisi yake katika maeneo yaliyopo Kahama – Buswelu na Kabuholo Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na Makamu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Paschalis Rugarabamu, katika sherehe za kufunga mwaka za wafanyakazi wake wanachuo zilizoshirikisha wafanyakazi wa Hospitali ya Kanda ya Ziwa-Bugando, zilizofanyika eneo la Buswelu Wilaya ya Ilemela jijini hapa.

"Chuo chetu tumeweka malengo ya miaka 50 ijayo kuanza upanuzi wa ujenzi wa taasisi yake, ili kiweze kujitegemea na kuondoka ndani ya eneo la Hospitali ya Kanda ya Ziwa Bugando kwa faida ya vizazi vijavyo," alisema Prof. Rugarabamu.

Alisema chuo hicho kimetenga kila mwaka siku ya Desemba 20 kufanya sherehe na kutembelea maeneo yake ya chuo kinayoyamiliki yaliyopo Kabuholo na Kahama-Buswelu jijini hapa, lengo na madhumuni muhimu ya kufanya sherehe hizo ni kuwawezesha wafanyakazi wake kutafakari walichokifanya katika mwaka mzima, ikiwamo kufanya michezo na burudani.

Prof. Rugarabamu alisema malengo mengine ni kupanda miti kwenye maeneo hayo kwa ajili ya kutunza mazingira, wafanyakazi kufahamiana zaidi na wafanyakazi wa hospitali ya Kanda ya Ziwa-Bugando kwa njia tofauti kazini, kula na kunywa pamoja kutokana na taasisi hizo kufanyakazi kwa ushirikiano wa pamoja ambao unaitwa Cuhas Bugando Day.

Katika sherehe hizo chuo hicho kilipanda miti takribani 4,000 lengo ni kutunza mazingira na kufikisha jumla ya miti 6,000 katika eneo hilo lenye ukubwa wa ekari 200, ambalo uhitaji wake ni kupanda miti 20,000, hivyo chuo hicho kina maono ya mbele zaidi kukipanua hapo baadaye.

Aidha, wafanyakazi wa chuo hicho walifanya harambee ya kuchangia Sh. 50,000 kila mmoja kwa ajili ya kila mtu kutunza miti kwa mwaka mzima kuumwagilia maji, ambapo jumla ya Sh. milioni moja zilipatikana.

## New Zealand yasitisha kuwatafuta waliopotea

**WILLUNGTON, New Zealand**

POLISI nchini New Zealand imesema inasitisha harakati za kutafuta miili ya watu wawili ambao bado hawajulikani baada ya kupotea katika tukio la mlipuko wa volcano mapema mwezi huu.

Mkuu wa Polisi, Andy McGregor, alisema kwamba familia za watu hao wawili zimefahamishwa kuhusiana na uamuzi huo wa kusitisha shughuli hizo.

"Polisi bado wanasalia tayari kufanya kazi hiyo endapo taarifa yoyote itaibuka kuhusu watu hao ambao hawajulikani walipo," alisema McGregor.

Watu hao ambao wanakisiwa kwamba wamefariki dunia ni mtalii wa Australia aliyekuwa na umri wa miaka 17 Winona Langford na Hayden Marshall-Inman ambaye ni raia wa New Zealand aliyekuwa mwelekezi wa watalii.

Miili yao inadhaniwa kusombwa na maji na kupelekwa baharini katika kisiwa hicho cha volcano ambacho hakikaliwi na watu.

Polisi hapo Jumatatu ilisema mtu mmoja aliyejeruhiwa katika mlipuko huo amefariki katika hospitali moja ya mjini Auckland na kusababisha idadi ya waliofariki dunia kufikia watu 17.

**DW**

## UN yapinga hukumu kesi mauaji Khashoggi

**NEW YORK, Marekani**

MPELELEZI wa Umoja wa Mataifa (UN), Agnes Callamard, amesema hukumu ya kifo kwa watu watano nchini Saudi Arabia waliohusika na mauaji ya mwandishi wa habari wa Kisaudia, Jamal Khashoggi, imesababisha hasira ulimwenguni.

Callamard alisema hukumu hiyo ni kama kejeli kwa sababu wahusika halisi wa tukio hilo bado wapo huru.

Mchunguzi huyo maalum aliyechunguza kifo cha Khashoggi, alisema atahakikisha kuwa hakuna mtu atakayeepuka kuwajibishwa, bila kujali wadhifa au nguvu alizonazo.

Khashoggi, mwandishi wa habari aliyekuwa wakati mmoja karibu na familia ya kifalme ya Saudia, aliuawa na viungo vyake kukatwakatwa ndani ya ubalozi wa nchi yake mjini Istanbul, Uturuki, mwaka jana.

Siku ya Jumatatu, mahakama mjini Riyadh iliwahukumu watu watano kwa mauaji ya mwandishi huyo. Callamard alipozungumza na shirika la habari la Ujerumani (DPA), aliyataja maamuzi katika kesi hiyo kuwa ni kejeli, na kwamba anataka haki itendeke.

**DW**

# Boeing yamtumbua mkurugenzi wake

**WASHINGTON, Marekani**

KAMPUNI ya kutengeneza ndege aina ya Boeing, imemfuta kazi Mkurugenzi Mkuu Mtendaji wake, Dennis Muilenburg, katika hatua ya kurejesha imani kwa wateja baada ya ajali mbili mbaya zilizohusisha ndege yake ya 737 Max.

Zaidi ya watu 340 walikufa katika mkasa uliochochea shutuma kwamba Boeing iliweka mbele faida zaidi ya usalama. Lakini uamuzi wa Boeing kumwondoa Muilenberg na nafasi huyo kupatiwa mjumbe wa zamani wa bodi yake, kunaacha maswali mengi kuhusu wajibu wa kuleta mabadiliko.

Boeing ilimtaja David Calhoun, kushika nafasi hiyo na rais, kabla ya hapo alikuwa mwenyekiti wa bodi ya kampuni hiyo tangu 2009.

"Kujiuzulu kwa Muilenburg ikiwa ni hatua nzuri, ni wazi kwamba kampuni ya Boeing inahitaji kufanya mabadiliko ya utawala wake wa kampuni," alisema Paul Njoroge, ambaye alimpoteza mke wake, watoto watatu na mama mkwe wake kwenye ajali ya ndege ya Ethiopian Airlines chapa 302 iliyoanguka Machi.

"Calhoun si mtu sahihi kwa kazi," aliongeza.

Zipporah Kuria, ambaye baba yake aliuawa katika ajali ya ndege ya Ethiopian Airlines, alisema kuwa Muilenburg angepaswa kuwa ameondolewa mamlakani zamani lakini uwajibikaji wa ajali unawahusu wengi.

Boeing imekuwa ikikabiliwa na shinikizo la uchunguzi mkali dhidi ya ndege za 737 Max kufuatia ajali zake zilizotokea katika kipindi cha miezi mitano, ya kwanza ikiwa ni ya Indonesia na baadaye ya Ethiopia.

Safari za ndege za 737 zimepigwa marufuku kusafiri kote duniani tangu Machi.

Huku kampuni hiyo ikiwa na matumaini ya kurejesha angani ndege zake ambazo ndizo zinazouzwa zaidi duniani kufikia mwishoni mwa mwaka huu, wakaguzi wa viwango vya ndege nchini Marekani wamesema wazi kuwa haitapata kibali cha kurejea angani haraka.

Wiki iliyopita Boeing ilisema kuwa itasitisha uzalishaji wa ndege zake.

Bodi ya Boeing ilisema mabadiliko ya uongozi wake ni muhimu ili kurejesha imani katika kampuni wakati inapojaribu kusafisha uhusiano wake na wasimamizi wa viwango vya safari za anga na wadau wote. ***BBC***




Polisi kutoka kikosi maalumu cha kukabiliana na uhalifu wakiwa tayari kulinda usalama, wakati wananchi wa Singapore wakijiandaa jana kusherehekea sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya 2020. **PICHA: ST**

# Mbwa kutoka Marekani marufuku Jordan, Misri

**NEW YORK, Marekani**

MAREKANI imekataa kupeleka mbwa wake wa kufichua vilipuzi katika mataifa ya Jordan na Misri kufuatia vifo vya baadhi ya wanyama hao kutokana na uzembe.

Taarifa kutoka wizara ya masuala ya kigeni nchini humo, imesema kifo chochote cha wanyama hao kinaleta uzuni kubwa.

Mnamo mwezi Septemba, ripoti ya Marekani ilibaini visa vya uzembe katika zaidi ya mbwa 100 waliopelekwa Jordan na Misri na mataifa mengine manane katika miaka ya hivi karibuni.

Mbwa hao wa Marekani walio na mafunzo walipelekwa katika mataifa hayo ikiwa ni mpango wa vita dhidi ya ugaidi.

Jordan na Misri kufikia sasa hazijatoa tamko lolote.

Wizara hiyo ilitoa taarifa juzi kwamba hatua hiyo inalenga kuzuia maelezo zaidi.

"Mbwa hao wana jukumu muhimu katika vita dhidi ya ugaidi katika juhudi zetu ughaibuni kuokoa maisha ya raia wa Marekani," maofisa hao walisema.

Maofisa hao hata hivyo walisema kwamba mbwa waliopelekwa nchini Jordan na Misri watasalia katika mataifa hayo kwa sasa.

Ripoti hiyo kutoka ofisi ya inspekta jenerali ilisema kwamba mbwa mmoja alifariki Jordan 2017 kutokana na joto kali.

Mbwa wengine wawili walirudishwa nchini Marekani wakiwa katika hali mbaya, ilisema taarifa.

Maofisa wa Marekani walisema kwamba waliamua kumuua mbwa mmoja kabla ya kumsaidia aliyesalia kuimarisha afya yake kwa kuwa alikuwa na uzani mdogo.

Mbwa wote watatu walikuwa ni wale wa Belgian Malinois.

Jordan ndio imekuwa ikichukua mbwa wengi kutoka Marekani, huku 100 wakitumwa katika falme za mashariki ya kati. ***BBC***

# Chongolo aagiza kuondoa udumavu kwa watoto

**Na Khadija Kalili**

MKUU wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo, amewataka viongozi wa lishe kutoa elimu kwa wazazi kuhusu udumavu ili kunusuru afya za watoto kuanzia umri sifuri hadi miaka mitano, ambao ndiyo nguvu kazi ya kizazi kijacho.

Chongolo alisema hayo wakati akifungua mkutano wa tathmini ya mpango wa awali wa bajeti ya lishe Kinondoni kwa mwaka 2020/21 katika mkutano uliofanyika Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

Aliwaambia wadau wa lishe kiasi cha fedha kilichotengwa 2019/20 kwa kuzingatia Sh. 1,000 kwa kila mtoto chini ya miaka ni Sh. 149, 700,383.

"Jamii yetu imekuwa haiwatendei haki ukuaji wa akili za vijana kuwa na uwezo na mapokeo ya kile tunachokitarajia kama hawatojengwa kwa kupatiwa lishe zenye matokeo chanya kwa makuzi ya ubongo wao itakuwa kazi bure," alisema Chongolo.

"Tujenge mazingira ya kuwa wilaya ambayo haina watoto wenye udumavu wa afya kunakosababishwa na ukosefu wa lishe bora, pia nasisitiza wataalamu wa lishe umuhimu wa utoaji wa elimu ya lishe bora kuanzia kwa wajawazito."

Ofisa Lishe, Martha Kusaga, alisema wamejitahidi kutoa elimu kwa wafanyabiashara wa vyakula shuleni umuhimu wa kuzingatia vyakula wanavyouza kwa watoto na kuwataka vizingatie kuwa virutubisho vyenye faida kwa mlaji na siyo bora kuuza.

Alisema kati ya mafanikio yaliyopatikana hadi sasa ni kuwapo kwa vituo 74 vinavyotoa elimu ya lishe kwa wajawazito na wanaonyonyesha huku kukiwa na watoa huduma 116 kutoka katika kata 20 tayari wamejengewa uwezo wa kutoa elimu ya lishe kwa makundi maalumu.

Pia alisema ili kuweza kutokomeza udumavu inapaswa kuimarisha matumizi sahihi ya madini na vitamini muhimu zinazokidhi mahitaji ya kifiziolojia na kuzuia magonjwa yanayotokana na upungufu wa viini lishe.

"Watoto 135,784 wamefikiwa sawa na asilimia 99.8 kwa utoaji wa vitamin A na dawa za minyoo (CHNM)," alisema.

# CUF yaibuka na operesheni 2020

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimesema kitazindua operesheni mpya kiliyoipa jina la '2020 Mwaka wa Demokrasia na Maridhiano ya Kisiasa'.

Taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Mkurugenzi wa Habari wa chama hicho, Abdul Kambaya, ilieleza kuwa, katika kuhakikisha hilo linatimia, viongozi wa kitaifa wa chama hicho kuanzia mwezi ujao, watakuwa na ziara katika mikoa mbalimbali nchini.

"Operesheni hii itatambulishwa nchi nzima kwa mikutano ya ndani ikiwa na lengo la kuonyesha umuhimu wa uwapo wa demokrasia na maridhiano kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2020," Kambaya alieleza katika taarifa yake hiyo.

"CUF inawatakia Wakristo wote nchini sikukuu njema ya Krismasi na kheri ya Mwaka Mpya wa 2020. CUF inawakumbusha viongozi wote wa vyama na serikali kutumia mafundisho yanayopatikana kwenye kumbukizi ya kuzaliwa kwa Kristo kama mwanzo wa kurejesha upendo na furaha miongoni mwa jamii ya kitanzania bila kujali itikadi za kisiasa, kabila na dini zetu.

"CUF pia inawatakia Watanzania wote kheri ya Mwaka Mpya na kuwataka kujipanga kikamilifu katika kutekeleza majukumu yetu ya ujenzi wa taifa letu na familia zetu."

**KATIBA MPYA**

Kambaya pia alisema CUF inaona ipo haja kwa hali ya sasa kuendeleza hoja ya kumalizia mchakato wa upatikanaji wa Katiba Mpya ambayo kwa kiasi kikubwa imeshakaribia kupatikana kwa kuwa maoni ya wananchi yameshakusanywa na Rasimu ya Kwanza ya Katiba Mpya imeshachapwa.

"Uwapo wa demokrasia na maridhiano ya kisiasa ni muhimu sana ili kufikia upatikanaji wa Katiba Mpya ambapo ndani yake itapatikana tume huru ya uchaguzi.

"Demokrasia na maridhiano ya kisiasa ni nyezo muhimu si tu katika kufikia maendeleo ya kiuchumi na kisiasa, bali pia kuleta upendo, umoja na kustawisha amani miongoni mwa jamii," alisema.



Baadhi ya wananchi wakinunua mananasi kama walivyokutwa eneo la soko kuu la Majengo jijini Dodoma jana. **PICHA NA IBRAHIM JOSEPH**

# Wapewa wiki 2 kurudisha mil. 15/-

**Na Gurian Adolf, MLELE**

MKUU wa Wilaya ya Mlele mkoani Katavi, Rachel Kasanda, ametoa siku 14 kwa watumishi watano wa Halmashauri ya Mlele wanaotuhumiwa kuiba vifaa vya ujenzi wa hospitali ya wilaya hiyo vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 15 kulipa fedha hizo.

Alitoa amri hiyo jana katika kikao alichokaa na watumishi wa halmashauri hiyo.

Alisema kuwa hivi karibuni kumejitokeza tabia kwa watumishi wasio waaminifu wakishirikiana na walinzi pamoja na vibarua walio kwenye ujenzi wa hospitali hiyo.

Alisema vifaa hivyo vilivyoibwa vilikuwa vimehifadhiwa kwenye stoo kwa ajili ya ujenzi wa hospitali unaoendelea katika mji wa Inyonga.

Alivitaja vifaa hivyo na idadi kwenye mabano kuwa ni feni (8), waya kwa ajili ya kusukia umeme (milimita 2.5), pamoja na milimita 1.5, jipsum powder, metal box, taa za umeme aina ya tube light, pvc, na saruji, vyote vikiwa na thamani ya Sh. 15,698 ,500.

Alisema watuhumiwa 11 wamebainika kuhusika na tukio hilo.

Watuhumiwa wamekamatwa na polisi baada ya kubainika kutokea katika mradi huo.

Mkuu huyo wa wilaya alisema tayari amewachukulia hatua watumishi wa Halmashauri ya Mlele wakiwamo watunza stoo ambao hawakufanya kazi yao kama ilivyostahili, huku wakiwa ni watumishi wa halmashauri hiyo.

Alisema watumishi hao walikiri wenyewe kuwa wapo tayari kulipa hasara iliyojitokeza katika ujenzi wa hospitali hiyo na amewapa wiki mbili walipe fedha hizo na kuwaagiza kwenda kuripoti katika vyombo vya sheria watalipa lini.

Aliwataja watumishi hao waliokubali kulipa hasara hiyo kuwa ni ofisa ununuzi, Essau Nele, Fidelisi Msongela, Mussa Uchele, Ombeni Aron na Obrey Kasembe.

Aliwataka kuhakikisha vifaa hivyo vinapatikana au fedha ili kukamilisha ujenzi wa hospitali hiyo, ambayo ujenzi wake umefikia asilimia 80 bila upungufu.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele, Alexius Kagunze, alisema wataendelea kuwachukulia hatua watumishi wote wanaoisababishia hasara serikali.

# Mbegu bora kilimo kuzalishwa nchini

**Na Mwandishi wetu, SONGWE**

SERIKALI imekusudia kuanzisha juhudi wezeshi kuwezesha mbegu bora za kilimo kuzalishwa nchini ili kuondokana na uagizaji wa mbegu nje ya nchi.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, aliyasema hayo juzi, baada ya kutembelea kampuni ya Namburi inayojihusisha na uzalishaji wa mbegu za vizazi za mahindi, mtama na mpunga iliyopo katika eneo la Vwawa wilayani Mbozi, wakati akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Songwe.

Alisema Tanzania ina uhitaji wa mbegu tani 186,000 za mazao mbalimbali, huku uzalishaji wa ndani ikiwamo uagizaji wa mbegu nje ya nchi ukiwa mdogo kwani haujafika hata tani 50,000.

Alibainisha kuwa Tanzania ina maeneo makubwa na bora kwa uzalishaji, hivyo ni lazima kuzalisha mbegu za kutosha nchini na kuachana na utegemezi wa mbegu kutoka nje.

Waziri Hasunga alitoa rai kwa wananchi kuhakikisha kuwa wananunua mbegu bora kwa ajili ya kukabiliana na msimu wa kilimo na kuachana na matumizi ya mazao yao ya misimu iliyopita waliyoyahifadhi kama mbegu.

Waziri Hasunga alikuwa akizungumza na wananchi wa kijiji cha Mbulu katika Kata ya Mahenje wilayani Mbozi baada ya kukagua skimu ya umwagiliaji ya Mbulu.

Alisema serikali imedhamiria kuimarisha skimu za umwagiliaji nchini ili kuondokana na kilimo cha kutegemea mvua.

Hasunga alisema kilimo cha kutegemea mvua ni hatari, kwa kuwa hakina uhakika wa upatikanaji wa chakula cha kutosha kutokana na changamoto mbalimbali zinazojitokeza za kukosekana kwa mvua kwa sababu ya mabadiliko ya tabia nchi.

Aliwaagiza maofisa ugani kuzuru katika maeneo ya wakulima, ili kutoa elimu sahihi za kilimo, matumizi sahihi ya viuatilifu pamoja na matumizi sahihi ya zana za kilimo.

Aibainisha kuwa programu ya kuendeleza kilimo awamu ya pili-ASDP II yenye jukumu la kuimarisha masoko na kuongeza thamani kuwa ni lazima wakulima watumia njia bora za kilimo ikiwa ni pamoja na kupata elimu bora na sahihi kwa wakulima.

Alisema katika programu hiyo moja ya mambo msingi ni matumizi bora ya maji na ardhi, hivyo sekta ya kilimo ni muhimili wa matumizi bora ya maji kupitia skimu za umwagiliaji.



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, akikagua ghala la kuhifadhi mbolea katika eneo la Vwawa wilayani Mbozi mkoani Songwe katika ziara ya kikazi. **PICHA:WK**

# Wailalamikia manispaa kukithiri taka

**Na Neema Hussein, KATAVI**

WAKAZI wa Kata ya Makanyagio Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi, wameulalamikia uongozi wa manispaa kwa kushindwa kupeleka gari la uzoaji taka kwa takribani miezi mitatu sasa na kusababisha kukithiri kwa uchafu katika eneo hilo.

Wakizungumza na Nipashe, wakazi hao walisema hali hiyo husababisha hata kuziba kwa mitaro ya maji wakati huu wa mvua kutokana na baadhi ya watu kutupa taka hizo kwenye mitaro hiyo.

"Gari la taka siku hizi halipiti kabisa...ni zaidi ya miezi mitatu sasa yaani taka zimekithiri," alisema mkazi mmoja na kuendelea:

"Kwa kweli wenye maeneo makubwa wanaamua kuchimba chini wanazifukia, wengine wanazimwaga kwenye mitaro na mitaro inaziba, mvua ikija maji hayapiti."

Agustino Chambala, Mwenyekiti wa Mtaa wa Mpadeko katika kata hiyo, alisema hali hiyo inatokana na kuwapo kwa gari moja tu manispaa nzima la kubeba taka.

Alisema kutokana na hali hiyo, wanauomba uongozi uwape kibali cha kukodisha gari binafsi kwa fedha zilizotolewa na wananchi Oktoba ili kunusuru tatizo hilo.

"Sisi baada ya kuona hali hii tulikaa kikao na viongozi wenzangu tukaamua kuomba kibali kwa viongozi wa juu ili tukodishe gari binafsi kuja kubeba hizi taka... kuna pesa ambayo ilibaki mwezi ambayo walichanga wananchi mara ya mwisho kwa ajili ya kuja kubebewa taka," alisema Chambala. Mkurugenzi wa Manispaa ya Mpanda, Maiko Zyungu, alipotafutwa na Nipashe kwa njia ya simu, alisema yuko nje ya mkoa na hana taarifa hizo.

Hata hivyo Zyumba aliahidi kulifanyia kazi suala hilo, huku akithibitusha kuwa gari lililopo halitoshi kukidhi idadi ya taka zinazozalishwa kwa siku.

"Mimi sipo ila nitawapigia waliopo waweze kulifanyia kazi maana gari tulilonalo halitoshi kukusanya taka manispaa yote kwa wakati mmoja kulingana na taka zinazozalishwa kwa siku ni kama tani 67," alisema Zyungu.

Alisema wana mpango wa kuongeza magari na kujenga dampo la kisasa kwa ajili ya kuhifadhi taka hizo.

# Wakulima 120 wafaidika malipo kupitia Tigopesa

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA zaidi ya 120 kutoka mikoa ya Simiyu na Shinyanga wamefaidika na huduma ya kupokea malipo yao kupitia Tigopesa kutoka kampuni ya simu ya mkononi ya Tigo.

Meneja wa Kampuni ya Tigo kwa upande wa mikoa ya Simiyu na Shinyanga, Phares Sadock, akizungumza juzi kuhusu huduma hiyo, alisema wakulima wamefaidika kwa kuwa ni njia salama ya kuwalipa wakulima.

Alisema wakulima waliofaidika na huduma hiyo ni kutoka Vyama vya Ushirika vya Zanzui, Kidabu, Gumali na Nuya na wakulima wa zao la pamba wamepokea malipo jumla ya Sh. milioni 189.

Sadock alisema kwa sasa wameanza na vyama vichache vya ushirika, lakini kwa msimu watajitahidi kufikia vyama vingi vya ushirika.

Kwa upande wake, Mratibu wa Malipo ya Mazao ya Wakulima kupitia Tigo pesa, Rushaka Abdul, alisema wameanza kutoa malipo kwa wakulima kwa baadhi ya vyama vya ushirika.

Abdul aliahidi watahakikisha wanawafikia wakulima zaidi kutoka vyama vya ushirika 384 kutoka vijiji 447.

Alisema baada ya kufanikisha malipo katika kwa vyama vya ushirika walioyoanza navyo mpaka sasa wamepokea mapendekezo ya malipo kwa vyama vya ushirika mbalimbali kwa ajili ya kuwasaidia kuwalipa.

Aliishukuru Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa kuwasaidia kuwapa ruhusa ya kuwalipa wakulima wenye madeni ya Sh. milioni 10 kwa njia ya Tigopesa.

Mmoja ya wakulima kutoka kata ya Zanzui, Philipo Daudi, alisema anaishukuru kampuni ya Tigo kwa kupata malipo yake.

Mhasibu wa Chama cha Ushirika cha Zanzui, Masanja Gambishi, aliishukuru Tigo kwa kufanikisha wakulima wa chama chao.

Aliiomba kampuni hiyo kuwasaidia pia wakulima katika ulipaji wa malipo yao wakati wa msimu mpya wa kilimo cha zao la choroko na alizeti utakapoanza.




# VIDAL

## HATAKI KUONDOKA BARCELONA

**BARCELONA, Hispania**

ARTURO Vidal amesisitiza yeye "ametulia na ana furaha" kuhusu majaliwa yake pale Barcelona licha ya kutokataa uwezekano wa kuhamia Inter Milan kwenye dirisha lijalo la usajili.

Oktoba mwaka huu, kiungo huyo alisema anajisikia furaha kuwa chaguo la pili kwa kocha Ernesto Valverde na angeweza kuangalia upande mwingine kama mambo hayatabadilika.

Vidal aliripotiwa kubwatuka kwenye mazoezi baada ya kuambiwa kwamba hatakuwapo kwenye kikosi cha kwanza katika mchezo wa El Clasico uliochezwa Desemba 18 mwaka huu, ingawa alijikuta akianza kwenye mechi yake ya nne ya LaLiga msimu huu dhidi ya Deportivo Alaves na kufunga bao.

Inter imedaiwa kwamba inataka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 kwenye dirisha dogo la Januari, ambaye alifurahia mafanikio chini ya kocha, Antonio Conte, pale Juventus, lakini hatafanya haraka kufanya uamuzi wake.

Akizungumza baada ya kuondoka kwenda nyumbani kwake Chile kwa mapumziko mafupi ya sikuuu ya Krismasi, Vidal aliwaambia waandishi wa habari kuhusu uwezekano wa dili hilo la Inter.

"Wawakilishi wangu ndio wataangalia nini kitanifaa, lakini nimetulia na nina furaha Barcelona. Wakati nikaporudi tutaona. Kwa sasa nataka kuwa na familia yangu, na baada ya hapo kurudi na kufanya uamuzi.

"Mimi sio ndiye ninayefanya uamuzi wa kucheza au la - hilo ni suala la kocha. Lakini watu wanaona hivyo, hivyo hilo linanifanya mimi nitulie, na nitaendelea kuangalia nafasi zinazokuja kwangu na kuendelea kufunga kama nilivyofanya.

"Natumaini kubeba kombe mwishoni mwa msimu."

Vidal ameanza katika mechi sita tu kwenye mashindano yote kwa Barca msimu huu 2019-20, huku Sergio Busquets, Frenkie de Jong, Arthur na sasa Ivan Rakitic wamekuwa wakitumika zaidi katika nafasi ya kiungo wa kati.

Majaliwa ya Rakitic pia yapo shakani, lakini Barca itamuuza kiungo huyo kama tu watapata ofa nzuri.

## GUARDIOLA HAFIKIRII MKATABA MPYA CITY

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amesisitiza ni mapema mno kwake kufikiria kuhusu kusaini mkataba mpya na Manchester City.

Mkataba wa sasa wa Guardiola unamalizika mwishoni mwa msimu wa 2020-21, ingawa kuna ripoti ambayo Guardiola amekanusha - ikidai kuna kipengele kinachomruhusu kuondoka mwishoni mwa msimu huu.

City imetwaa taji la Ligi Kuu England mara mbili ndani ya msimu yake mitatu na klabu hiyo, lakini sasa anapitwa pointi 11 na vinara Liverpool, wakiwa nafasi ya tatu katika msimamo.

Guardiola amedai kwamba ana furaha klabuni hapo, ingawa amezungumzia kuhusu majaliwa mapya ni mapema mno.

"Tayari nimekuwa hapa kwa misimu minne na mwishoni mwa mwaka itakuwa mitano kwa sababu nataka kuwa hapa hadi wakati huo," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Hivyo bado muda mrefu. Angalia kinachotokea, klabu zinafukuza makocha kila wiki. Nimejibu swali hilo mara nyingi tu. Najisikia vizuri kuwa hapa.

"Kusaini mkataba mpya nahitaji kuona namna gani mambo yatakuwa na kama nastahili."



## ANCELOTTI AMWITA IBRAHIMOVIC EVERTON

**LIVERPOOL, England**

CARLO Ancelotti ameweka wazi nia yake ya kujaribu kumsajili Zlatan Ibrahimovic katika kikosi chake cha Everton, ingawa amesisitiza bado hajafanya mazungumzo na nyota huyo raia wa Sweden.

Ibrahimovic ni mchezaji huru kwa sasa baada ya kuondoka katika Ligi Kuu Marekani (MLS), katika klabu ya LA Galaxy, mapema mwaka huu na nyota huyo mwenye umri wa miaka 38 amekuwa akihusishwa zaidi na mpango wa kurudi kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, huku Milan na klabu ya zamani ya Ancelotti Napoli zimeripotiwa kumwania.

Hata hivyo, huku Ancelotti - ambaye aliwahi kumnoa Ibrahimovic pale Paris Saint-Germain - akiwa amejiunga Everton, mshambuliaji huyo ametajwa kwamba anaweza kutua pale Toffees.



Ancelotti amesema mlango unaweza kuwa wazi kama Ibrahimovic ataamua kwenda pale Goodison Park.

"Zlatan Ibrahimovic ni rafiki yangu mzuri, alikuwa mchezaji wangu," alisema Ancelotti akiwaambia waandishi wa habari Jumatatu.

"Bahati nzuri nimewafundisha wachezaji wengi wazuri, wanaovutia. Ibrahimovic amemaliza muda wake kule Marekani, lakini kwa ukweli kabisa sijui mawazo yake.

"Kwa uhakika kabisa sijui. Natakiwa kumuita. Kama anataka kuja hapa, kufurahia anaweza kuja."

## HABARI MICHEZO




# MATIC
## AMTABIRIA MAKUBWA RASHFORD

**MANCHESTER, England**

MARCUS Rashford anaweza "kufanya vizuri zaidi na zaidi" na bado ana nafasi ya kujifunza na kuwa mchezaji aliyepevuka, mchezaji mwenzake wa Manchester United, Nemanja Matic, amesema.

Rashford amefunga mabao 14 katika mashindano yote msimu huu wa 2019-20, kitu ambacho ni bora zaidi kwake kwa msimu mzima tangu aanze kucheza timu ya wakubwa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 ameonyesha kitu fulani na kuwa kiongozi chini ya kocha, Ole Gunnar Solskjaer, chenye vijana wengi na amekuwa na kiwango kisichochuja kwa kipindi cha miezi michache pale Old Trafford.

Lakini Matic, anafikiri Rashford anaweza kuwa mchezaji bora zaidi, ilimradi tu akipewa muda wa kujiimarisha.

"Marcus ana nafasi kubwa ya kuwa mchezaji mkubwa zaidi," amesema Matic akiiambia Omnisport.

"Ni mtu mzuri nje ya dimba, lakini nafikiri hajatumia ubora wake wote bado. Anahitaji kupevuka zaidi na naweza kusema kila mwaka kila mwezi anakuwa bora na bora.

"Nafikiri kwa siku za usoni, kwa kipindi cha miaka miwili au mitatu, ataonyesha nini anachoweza kukifanya na atafanikiwa kwa sababu anaweza kufanya zaidi na zaidi kwa maoni yangu.

"Bado ni kijana. Tunamtarajia kucheza mechi 40 katika kiwango kile kile kwa sababu ni kijana, bado anaendelea kujifunza, bado anaendelea kuimarisha mwili wake na akili yake.

"Anaweza kuwa mmoja wa washambuliaji bora duniani, kwa uhakika kabisa."

# Perez apata mpinzani urais Madrid

**MADRID, Hispania**

RAIS wa zamani wa Real Madrid, Vicente Boluda, ametangaza atagombea nafasi ya urais dhidi ya Florentino Perez katika uchaguzi ujao.

Mfanyabiashara huyo kutoka Valencia, mwanachama wa klabu hiyo tangu mwaka 1998 na kwa muda mfupi kuwa rais mwaka 2009, amepanga kugombea dhidi ya Perez katika uchaguzi utakaofanyika mwaka 2021.

Perez, ambaye alichukua nafasi hiyo kutoka kwa Boluda mwaka 2009 baada ya kujiuzulu kwa Ramon Calderon.

"Real Madrid ina rais ambaye kwa uhakika anafanya vizuri," alisema Boluda katika mkutano wa mkutano mjini Valencia Jumatatu, kwa mujibu wa Cadena SER.

"Ni kitu kingine mwaka ujao, kutakuwa na uchaguzi mwingine na nataka kuwa pale ili nichaguliwe, na kwa hilo kutakuwa na wagombea wawili na mmoja anatakiwa kuwa tofauti na mwingine.

"Nitagombea nafasi ya urais, sina namna nyingine lazima nigombee."

Boluda, ambaye amezungumzia kwamba, Madrid inahitaji usajili mkubwa wa wachezaji watatu na akaongeza rais wa klabu anaweza kwenda nchi yoyote na akapokelewa kama rais wa serikali."



# Mbappe: Sitachukua nafasi ya Neymar PSG

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe ameamwambia Neymar kamwe hatajaribu kumpiku yeye na kuwa mchezaji mkubwa zaidi wa Paris Saint-Germain.

Huku Neymar akiwa anakabiliwa na majeruhi ya mara kwa mara kwa kipindi chake pale Paris, Mbappe amekuwa akijiimarisha yeye mwenyewe kama mchezaji muhimu wa PSG katika safu ya ushambuliaji tangu alipohamia hapo akitokea Monaco mwaka 2017.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 amefunga mabao 39 katika mashindano yote msimu uliopita na tayari amefikisha magoli 18 kwenye msimu huu.

Hata hivyo, Mbappe amesisitiza hatarajii kumpiku Neymar, ambaye amekuwa kwenye kiwango kizuri chini ya kocha Thomas Tuchel msimu huu.

"Wakati nilipofika Paris, kulikuwa hakuna mjadala. Alikuwa yeye (Neymar), nyota, ambaye nilikuja kumsaidia kidogo," amesema Mbappe akiiambia France Football.

"Anapata majeruhi, (Brazil ikitolewa mapema) kwenye fainali za Kombe la Dunia na nikashinda. Na pale habari zikaanza kuhusu upinzani wetu, kuhusu uamuzi wangu wa kuchukua nafasi hapa.

"Nilishtushwa kusikia hivyo. Wakati niliporudi Agosti mwaka jana, kitu cha kwanza nilichofanya ni kwenda na kumshika Neymar na nikamwambia: "Usihofu, sitakuwa natembea kwenye kitanda chako.

"Nakuhakikishia kwamba sitachukua nafasi yako, endelea nayo. Mara zote nipo hapa kwa ajili ya kukusaidia."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GUARDIOLA AJITOSA KUMWANIA GUAITA

●●●Pia kocha huyo apanga kufanya mabadiliko makubwa kwenye kikosi...

**MANCHESTER, England**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu England, Manchester City, wanatajwa kuwa wameanza mchakato wa kuwania saini ya golikipa wa Crystal Palace, Vicente Guaita, kama Claudio Bravo, ataamua kuondoka klabuni hapo katika kipindi cha majira ya joto mwakani.

Guaita amekuwa mmoja wa wachezaji wa Crystal Palace ambao wameonyesha kiwango cha juu msimu huu na wakiwa na safu bora ya ulinzi nyuma ya Liverpool, Leicester na Sheffield United.

Kwa mujibu wa gazeti la AS la Hispania, limeandika kuwa macho ya Manchester City na Kocha Pep Guardiola, yako kwa mlinda mlango huyo.

Katika upande mwingine, gazeti hilo lilisema kuwa Guardiola atalazimika kusaka golikipa chaguo la pili mpya hapo mwakani kutokana na hatima ya Bravo bado haijajulikana, licha ya kuwa tayari kumpa mkataba mrefu.

City imefungwa mabao 20 katika mechi za Ligi Kuu England msimu huu, idadi sawa na magoli waliyofungwa Palace, lakini wakiwa kwenye wakati mgumu kuelekea kwenye mbio za kuwania taji hilo.

Mabingwa hao watetezi kwa sasa wako katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo, pointi moja nyuma ya Leicester wakati wanazidiwa pointi 11 na vinara Liverpool, ambao wamecheza mechi moja pungufu.

Wiki iliyopita, taarifa nyingine ziliandikwa kuwa Guardiola anataka kufanya mabadiliko makubwa katika klabu hiyo msimu ujao kwa malengo ya kuondoa tofauti iliyopo kati ya timu yake na Liverpool, na uamuzi huo unalenga kuirejesha City kwenye ushindani na hatimaye kufanya vema na kukaa katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa Ligi Kuu England.

Keshokutwa Ijumaa, City inatarajia kuwa ugenini kuwafuata Wolves, wakati Palace itaikaribisha West Ham.

Taarifa kutoka Hispania zinaeleza kuwa, City wanajipanga kumpa mkataba wa muda mrefu golikipa huyo

## KWA UFUPI

**BARCA KUMREJESHA NEYMAR**

BARCELONA wameanza mchakato wa kuhakikisha mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Brazil na Paris St-Germain, Neymar anarejea katika klabu yao. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

**UNITED, LEIPZIG VITANI**

MKURUGENZI wa Soka wa RB Leipzig, Oliver Mintzlaff, amebainisha kuwa klabu yake itapambana na Manchester United katika vita ya kuwania saini ya straika wa Timu ya Taifa ya Norway, Erling Haaland, ambaye anaichezea Red Bull Salzburg. ***(Mail)***

**ISCO ANUKIA CHELSEA**

CHELSEA wamepewa ofa ya kumsajili Isco (27), kwa dau la pauni milioni 44 ili Real Madrid iweze kuendelea na mchakato wake wa kunasa saini ya kiungo wa Tottenham, Christian Eriksen, ambaye ana umri wa miaka 27. ***(Mirror)***

**KOLASINAC AGOMBEWA ITALIA**

BEKI wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Bosnia-Herzegovina, Sead Kolasinac (26), anawindwa na Napoli and Roma. ***(Sky Sports)***

**POGBA KUBAKIA UNITED**

MABOSI wa Real Madrid wamemweleza wakala wa Paul Pogba, Mino Raiola, kuwa hawatamsajili kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa katika kipindi cha dirisha dogo la Januari. ***(Mail)***

**DIOP KUIKAMUA SPURS**

TOTTENHAM inatakiwa kulipa kiasi cha pauni milioni 50 ili kunasa saini ya beki wa kati wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Issa Diop (22), ambaye anaichezea klabu ya West Ham. ***(Express)***

**SOUMARE AGEUKA LULU**

TOTTENHAM Spurs inajiandaa kuwania saini ya kiungo wa Lille, Boubakary Soumare. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 20 pia anawaniwa na Manchester United. ***(L'Equipe - via Football 365)***

**KESSIE AKARIBIA WOLVES**

AC Milan imesema kuwa thamani ya kiungo wake Franck Kessie (23), ni pauni milioni 26. Wolves inatajwa kumwania nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast katika dirisha dogo la Januari. ***(Calciomercato - in Italian)***

**LYON YAMWANIA LEMAR**

LYON imemtaja kiungo wa Atletico Madrid na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Thomas Lemar (24), kuwa mmoja wa wachezaji inaowahitaji katika dirisha dogo la usajili. ***(L'Equipe - in French)***

**CAVANI, ATLETICO SAFI**

ATLETICO Madrid imefikia makubaliano ya kumsajili straika wa Paris Saint Germain na Timu ya Taifa ya Uruguay, Edinson Cavani (32). ***(Star)***

**UNITED YAMFUATA MANDZUKIC**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amerudisha nguvu katika kuwania saini ya straika wa Juventus na Timu ya Taifa ya Croatia, Mario Mandzukic (33), kwa mkataba wa muda mfupi. ***(Express)***



HABARI MICHEZO

# MAANDALIZI RIADHA TAIFA NGORONGORO YAKAMILIKA

Na Mwandishi Wetu

MAANDALIZI ya mashindano ya Taifa ya riadha ambayo yanatarajiwa kufanyika Jumamosi na Jumapili kwenye Chuo cha Elimu ya Taifa Butimba, jijini Mwanza yamekamilika, imeelezwa.

Michuano hiyo ya mwaka huu itajulikana kama "Mashindano ya Riadha ya Taifa ya Ngorongoro 2019" yanatarajiwa kushirikisha wanariadha kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani.

Taarifa iliyotolewa na Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), imesema kuwa inatambua michango na uwezeshaji wa wadau mbalimbali katika sekta ya michezo hususan riadha, pia likitambua wajibu wa michezo katika kuchangia maendeleo ya Taifa ikiwamo kuitangaza nchi na vivutio vyake, limeamua kuyapa jina hilo kwa ajili ya kuheshimu ushirikiano unaofanywa na Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro (NCCA).

Taarifa hiyo iliongeza kuwa katika kalenda ya mwaka ya RT, inayoelekea ukingoni, inaonyesha kuwa NCCA imetoa mchango mkubwa katika kufanikisha Mashindano ya Nyika ya Taifa mwaka huu ambayo yalifanyika Moshi, mkoani Kilimanjaro, ushiriki wa Tanzania katika mashindano ya Nyika ya Dunia huko Aarhus nchini Denmark, mashindano ya wazi ya Taifa mwaka jana ambayo yalifanyika jijini Arusha na matukio mengine mbalimbali ya chama hicho.

"RT tunawashukuru na kuwaomba wazidi kuendeleza ushirikiano, pia tunawakaribisha wadau wengine wenye mapenzi mema na maendeleo ya Taifa la Tanzania hususan katika sekta ya michezo, tutawapa ushirikiano wa kutosha," ilisema taarifa hiyo.

Mkuu wa Idara ya Mawasiliano wa chama hicho, alisema kuwa viongozi wa mikoa wanatakiwa kuhakikisha wanariadha wao watakaoshiriki mashindano hayo wanawasili Mwanza keshokutwa Desemba 27 mwaka huu.

"Maelezo zaidi kuhusu michezo itakayochezwa, idadi ya washiriki kwa kila mkoa, tumetumwa kwa makatibu wa mikoa yote na tunaomba izingatiwe," iliongeza taarifa hiyo.

Mashindano yanatarajiwa kuwa sehemu ya kutoa wachezaji na maandalizi ya michuano ya Dunia ya umri chini ya miaka 20 itakayofanyika jijini Nairobi, Kenya na Michezo ya Olimpiki, pia RT itaongeza orodha ya wanariadha wake kwa kufahamu viwango vyao vipya na kuifanya Kamati ya Ufundi kufanya kazi yake kwa wepesi.

Wakati huo huo, katika utekelezaji wa matakwa ya Katiba, Kamisheni ya Wanariadha inatarajia kufanya uchaguzi mkuu Jumapili.

Nafasi zitakazogombewa katika uchaguzi huo ni pamoja na uenyekiti, ukatibu mkuu, wajumbe wawili wanaume na wajumbe wawili wanawake.



Mshambuliaji wa Azam FC, Donald Ngoma, (katikati), akijiandaa kuwatoka mabeki wa African Lyon, katika mechi ya Kombe la FA iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi. Azam ilishinda kwa penalti 4-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# M-Bet kumbadilisha shabiki wa Simba

Na Mwandishi Wetu

SIKUKUU ya Krismasi imekuwa nzuri kwa shabiki wa Simba na Manchester United, Fredrick Kimario, ambaye ameshinda Sh. milioni 124.1 baada ya kubashiriki kwa usahihi jumla ya mechi 12 katika za mchezo wa kubahatisha wa Perfect 12.

Kitita hicho cha fedha alishinda Kimario, mkazi wa Dodoma kinakamilisha kiasi cha Sh. bilioni 3 ambacho kimetolewa na Kampuni ya M-Bet Tanzania kwa washindi mbalimbali tangu kuanza kwa mwaka huu.

Meneja Masoko wa M-Bet, Allen Mushi, alisema kuwa kampuni yao inazidi kupata washindi na Kimario anaaga mwaka kwa kishindo kwa kutwaa zawadi hiyo akiwa ni mshindi wao wa 19.

"M-Bet inazidi kuchanja mbuga na kuinua vipato vya Watanzania, na inachangia maendeleo ya nchi chini ya Serikali ya Awamu ya Tano ya Rais Dk. John Magufuli. Nawaomba Watanzania kucheza ili kushinda zawadi za fedha na kubadili maisha yao," alisema Mushi.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa fedha zake, Kimario, alisema kuwa alianza "kubeti" muda mrefu kabla ya kupata ushindi huo mnono.

Kimario alisena kuwa amekuwa akishinda fedha kiasi kisichopungua Sh. 400,000 na ushindi huu umemfanya kuanza kufikiria mambo makubwa zaidi ya kibiashara na kuacha kazi yake ya sasa ya kuajiriwa.

"Sikukata tamaa na kuendelea kubeti, niliamini kuwa siku moja nitapata bahati ya kushinda, nashukuru Mungu kupata kiasi hiki cha fedha na nitakaa na ndugu zangu kupanga jinsi ya kuanzisha biashara zangu," alisema mshindi huyo.

# Azam FC yaifuata Coastal mapema

Na Mwandishi Wetu

LICHA ya kusonga mbele katika mashindano ya Kombe la FA, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddi Cheche, amesema kuwa kikosi chake hakikucheza vema katika mchezo huo dhidi ya African Lyon inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza.

Mabingwa hao watetezi wa Kombe la FA, walipata ushindi wa penalti 4-1, baada ya kutoka sare ya bao 1-1 katika dakika 90 za kawaida.

Cheche alisema kuwa baada ya kusonga mbele katika michuano hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara kwenye mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, sasa wanaelekeza nguvu zao katika Ligi Kuu.

**"Hatukucheza vizuri, ila kwa sababu tuna jua mashindano haya yanachezwa kwa mtindo wa mtoano, tulijiandaa kupata ushindi kwa njia zote, kufunga kwa faulo, krosi au matuta ambayo ya metusaidia," alisema Cheche.**

Azam FC inatarajia kushuka dimbani kesho kuwakabili wenyeji wao Coastal Union, katika mchezo wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga.

# IDUMU YAKARIBIA LIGI KUU ZANZIBAR

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

WAKATI Idumu FC ikiweka mguu mmoja ndani kuelekea Ligi Kuu Zanzibar, jumla ya mabao 181 yamefungwa katika michezo 78 ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, imeelezwa.

Ligi hiyo tayari imesimama na timu zinazoshiriki zimeanza kufanya usajili wa dirisha dogo ili kuimarisha vikosi vyao kwa ajili ya kumalizia mzunguko wa lala salama ambao unatarajiwa kuanza mapema mwakani.

Idumu FC yenye pointi 22 ndiyo vinara wa ligi hiyo wakifuatiwa na Black Sailor ambao wanalingana pointi, katika ligi hiyo inayoshiriki timu 13 wakati nafasi ya tatu inashikiliwa na Taifa Jang'ombe yenye pointi 21, huku Mchangani yenye alama sawa ikifuata na "Tano Bora" inakamilishwa na Uhamiji yenye pointi 20.

Katibu wa Kamati ya Mashindano ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Hussein Ahmada, amezikumbusha timu zinazoshiriki ligi hiyo kufuata kanuni na taratibu katika kufanya usajili kwenye kipindi cha dirisha dogo ambacho kinaendelea.

Aliongeza kuwa ligi hiyo ina ushindani kwa sababu timu zote zinahitaji kufanya vema ili ziweze kupanda daraja na kushiriki Ligi Kuu Zanzibar katika msimu ujao wa 2020/21.

Michezo
Jumatano Desemba 25, 2019
Nipashe



## Guardiola ajitosa kumwania Guaita

HABARI UK 30



Mshambuliaji wa Liverpool, Sadio Mane (kulia), akiwania mpira dhidi ya beki wa Flamengo, katika mechi ya fainali ya Klabu Bingwa ya Dunia ya Fifa iliyochezwa kwenye Uwanja wa Khalifa, Qatar Jumamosi iliyopita. Liverpool ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# MKWASA ALALAMIKA YANGA IKIKAMATWA

## ●●●Ni katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Mbeya City iliyomalizika kwa...

**Na Isaac Kijoti, MBEYA**

BAADA ya kushuhudia timu yake ikipata sare tasa dhidi ya Mbeya City katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine, Kaimu Kocha Mkuu wa Yanga, Boniface Mkwasa, amelia na waamuzi wa mchezo huo kwa 'kuwanyonga'.

Kwa matokeo hayo, Yanga iliyocheza mechi tisa, imefikisha pointi 18 wakati Mbeya City ambao sasa wananolewa na Amri Saidi wana pointi tisa, lakini wameshuka dimbani mara 13.

Mkwasa ambaye hiyo ni sare yake ya pili mfululizo tangu atwae mikoba hiyo kutoka kwa Mwinyi Zahera, kufuatia mchezo ulipita kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya KMC, alisema waamuzi walifunika makosa mengi ambayo yangeweza kuwanufaisha.

Akizungumza baada ya mechi hiyo iliypchezeshwa na Florentina Zablon kutoka Dodoma, Mkwasa alisema waamuzi wa aina hii ndio wanaochangia kushusha mpira wa Tanzania.

"Marefa wamekuwa kichefuchefu, namna hii mpira wetu utaendelea kushuka, nadhani mmeona wenyewe namna ambavyo matukio mengi yalifunikwa," alisema.

Refa Zablon alilamikiwa na wachezaji wa Yanga wakitaka penalti baada ya Patrick Sibomana kuonekana kama ameangushwa ndani ya 18 dakika ya 70.

Hata hivyo, kama Papy Tshishimbi angekuwa makini kuunganisha krosi ya Deus Kaseke katika dakika ya 54 Yanga ingeweza kupata bao la kuongoza.

Na katika dakika ya 58, David Molinga, alikosa bao la wazi huku dakika moja baadaye Peter Mapunda akishindwa kuiandikia goli Mbeya City baada ya kuwatoka mabeki wa Yanga.

Katika mechi hiyo iliyokuwa ya kushambuliana kwa zamu, kipindi cha kwanza kilianza huku kukiwa na mvua kubwa iliyodumu kwa dakika 10 na kusababisha maji kutuama katika baadhi ya maeneo uwanjani hapo.

Mvua hiyo, ilisababisha mpira kutokutulia na wachezaji kulazimika kucheza mipira ya juu, hata hivyo Yanga ilikuwa ya kwanza kufika langoni kwa Mbeya City lakini ilishindwa kuzitumia vema nafasi ilizotengeneza.

Kaseke alionekana kuwa msumbufu zaidi katika safu ya ulinzi Mbeya City, akihama kutoka winga ya kulia hadi kushoto na dakika ya pili tu akasababisha kona ambayo haikuzaa matunda kwa timu yake.

Licha ya mshambuliaji Mkongomani Molinga kuhaha kila kona, hakuweza kufurukuta kutokana na kuthibitiwa vema na mabeki wawili wa Mbeya City, Samson Madeleke na Baraka Johnson.

Mbeya City iliamka na kuanza kufanya mashambulizi makali langoni kwa Yanga katika dakika ya 28, 30 na 34 kupitia kwa Peter Mapunda lakini kipa Farouk Shikalo alikuwa makini kucheza hatari hizo.

Hadi kipindi cha kwanza kinamalizika hakuna timu iliyofanikiwa kukuona lango la mwenzake lakini Yanga ikipata faulo nyingi zaidi, matokeo ambayo yalidumu hadi dakika 90 zinamalizika.

Mkwasa alianza kuiongoza timu hiyo akiipa ushindi wa bao 1-0 ugenini dhidi ya Ndanda FC, halafu akashinda magoli 3-2 nyumbani dhidi ya JKT Tanzania kabla ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 CCM Kirumba dhidi ya Alliance FC.

Sare kwa Mkwasa akiipata Uwanja wa Taifa dhidi ya KMC FC kutokana na mechi kumalizika ubao wa matangazo uwanjani hapo ukisomeka bao 1-1 kabla ya sare tasa ya jana.

Mbeya City: Haruna Mandana, Keneth Kunambi, Hassan Mwasapili, Samson Madelene, Baraka Johnson, Edger Mbembela, Seleman Mangomba, George Chota, Peter Mapunda, Gamba Idd na Seleman Ibrahim.

Yanga: Farouk Shikalo, Mustafa Suleiman, Jafary Mohammed, Lamine Moro, Ally Mtoni "Sonso", Said Juma, Deus Kaseke, Papy Tshishimbi, David Molinga, Raphael Daud na Patrick Sibomana.

# Simba yapania kuendeleza dozi

**Na Somoe Ng'itu**

IKIWA na silaha zake kamili, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Wekundu wa Msimbazi, wanatarajia kuwakaribisha Lipuli FC kutoka mkoani Iringa, katika mechi ya ligi hiyo itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Katika mechi ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Arusha FC ya jijini Arusha, iliyochezwa Jumapili iliyopita, Simba iliwakosa nyota wake saba waliokuwa katika kikosi cha Tanzania Bara (Kilimanjaro Stars), ambacho kilikuwa Kampala, Uganda kwa ajili ya kushiriki michuano ya Kombe la Chalenji.

Mechi ya leo ni ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara kwa Kocha mpya, Sven Vandenbroeck na Msaidizi wake, Suleiman Matola "Veron", lakini ni ya pili katika mashindano, baada ya kupata ushindi mnono wa mabao 6-0 dhidi ya Arusha FC na kusonga mbele katika michuano hiyo.

Nahodha na kiungo wa zamani wa Simba, Matola, aliliambia gazeti hili kuwa mechi zote za Ligi Kuu Tanzania Bara ni ngumu na kikosi chao kimejiandaa kukabiliana na ushindani kwa sababu wanahitaji kupata ushindi.

Matola alisema kuwa kikosi cha Lipuli kimebadilika na kitendo cha kuifundisha timu hiyo katika msimu uliopita, haimaanishi kwamba mchezo huo utakuwa mwepesi.

"Tumejiandaa vizuri kuelekea mchezo huo, tunajua wao pia wamejiandaa na kujipanga kupata matokeo mazuri, kitu kikubwa sisi kila timu tunayocheza nayo huwa tunaiheshimu, tunaamini kuwa mambo yakienda kama tulivyojipanga, tutapata matokeo mazuri katika mechi hiyo," alisema Matola.

Safu ya ushambuliaji ya kikosi cha Lipuli ambacho kinanolewa na Kocha Mkuu, Haerman Haruna, inatarajiwa kuongozwa na straika, Paul Nonga, Seif Karihe na Daruweshi Saliboko.

"Tumefanya maandalizi mazuri, tunajua mchezo utakuwa mgumu kwa kila timu, tunajipanga kucheza kwa umakini na kutulia tutakapokuwa na mpira, Simba isitarajie mteremko, tunajiandaa kuendeleza kasi tuliyokuwa nayo kabla ya ligi haijasimama kupisha mashindano ya Kombe la Chalenji," alisema Nonga.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >